**12 MEI, 2026**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Ishirini na Saba - Tarehe 12 Mei, 2026**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Cecilia D. Paresso) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**12 MEI, 2026**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na maswali. Swali la kwanza litaelekezwa Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI. Sasa namwita Mheshimiwa Profesa Joyce Lazaro Ndalichako, Mbunge wa Kasulu Mjini, aweze kuuliza swali lake.

Na. 307

**Hitaji la Watumishi Kada ya Afya Kasulu Mjini**

**MHE. PROF. JOYCE L. NDALICHAKO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua changamoto ya uhaba wa Watumishi wa Kada ya Afya katika Halmashauri ya Mji wa Kasulu?

**MWENYEKITI:** Majibu, Naibu Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Joyce Lazaro Ndalichako, Mbunge wa Jimbo la Kasulu Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2020/2021 hadi mwaka 2025/2026 jumla ya watumishi wa kada za afya 37,921 wameajiriwa na kupangiwa vituo vya kazi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Halmashauri ya Mji Kasulu ina mahitaji ya watumishi wa Kada za afya 868 waliopo ni 343, sawa na 40% na upungufu ni watumishi 525 sawa na 60%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2025/2026 Serikali imeajiri jumla ya wataalam wa kada za afya 5,000 na kuwapanga katika

Halmashauri zenye upungufu, ikiwemo Halmashauri ya Mji wa Kasulu iliyopangiwa watumishi 31.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga bajeti na kuajiri wataalam wa kada mbalimbali za Afya na kuwapanga katika halmashauri zenye upungufu nchini ikiwemo Halmashauri ya Mji wa Kasulu, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako, swali la nyongeza.

**MHE. PROF. JOYCE L. NDALICHAKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza, ninapenda kuishukuru Serikali kwa majibu, lakini pia, ninapenda kushukuru kwa watumishi 31 ambao walipangiwa ajira katika Halmashauri ya Mji wa Kasulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majibu Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba, mahitaji ya watumishi wa afya katika Halmashauri ya Mji wa Kasulu ni watumishi 525, yaani sawa na upungufu wa 60%. Upungufu huo unaathiri utoaji wa huduma katika Hospitali ya Mlimani, Kituo cha Afya Kiganamo, Heru Juu pamoja na Nyansha na pia katika zahanati zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu kwa Serikali, je, kwa kuzingatia upungufu wa 60% ya watumishi wa kada za afya katika Halmashauri ya Mji wa Kasulu, Serikali ipo tayari katika ajira nyingine kutupangia watumishi wengi zaidi, ili waende kuimarisha huduma za utoaji wa afya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili. Hawa watumishi ambao tumepangiwa baadhi yao wameshaanza kupata uhamisho kwenda katika maeneo mengine. Je, Serikali iko tayari kuweka mfumo ambao watumishi wanapokuwa wanahama, basi tunapata watumishi mbadala, ili waweze kuendelea kutoa huduma za afya? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninampongeza sana Mheshimiwa Prof. Joyce Lazaro Ndalichako, Mbunge wa Kasulu, amekuwa mfuatiliaji wa karibu sana wa watumishi wa sekta mbalimbali, ikiwemo sekta ya afya, katika Jimbo la Kasulu Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi wameendelea kuhitajika katika maeneo mbalimbali kote nchini, na moja ya sababu ya mahitaji makubwa ya watumishi ni kutokana na kazi kubwa iliyofanywa na Serikali hii ya Awamu ya Sita, inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ya kujenga vituo vya afya kwa wingi zahanati, hospitali za wilaya na *automatically* imeongeza uhitaji wa watumishi, lakini Serikali imekuwa ikitoa kibali cha ajira kila mwaka. Hivi karibuni katika siku zile 100 za kwanza za Serikali hii ya Awamu ya Sita kipindi cha pili imeajiri watumishi wa sekta ya afya 5,000 na kuwapanga kwenye maeneo yenye uhitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeweka utaratibu, tumeainisha mikoa yote na halmashauri zote zenye upungufu zaidi wa watumishi na wakati wa vibali vya ajira halmashauri hizi, ikiwemo Halmashauri ya Kasulu Mjini, zinapewa kipaumbele kwa kupelekewa watumishi wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Prof. Ndalichako kwamba, Halmashauri ya Kasulu ni miongoni mwa halmashauri ambazo zimeainishwa kwenye halmashauri zenye upungufu mkubwa wa watumishi na itaendelea kupewa kipaumbele kupelekewa watumishi wengi zaidi kila kibali kinapotokea kuhakikisha kwamba tunapunguza *gap* la watumishi katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, kuhusu uhamisho wa watumishi. Katika ajira zinazotolewa na Serikali tumeweka masharti kwamba, mtumishi yeyote anayepangiwa kwenye kituo hatakiwi kuhama, angalau ndani ya miaka mitatu baada ya kupangiwa kituo kile, isipokuwa kama ana sababu nzito za kiafya na zile ambazo

Serikali itajiridhisha kwamba asaidiwe kwa uhamisho. Kwa hiyo, tutaendelea kuhakikisha tunasimamia suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, yako maeneo ambayo watumishi wamehamishwa kila tunapoajiri. Tutaendelea kuona tunafanya msawazo wa ndani, lakini pia kupeleka watumishi wengine katika maeneo haya, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nuru Kashakari, swali la nyongeza.

**MHE. NURU I. KASHAKARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Uvinza ina vituo vya afya viwili ambavyo vinahudumia wananchi. Kwa mfano, Kituo cha Afya Nguruka na Ilagala; Kituo cha Afya cha Nguruka kinahudumia zaidi ya wananchi 362,000, na Kituo cha Afya cha Ilagala kina hudumia wananchi 163,000. Pale kuna uhaba waz watumishi, watumishi ni wachache

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupita wananchi wanaohudumiwa katika vituo hivi, je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka watumishi wa afya kwenye maeneo haya ili kuwasaidia wananchi? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, katika Halmashauri ya Uvinza tuna hicho Kituo cha Afya cha Nguruka ambacho kwa kweli kiko katikati ya mji na kinahudumia wananchi wengi sana, na Serikali imeendelea kupeleka fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamhakikishia tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua tunahitaji kupeleka watumishi zaidi katika Kituo hiki cha Afya cha Nguruka na pia, cha Ilagala, ili kuboresha huduma. Tutahakikisha kila kibali cha ajira kinapojitokeza tunawapa kipaumbele katika vituo hivi vya afya na vingine vyewe upungufu wa watumishi, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona, Mheshimiwa Dkt. Neema Majule.

**MHE. DKT. NEEMA P. MAJULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kumwuliza Naibu Waziri kwamba, Mkoa wa Dodoma una kata 209 na vijiji 844. Serikali imejitahidi sana kujenga hospitali, vituo vya afya na zahanati, lakini tukifanya kampeni tumepita, zahanati nyingine zina mtumishi mmoja na nyingine watumishi wawili, na hivyo, imelazimika wanawake wa Dodoma wanaotaka kujifungua kwenye sehemu husika kusafiri, tena muda mrefu kwa ajili ya huduma ya kujifungua. Mheshimiwa Naibu Waziri, ni lini vituo hivi ambavyo mmejua kabisa vimejengwa vitapata watumishi? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba tunavyo vituo vya afya vingi katika Mkoa wa Dodoma, kama Mheshimiwa Dkt. Neema, alivyosema. Dhamira ya Serikali ni kusogeza karibu zaidi na wananchi huduma za afya, ili kuwapunguzia umbali wa kupata huduma hizo wananchi wengine wakiwepo akina mama wajawazito. Tufahamu kwamba vipo vituo ambavyo vina upungufu wa watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kwanza ambalo Serikali imehakikisha inalisimamia kwa karibu ni kwamba, vituo vyote vilivyojengwa vianze kutoa huduma hata kama kuna watumishi wachache. Tuhakikishe wajawazito na wananchi wengine wanaendelea kupata huduma, wakati tunaendelea kujipanga kupeleka watumishi wengine katika vituo hivi.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea. Sasa ninamwita Mheshimiwa Charles Mhando Njama, Mbunge wa Korogwe Mjini, aweze kuuliza swali lake.

**12 MEI, 2026**

Na. 308

**Ujenzi wa Vituo vya Afya Jimbo la Korogwe Mjini**

**MHE. CHARLES M. NJAMA** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa vituo vya afya Kata ya *Old Korogwe*, Kwamndolwa, Mtonga na Bagamoyo utaanza?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Charles Mhando Njama, Mbunge wa Jimbo la Korogwe Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya *Old Korogwe* ina jumla ya wakazi 8,126 ambao wanapata huduma za upasuaji katika Kituo cha Afya Majengo. Kata ya Kwamndolwa ina wakazi 5,354, wakazi wa Kata hiyo wanapata huduma kwenye Hospitali ya Magunga iliyopo kilometa 15. Kata ya Bagamoyo ina wakazi 7,945, huduma za upasuaji wanazipata kwenye Hospitali ya Magunga iliyopo kilometa 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Mtonga ina wakazi 16,300, huduma za upasuaji wanazipata kwenye Hospitali ya Magunga iliyopo kilometa 18. Kata ya Mtonga ina uhitaji zaidi ambapo ina wananchi 16,300 na wanapata huduma ya upasuaji katika hospitali ya Wilaya, umbali wa kilometa 18. Serikali itaweka mpango wa ujenzi wa kituo cha afya katika Kata ya Mtonga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeweka kipaumbele cha kukamilisha miradi viporo ya huduma za afya katika vituo vya afya 364, ili viweze kutoa huduma stahiki, zikiwemo huduma za dharura za upasuaji, ambapo mwaka 2026/2027 jumla ya vituo 111 vimetengewa

shilingi bilioni 23.37, kwa ajili ya kuongezea miundombinu muhimu. Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya Afya kwenye Kata za kimkakati zitakazokidhi vigezo katika Halmashauri ya Mji wa Korogwe, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Charles Mhando Njama.

**MHE. CHARLES M. NJAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ambayo ametupatia, lakini nina maswali mengine mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza. Kama ulivyoeleza katika majibu yako, Kituo chetu cha Afya cha Kata ya Majengo kinahudumia wananchi wengi zaidi, siyo tu wa Kata ya Majengo, kulingana na maeneo kilipo, kinahudumia watu wengi wa eneo la Jimbo la Korogwe Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata shilingi 500,000,000 ambazo zimetusaidia kuboresha sana kituo kile cha afya na sasa kimekuwa kikihudumia takribani wananchi 2,200 kwa mwezi, ambapo kinakaribia Hospitali yetu ya Magunga, lakini kituo kile kina changamoto kubwa ya *OPD*. Je, ni lini Serikali itakuwa tayari kutenga fedha, kwa ajili ya kwenda kuboresha *OPD* ya Kituo chetu cha Afya cha Majengo, ili wananchi waweze kupata huduma nzuri zaidi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili. Tuna vituo vitatu vya afya, Majengo, Mgombezi pamoja na Kwa Msisi, lakini havina *ambulance*. Je, Serikali iko tayari kuwaambia wananchi wa Korogwe Mjini, ni lini vituo hivi vya afya vitapata *ambulance* ili kurahisisha huduma pale ambapo tunapata hali ya dharura, hasa kwa akina mama wajawazito? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninampongeza sana Mheshimiwa Charles

Mhando Njama, Mbunge wa Korogwe Mjini, amewasilisha hoja hii kwa niaba ya wananchi wa Korogwe Mjini mara kadhaa. Serikali hii sikivu ya Awamu ya Sita imechukua hoja zote za Mheshimiwa Mbunge, kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, tunaboresha huduma za afya katika Jimbo la Korogwe Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kwamba, fedha iliyopelekwa Kituo cha Afya cha Majengo ambacho kinahudumia wananchi wengi imefanya kazi nzuri, lakini bado tuna upungufu wa baadhi ya miundombinu ikiwemo Jengo la *OPD*. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, ujenzi wa vituo hivi vya afya ni endelevu. Tulianza na awamu ya kwanza, tumejenga majengo yaliyopo sasa, lakini tutakwenda na awamu ya pili, kwa ajili ya kuhakikisha tunajenga majengo yanayopungua katika vituo hivyo, ili kuviwezesha kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, tunafahamu kwamba, vituo vya afya vinahitaji magari ya wagonjwa, kwa maana ya *ambulance*. Katika kipindi cha miaka miwili iliyopita Serikali imepeleka *ambulance* kwenye vituo vya afya na hospitali za wilaya katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, zaidi ya magari ya wagonjwa 500 na Serikali inaendelea kutenga fedha kwa awamu kupeleka magari ya wagonjwa kwenye Vituo vya Afya ikiwemo Kwa Msisi, Majengo na vituo vingine ambavyo vitahitaji magari ya wagonjwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona, Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa, Kata ya Didia ambayo iko Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga ni ya kimkakati, ina idadi kubwa ya watu na ni kata ambayo inazalisha sana zao la mpunga. Je, ni lini Serikali itajenga kituo cha afya katika kata hii?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa

Mwenyekiti, ahsante sana. Ninampongeza sana dada yangu, Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, amekuwa mfuatiliaji wa karibu kuhusiana na ujenzi wa kituo cha afya kwenye kata hiyo ya kimkakati katika Wilaya ya Shinyanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali inaendelea kufanya tathmini na kuainisha kata zenye idadi kubwa ya wananchi, ambazo ziko umbali mrefu kutoka vituo vya karibu kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya. Tutahakikisha tumetoa kipaumbele katika kata hiyo, ili kwa awamu tuendelee kupeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya kila kata.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asia Halamga, swali dogo la nyongeza.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Ninazipongeza jitihada za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan toka ameingia madarakani tumepata vituo vya afya karibu vinne, lakini Jimbo la Hanang lina upungufu wa vituo vya afya 24. Je, ni lini Serikali itatuongezea vituo vya afya kwa sababu, bado tuna uhitaji mkubwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile ambavyo vimekamilika kwa jitihada ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ni lini sasa tutapewa vifaatiba ili tuweze kupata huduma? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa vituo vya afya ni zoezi endelevu na ni kweli kama Mheshimiwa Asia Halamga, Mbunge wa Hanang, alivyosema. Serikali tutapeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya katika Jimbo la Hanang.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuhakikishia Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Hanang, tunaendelea kufanya tathmini na kuainisha kata za kimkakati zenye vigezo na kuendelea kutenga fedha kwa awamu, ili tuendelee kusogeza huduma za afya, lakini pia, vifaa tiba katika vituo vyetu ambavyo tunajenga katika Jimbo la Hanang na katika maeneo yote kote nchini. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam Kisangi, swali dogo la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi niulize swali la nyongeza. Kata ya Sandali katika Jimbo la Temeke ina wakazi wanaokaribia 40,000 na zaidi, lakini hakuna kituo cha afya. Je, Serikali lini itajenga kituo cha afya katika Kata ya Sandali iliyopo katika Jimbo la Temeke? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko kata ambazo zina idadi kubwa sana ya wananchi na maelekezo ya Serikali yametolewa kwa Wakurugenzi wote wa Mamlaka za Serikali za Mitaa na hususan halmashauri zile ambazo angalau zina mapato makubwa ya ndani, kama Halmashauri ya Manispaa ya Temeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, kuwakumbusha Wakurugenzi, kumkumbusha Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke na kumsisitiza kwamba, ni muhimu kufanya tathmini. Ikiwa kata hiyo inahitaji kujenga kituo cha afya kwa idadi ya wananchi waliopo na umbali kutoka kituo kingine, basi hatua za kutenga fedha za mapato ya ndani zianze na ujenzi uanze wakati Serikali kuu pia inatafuta fedha kwenda kuwaunga mkono na kukamilisha vituo hivyo vya afya.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tunaendelea. Sasa ninamwita Mheshimiwa Yohana Stephen Msita, Mbunge wa Itigi, aweze kuuliza swali lake.

Na. 309

**Ujenzi wa Vituo vya Afya Jimbo la Itigi**

**MHE. YOHANA S. MSITA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Vituo vya Afya Kata za Mgandu, Mwamagembe, Ipole na Idodyandole – Itigi?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Yohana Stephen Msita, Mbunge wa Jimbo la Itigi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha miaka mitano, Halmashauri ya Wilaya ya Itigi imepokea jumla ya shilingi bilioni 3.34 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya Halmashauri kwa shilingi bilioni 1.75, ujenzi wa vituo vya afya viwili shilingi bilioni 1.186 na ukamilishaji wa maboma ya zahanati 11 shilingi 650,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali imetoa shilingi 686,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Idodyandole, ujenzi unaendelea. Aidha, katika mwaka wa fedha 2026/2027 Serikali imetenga shilingi 800,000,000 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa miundombinu katika Hospitali ya Wilaya ya Itigi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea na ujenzi wa vituo vya afya katika Kata za kimkakati, zikiwemo Kata za Mwamagembe,

Mgandu na Ipole kwa kuzingatia vigezo na upatikanaji wa fedha, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yohana Stephen Msita, maswali ya nyongeza.

**MHE. YOHANA S. MSITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, wananchi wa Itigi wamekuwa wakijitolea kwa nguvu na mali zao katika kujenga majengo ya vituo vya afya na zahanati kama maeneo ya Mkajenga, Agondi, Matumaini na Itagata, je, Serikali haioni sasa umuhimu wa kuharakisha utoaji wa fedha ili waendelee kuwasaidia wananchi hawa katika juhudi ambazo wanaendelea kuzionesha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, je, Serikali ina mpango gani wa kujenga jengo la *X-Ray* katika Kituo cha Afya pale Itigi pamoja na kupeleka *X-Ray machine?* Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninampongeza sana sana Mheshimiwa Yohana Stephen Msita, Mbunge wa Itigi na wananchi wa Itigi kwa kuendelea kutoa nguvu zao na michango yao mbalimbali katika kuibua miradi ya ujenzi wa zahanati na vituo vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni mwongozo wa Serikali, na Serikali siku zote imekuwa ikitenga fedha kwenda kuwaunga mkono wananchi kwenye umaliziaji wa maboma ya zahanati. Katika miaka mitano iliyopita, fedha nyingi zimetolewa kwa ajili ya kukamilisha maboma ya zahanati. Serikali itaendelea kutenga fedha kwenye bajeti zake kwenda kuwaunga mkono wananchi ambao wameanza ujenzi wa zahanati kwa nguvu zao katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Msita kwamba tutahakikisha pia tunatoa kipaumbele kwenye maboma ambayo yameanzishwa na wananchi katika Jimbo la Itigi katika ukamilishaji wa zahanati hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, tunafahamu katika vituo vyetu vya afya ni muhimu kuwa na majengo ya *X-Ray*, lakini pia na mashine zenyewe za *X-Ray*. Serikali imeendelea kujenga majengo ya *X-Ray* kwa awamu na tutaendelea pia kupeleka mashine hizi ili kuboresha vipimo katika vituo vya afya kikiwemo kituo hicho cha afya ambacho Mheshimiwa Mbunge amekitaja.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Zuberi Mfaume, swali dogo la nyongeza.

**MHE. ZUBERI Y. MFAUME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza, niipongeze Serikali kwa kasi ya kujenga vituo vya afya nchi nzima. Pia, nina swali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Kibogwa iliyopo katika Jimbo la Morogoro Kusini ni kata iliyoko milimani na ina mito mikubwa ya kuvuka na wanapaswa kusafiri umbali wa kilomita 50 kufikia vituo vya afya. Je, Serikali ina mpango gani sasa kupeleka kituo cha afya katika Kata ya Kibogwa? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilishaweka mpango mkakati wa kuainisha maeneo ambayo yana idadi kubwa ya wananchi na Kata ambazo ziko maeneo ya mbali zaidi kutoka kituo cha karibu kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge anasema, kilomita 50, na pia hali ya kijiografia ya maeneo husika kama visiwa, milimani na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo haya kwa kawaida yanapewa kipaumbele zaidi kujenga vituo vya afya ili kusogeza huduma karibu na wananchi. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tumepokea hoja hiyo, tutafanya mawasiliano na Halmashauri ya Morogoro ili kuweza kuona kama Kata hiyo inakidhi vigezo tuanze kuiweka kwenye mipango yetu ya mapato ya ndani ya halmashauri na Serikali Kuu kwa ajili ya kuendelea kutenga fedha kwa awamu kwa ujenzi wa kituo cha afya.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Edifonsi  Kanoni, uliza swali lako la nyongeza.

**MHE. EDIFONSI J. KANONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza. Jimbo la Kalambo katika Kijiji cha Msishindwe, Tiangoma, Rolesha, Mpombwe, Nondo, Musoma, Kafukoka, Mikonko, Kalembe, Panga, Kiundilamema, Kitwanga, Mnamba pamoja Tunyi ni vijiji ambavyo wananchi wamejenga vituo vya afya kufikia usawa wa *lenta*. Ni nini mpango wa Serikali wa kutenga bajeti kwa ajili ya kukamilisha hizo zahanati ili wananchi waandelee kunufaika na huduma ya afya? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mheshimiwa Kanoni alishawasilisha orodha ya maboma ya zahanati ambayo yanahitaji umaliziaji. Nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Jimbo la Kalambo kwa kutoa michango yao na kuanza ujenzi wa maboma ya zahanati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie tu kwamba tutaendelea kutenga fedha kwa awamu kuwaunga mkono wananchi katika juhudi zao kukamilisha maboma ili kuanza kutoa huduma katika vijiji ambavyo amevitaja ambavyo tayari vina maboma ya zahanati.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana. Kijiji cha Kisana kuna zahanati ambayo imejengwa zaidi ya miaka 12 iliyopita katika Kata ya Kyebitembe katika Jimbo la Muleba Kusini. Je, Serikali ina mkakati gani kumaliza maboma ambayo yana miaka zaidi ya 10 bila kutumika na wananchi walitoa nguvu zao katika ujenzi wa maboma hayo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika kipindi cha miaka mitano iliyopita ilipeleka zaidi ya shilingi 25,000,000,000 kwenye Halmashauri na Majimbo yetu kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi. Kigezo ambacho kilikuwa kinatumika kimojawapo kilikuwa ni maboma yale ambayo yamejengwa muda mrefu zaidi kupewa kipaumbele kupelekewa fedha kukamilika na kuanza kutoa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Kikoyo kwamba maboma hayo ambayo yana muda mrefu, bado yako kwenye mpango Serikali na Serikali inaendelea na taratibu za kibajeti na kupeleka fedha kwa ajili ya ukamilishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitoe wito kwa Halmashauri kwa yale maboma ambayo yamekaa muda mrefu na yako ndani ya uwezo wa mapato ya ndani ya halmashauri waendelee pia kutenga fedha kwa awamu kila mwaka wa fedha kwa ajili ya ukamilishaji ili kusogeza huduma karibu zaidi na wananchi.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kata ya Kenyamanyori ni Kata iko nje ya Mji wa Tarime na wananchi wanapata adha kubwa sana kuja kupata huduma kwenye Hospitali ya Mji wa Tarime na miundombinu ya barabara siyo rafiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, wananchi wameshaanza kujenga kituo cha afya na hata Mfuko wa Jimbo tulipeleka fedha pale, Serikali inaweka juhudi gani za dharura kuhakikisha kwamba inapeleka fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa kituo cha afya kwenye Kata ya Kenyamanyori?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti. Ninawapongeza sana wananchi wa Jimbo la Tarime Mjini na Mbunge wa Jimbo hili, Mheshimiwa dada Esther Matiko kwa kuhamasisha wananchi kuanza ujenzi wa kituo cha afya katika kata hiyo ambayo ipo pembezoni na mbali kutoka vituo vya afya vya jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tumepokea hoja hiyo, lakini nitumie nafasi hii pia kumsisitiza Mkurugenzi kuona uwezekano wa kuanza kutenga fedha angalau kidogo kwa mapato ya ndani wakati sisi Serikali Kuu tunaendelea na kuandaa fedha kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa vituo hivyo vya afya.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea. Sasa ninamwita Mheshimiwa Haiderali Hussein Gulamali, Mbunge wa Ilongero, aulize swali lake.

Na. 310

**Ujenzi wa Soko la Vitunguu Merya**

**MHE. HAIDERALI H. GULAMALI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Soko la Vitunguu Njia panda ya Merya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Haiderali Hussein Gulamali, Mbunge wa Jimbo la Ilongero, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua uhitaji wa soko la vitunguu katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida. Kutokana na uhitaji huo, Halmashauri iliandaa andiko mradi lenye thamani ya shilingi bilioni 2.9. Mwezi Septemba, 2024 Halmashauri ya Wilaya ya Singida iliwasilisha andiko Wizara ya Kilimo kwa ajili ya kuomba ushirikiano katika utekelezaji wa mradi huu. Wizara ya Kilimo iliridhia ombi hilo ambapo ujenzi wa soko hili utafanyika kwa ushirikiano kati ya Halmashauri ya Wilaya ya Singida na Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua iliyofikiwa kwa sasa ni kuandaa mkataba wa makubaliano kuhusu namna mradi utavyotekelezwa na pande zote mbili. Mara baada ya makubaliano hayo kukamilika, taratibu za ujenzi zitaanza rasmi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Haiderali Hussein Gulamali, maswali ya nyongeza.

**MHE. HAIDERALI H. GULAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyokiri Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba kutoka mwaka 2014 hadi sasa ujenzi huo haujatimia masuala ya mkataba na kadhalika yanaendelea, nimhakikishie kwamba mimi binafsi nitafuatilia na nitaleta nakala ya huu mkataba ofisini kwake ili mara moja atuhakikishie kwamba baada ya kupokea zoezi hili la ujenzi lianze mara moja, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Bila shaka maoni yako yamepokelewa. Tunaendelea, sasa ninamwita Mheshimiwa Lucy Mayenga aweze kuuliza swali dogo ya nyongeza.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Songwa ina akina mama ambao ni wachapakazi sana ambao wamejituma kwa muda mrefu kulima kilimo cha nyanya. Je, ni lini Serikali na hasa Mheshimiwa Naibu Waziri atakuja Kata ile ya Songwa kipindi cha msimu aone jinsi akina mama wale chini ya Diwani wao Mheshimiwa Ngolomole wanavyohangaika na masoko ili aweze kufikiria kujenga soko la nyanya katika eneo hilo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana dada yangu Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mbunge wa Jimbo la Kishapu. Ninakumbuka suala hili alishaliwasilisha Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, na sisi tumeendelea kuwasiliana na Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu kuanza kuandaa michoro na makadirio ya gharama ili kuanza kutenga fedha ya mapato ya ndani wakati tunasubiri fedha za kutoka Serikali Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba moja ya vipaumbele vya Serikali ni kuboresha maeneo ya kufanyia biashara ya wajasiriamali wodogo wadogo ili kuhakikisha kwamba wanastawi kiuchumi na tutahakikisha kwamba tunaendelea kufanya hivyo katika maeneo yote likiwemo Jimbo la Kishapu.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Emmanuel Khambay, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL J. KHAMBAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Mji wa Babati ni mji ambao unakua kwa kasi. Je, ni lini Serikali itatoa shilingi 5,000,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa soko la kisasa kwa ajili ya Halmashauri ya Mji wa Babati?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mji wa Babati ni moja ya mji ambao iko kwenye mradi wa *TACTIC* wa Miji 45 na ninafahamu kuna miundombinu kadhaa ambayo inatarajiwa kujengwa katika Mji wa Babati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Khambay, Mbunge wa Jimbo la Babati Mjini, kwamba Serikali iko kwenye hatua nzuri za kutekeleza miradi hiyo kuhakikisha kwamba tunajenga masoko, barabara lakini na miundombinu mingine ili Mji wetu wa Babati uendelee kuwa Mji wa kisasa na bora zaidi kwa maslahi ya wananchi.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Mwita Waitara, swali dogo la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Kuna masoko madogo madogo ya Halmashauri zetu ambapo Halmashauri zinakusanya kodi, lakini hakuna vyoo katika maeneo hayo hali inayopelekea kuchafua mazingira. Serikali inaweza ikatoa agizo kwa Wakurugenzi nchi nzima, kila palipo na mkusanyiko wa kufanyia biashara na wanakusanya kodi wachimbe vyoo na kuweka maji ili kutimiza usafi? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni wajibu wa Halmashauri zetu yale maeneo yote ambayo yana masoko ni lazima yawe na miundombinu yote muhimu ya kiafya na huduma za kijamii katika maeneo hayo. Mojawapo ni kuwa na vyoo, maji na miundombinu mingine muhimu ya msingi na wezeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, kuwasisitiza

Wakurugenzi wote kwamba ni lazima kila soko ambalo lina mkusanyiko wa wananchi wahakikishe miundombinu ya vyoo ipo, maji yanapatikana na ule ushuru ambao wanaukusanya katika maeneo hayo iwe ni sehemu ya fedha inayorejea kuboresha miundombinu ile ili wananchi waweze kufanya kazi katika mazingira bora, lakini pia kuepusha uwezekano wa milipuko ya magonjwa katika maeneo ya masoko.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea. Sasa ninamwita Mheshimiwa Dkt. Charles Wilson Mahera, Mbunge wa Butiama, aulize swali lake.

Na. 311

**Ujenzi na Ukarabati wa Barabara za Jimbo la Butiama**

**MHE. DKT. WILSON C. MAHERA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza na kukamilisha utekelezaji wa ujenzi na ukarabati wa barabara katika Jimbo la Butiama?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Wilson Mahera Charles, Mbunge wa Jimbo la Butiama, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya aya Butiama ina mtandao wa barabara wa kilometa 596.62 unaohudumiwa na Wakala wa Barabara Vijijini na Mjini. Serikali imekuwa ikitenga bajeti ya matengenezo, ukarabati na ujenzi wa barabara mbalimbali ambapo bajeti ya Wilaya imeendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Wilaya ya Butiama limeidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 2.59 kwa ajili ya matengenezo na ukarabati wa barabara maeneo korofi yenye urefu wa Kilometa 145.32 na ujenzi wa madaraja 14 pamoja na makalavati 26. Kazi hizi baadhi yake zinaendelea kutekelezwa maeneo mbalimbali ya Jimbo la Butiama ambapo kiasi cha shilingi 722,649,050 kimepelekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2026/2027 Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 2.74 kwa ajili ya Wilaya ya Butiama kwa ajili ya matengenezo na ukarabati wa barabara maeneo korofi yenye urefu wa Kilometa 155.42 na ujenzi wa madaraja 17 na makalavati 29.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa ujenzi na ukarabati wa barabara za wilaya ya Butiama ili kuwawezesha wananchi kuendelea na shughuli za kiuchumi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Wilson Mahera, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. WILSON C. MAHERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, wananchi wa Kata ya Kyanyari na Kata ya Masaba inayounganishwa na Jimbo la Bunda hawana barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imejenga daraja pale lakini wamekuwa wakisubiri kwa muda ili kuweza kupata barabara ili tuweze kuungana kati ya Bunda na Butiama. Vilevile ukija kwenye Kata ya Kyanyari unaungana na Musoma Vijijini pia hakuna muunganiko, kuna barabara inayokwenda Wanyere, daraja lina hali mbaya sana na limetengeneza bwawa. Kwa hiyo, ningependa kwa kweli katika bajeti hii fedha ziende ili kusudi barabara hizo mbili ziweze kupitika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ni kwamba wananchi wa Kata ya Sirorisimba pamoja na Buswahili hawana muunganiko mzuri na wamekuwa wakisubiria barabara mpya mbayo inatakiwa

kujengwa kati ya Kijiji cha Nyambili, inapita Nyandewa kwenda Buswahili. Ninaamini kwamba tumetenga kwenye bajeti lakini kutenga bajeti ni jambo moja na kupeleka fedha ni jambo lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wamekuwa wanasubiri barabara hiyo kwa muda mrefu sana. Ninaomba kujua, je, barabara hiyo wakati huu itafunguliwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Wilson Charles Mahera, Mbunge wa Butiama, amekuwa Mbunge madhubuti na imara na anafuatilia sana ustawi wa wananchi wa Jimbo la Butiama. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Butiama kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, itaendelea kukupa ushirikiano kuhakikisha tunaboresha huduma za barabara katika Jimbo la Butiama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba ziko Kata ambazo hazijaunganishwa na kata nyingine katika Jimbo la Butiama na Serikali inaendelea kwa awamu kutenga fedha kwa ajili ya kufungua barabara nyingine, lakini pia kuziingiza kwenye mtandao unaohudumiwa na *TARURA* ili ziweze kupata bajeti kila mwaka kwa ajili ya matengenezo na ukarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge barabara hizo alizozitaja ambazo tayari alishawasilisha Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI. Tutaendelea kutenga fedha kwa awamu kuhakikisha kwamba zinatengenezwa, zinafunguliwa na zinaendelea kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili tunafahamu kwamba katika barabara ambazo zimeathiriwa na mvua, mojawapo ni barabara katika Jimbo la Butiama. Tayari *TARURA* Mkoa wa Mara na Wilaya ya

Butiama na Mheshimiwa Mbunge wameshaleta maombi ya shilingi bilioni 1,382 kwa ajili ya ukarabati wa barabara ya Buturi, Chuo cha Mwalimu Nyerere, Chifu Ihunyo, Kiwazaru, Kyatungwe, *Mwibagi Store*, Nyakiswa, Mang'atika, Rwamkoma, Kiabakari, Kamugegi, Mirwa na Sirorisimba. Maeneo hayo yote pamoja na hayo uliyoyataja tayari tuko kwenye hatua za kupeleka fedha kwa ajili ya kuanza ukarabati wa barabara hizo.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Bakari Shingo, swali la nyongeza.

**MHE. BAKARI B. SHINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninataka nifahamu kwamba Serikali ina mpango gani juu ya daraja la Kata ya Ukonga maeneo ya Saba Saba kuelekea Mongo la Ndege ambalo wakati wa mtangulizi wangu Mheshimiwa Jerry Serikali iliwahi kutembelea na ikaona umuhimu wa kulijenga tena daraja lile ambalo lilisombwa na maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, nilitaka nilifahamu pia Serikali ina mpango gani...

**MWENYEKITI:** Swali la nyongeza ni moja.

**MHE. BAKARI B. SHINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inafahamu kwamba katika Jimbo la Ukonga tunalo daraja ambalo linahitajika katika eneo ambalo linaunganisha Ukonga kwenda Mongo la Ndege. Pia ni kweli kwamba Serikali ilishafika pale na kufanya tathmini na kuona gharama zinazohitajika kwa ajili ya ujenzi wa daraja lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Ukonga kwamba Serikali bado ina mpango ule

na dhamira ile. Kinachoendelea sasa ni utaratibu wa kibajeti ili mapema iwezekanavyo twende tukaanze ujenzi wa daraja lile baada ya kuweka vizuri masuala ya kibajeti.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, swali dogo la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Barabara ya Msonza, Kimara inapita Magome, Ndengisivili mpaka Kimara, lakini barabara hii inaunganisha Kata tatu na barabara zake hazipitiki kabisa. Wananchi wanabebwa kwa machela kupelekwa kwenye vituo vya afya na hawana vituo vya afya. Je, lini Serikali itaona umuhimu ili barabara hii ijengwe, wananchi waweze kufika katika vituo vya afya salama?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo barabara ambazo hazipitiki kutokana na athari ya mvua nyingi katika mwaka huu. Serikali imeshatoa maelekezo kwa Mameneja wa *TARURA* mikoa na wilaya kote nchini kwamba maeneo ambayo ni korofi na yanaathiri kupitika kabisa kwa barabara zile, ambayo ndani ya muda huu tunaweza kufanyia matengenezo pamoja na hali ya hewa ya mvua kuendelea, Mameneja watoe kipaumbele, wafike katika maeneo hayo wafanye tathmini na kufanya jambo linalowezekana kuwezesha wananchi waendelee kupita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, zile barabara ambazo zinawezekana kutengenezwa Serikali tutahakikisha tunafanya matengenezo ili wananchi waendelee kupita. Vilevile tutaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunatengeneza barabara hizo kwa ubora mkubwa zaidi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Khalid Nsekela, swali dogo la nyongeza.

**MHE. KHALID M. NSEKELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru. Barabara ya Nkwenda, Kakanja, Kimuli hadi Mabira ni barabara kiungo kikubwa sana katika shughuli za uchumi kwa Jimbo la Kyerwa. Je, Serikali ina mpango gani wa kuikarabati na kuijenga ili shughuli hizo ziendelee?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo barabara ambazo orodha yake tumeshazipokea kwa ajili ya ukarabati na ujenzi katika halmashauri mbalimbali, likiwemo Jimbo la Kyerwa. Pia zipo barabara ambazo tunaendelea kuzifanyia tathmini kwa ajili ya kuzifungua kwa maana ya barabara mpya kulingana na mahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, barabara hizo ambazo tayari zipo kwenye jimbo letu na zipo kwenye mtandao huo unaohudumiwa na *TARURA*, tutaendelea kuzitengea fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Serikali inaendelea na tathmini za mwisho za athari ya mvua kwenye barabara hizo ili fedha ianze kutengwa na kupelekwa kwa awamu kwa ajili ya kufanya marekebisho; na tutahakikisha pia barabara hiyo ya Mheshimiwa Mbunge tunaipa kipaumbele.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Elinikyo Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Sonu-Sawe kilomita sita, imekuwa barabara korofi sana, na kipindi hiki cha mvua haipitiki kabisa ilhali ndiyo barabara inayotumika kusafirisha mazao kama ndizi ambazo tunazitumia hapa Dodoma. Je, ni lini sasa Serikali itajenga barabara hii ili iweze kupitika?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tulishakubaliana, na tumeweka mpango Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kupitia *TARURA* kwamba kweli katika nchi yetu zipo barabara ambazo ni korofi mara nyingi. Kila mwaka msimu wa mvua zinakuwa korofi, zinaharibika kutokana na hali ya hewa na hali ya kijiografia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshakubaliana, kwanza, kuja na *design* ya aina ya barabara ambazo zitadumu zaidi katika maeneo yenye mvua nyingi, milima na hali za kijiografia ambazo zinaathirika kirahisi na mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tunaendelea na utaratibu huo, na tutakapofika hatua ya kuwa na *design* ambayo tunaitekeleza, tutahakikisha barabara hiyo tunaiingiza kwenye *design* maalum ambayo itawezesha kukomesha kuharibika kila mwaka na kuitia hasara Serikali na wananchi. Kwa sasa tutaendelea kuifanyia matengenezo ya muda ili iendelee kupitika na kutoa huduma kwa wananchi wa Jimbo la Hai.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi na Mheshimiwa Naibu Waziri tunapakana jimbo, na anafahamu kwamba majira haya mvua zimesimama. Kwa hiyo, wakandarasi wanatakiwa waingie *site*. Kwa Makete tuna barabara ya kutoka Ibaga kuelekea Mang'oto, Barabara ya Ukwama – Ihanga, Barabara ya Kinyika - Kikondo, na Barabara ya Ikuwo kule. Je, ni lini wakandarasi wataanza kujenga barabara hii, na hasa ukijua kwamba Serikali imeshatoa fedha na tayari wameshasaini makataba?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Festo Sanga ni jirani yangu, ninapakana naye katika Jimbo la Wanging'ombe. Ninafahamu kwamba anasimamia kwa karibu sana suala la barabara katika Jimbo la Makete, na Jimbo la Makete ni moja ya majimbo yenye mvua nyingi na hali yake ya kijiografia ni milima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekubaliana kwamba *TARURA,* Mkoa wa Njombe na Wilaya ya Makete, kwanza, tuendelee kuboresha aina ya barabara zinazojengwa, lakini pili, tuhakikishe kwamba wale wakandarasi wote ambao wamesaini mikataba na tayari wapo *site,* waendelee na kazi na kumaliza kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wale ambao hawajaenda *site,* nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kumwelekeza Meneja wa *TARURA* Mkoa wa Njombe na Meneja wa *TARURA* Wilaya ya Makete wafuatilie kwa haraka iwezekanavyo kuhakikisha kuwa wakandarasi wote wanakwenda *site* kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizo kadiri ya mikataba na barabara zikamilike kwa wakati. Sisi tutafuatilia kuona utekelezaji wa barabara hizo.

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea, na sasa ni Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. Ninamwita Mheshimiwa Suleiman Mohamed Rashid, Mbunge wa Mwela, aulize swali lake.

Na. 312

**Kero za Muungano Zilizotatuliwa**

**MHE. SULEIMAN MOHAMED RASHID** aliuliza: -

Je, kero ngapi za Muungano zimetatuliwa mpaka sasa?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Suleiman Mohamed Rashid, Mbunge wa Mwera, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha kwanza cha Serikali ya Awamu ya Sita, Serikali imefanikiwa kutatua na kupatia ufumbuzi jumla ya hoja 15 kati ya hoja 18 za Muungano zilizokuwa zikijadiliwa na pande zote mbili za Muungano. Hivyo, kuondolewa kwenye orodha ya hoja za Muungano zilizokuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Suleiman Mohamed Rashid maswali ya nyongeza.

**MHE. SULEIMAN MOHAMED RASHID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niipongeze Serikali kwa hatua ambayo imefikia. Pia ninampongeza pia Naibu Waziri kwa majibu ambayo ameweza kutupatia. Nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Je, ni faida gani ambayo imepatikana baada ya utatuzi wa hoja 15 kati ya hoja 18?

(b) Je, ni mikakati gani ya Wizara ambayo imejipangia kuhakikisha hoja tatu ambazo zimebakia tunazitatua kabla 2030?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Suleiman Mohamed Rashid, amekuwa ni mfuatiliaji mzuri sana wa masuala haya ya Muungano, yeye pamoja na Wabunge kutoka Zanzibar pamoja na Wabunge wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2006 aliyekuwa Rais wetu, Mzee wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete alitoa maelekezo ya kubadilisha namna ya kufanya majadiliano kuhusu hoja za Muungano. Hivyo, ilipelekea kuundwa kwa Kamati ya pamoja ambapo Kamati hii imeleta ufanisi mkubwa sana katika kushughulikia hoja za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2006 hadi leo Kamati hii imepokea hoja 25, na katika hizo imeshashughulikia hoja 23 na kuzibakiza hoja mbili. Kwa hiyo, huo ulikuwa ni mkakakati mkubwa ndani ya Serikali wa kuhakikisha tunaweka mazingira mazuri ya kuondoa hoja hizi kwenye hoja za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ndani ya Serikali tumeendelea kupitia timu mbalimbali za wataalamu kufanya mapitio ya sheria, mapitio ya kisera pamoja na kuandaa nyaraka mbalimbali kwa ajili ya kuiwezesha Kamati hii ya pamoja kufanya maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kamati hii ya pamoja kiutaratibu ambao tumeuweka inaongozwa na Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge ametaka pia kufahamu faida ambazo zimepatikana kwa kuondosha hoja hizi za muungano ambazo zimekwisha fanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazitaja chache kwa sababu ni nyingi. Kwanza, ushiriki wa Zanzibar kwenye masuala ya Kimataifa na kikanda umekuwa bayana. Nafasi ya Zanzibar inaonekana kwa dhahiri katika ushiriki huo, katika kuandaa hoja na kuandaa msimamo wa pamoja

kama nchi kwenye makubaliano ya Kimataifa tunapokuwa tumewasilisha hoja au kuhudhuria mikutano hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tumeweka utaratibu mzuri wa shughuli za uvuvi kwenye ukanda wa uchumi wa bahari kuu. Tumeweka miongozo ambayo inaondoa migongano isiyokuwa ya lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile wafanyabiashara kutoka Zanzibar wameondolewa mzigo wa kulipa kodi mara mbili. Kodi ya mapato *(Pay as You Earn)* pamoja na Kodi ya Zuio *(Withholding Tax)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vivyo hivyo, kupitia kamati hii ya pamoja tumepelekea kuondoa hoja iliyokuwa ikitupa mkanganyiko katika mikopo ya Kimataifa inayohitaji dhamana na ile isiyohitaji dhamana ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Maji, na sasa ninamwita Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini, aulize swali lake.

Na. 313

**Mradi wa Maji – Mji Mdogo wa Kifanya**

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa mradi wa maji kwenye Mji Mdogo wa Kifanya katika Kata ya Kifanya?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Jimbo la Njombe Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kuwa utekelezaji wa miradi ya maji nchini unakamilika ili kuweza kuboresha huduma ya maji kwa wananchi wake. Mradi wa maji kwa ajili ya kuhudumia miji Mji Mdogo wa Kifanya uliopo Wilaya ya Njombe umefanyiwa usanifu na kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa kazi zinazotarajiwa kutekelezwa kupitia mradi huo ni pamoja na ujenzi wa kidakio *(intake)*, ujenzi wa tanki la chini *(sump well)* ujazo wa lita 100,000 pamoja na tanki la kuhifadhia maji lita 300,000 na ujenzi wa vituo vya kuchotea maji vitano. Mradi unalenga kunufaisha zaidi ya wakazi 5,484 waishio kwenye Mji Mdogo wa Kifanya uliopo katika Wilaya ya Njombe Mkoani Njombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha za kuanza utekelezaji wa mradi huo unaotarajia kugharimu zaidi ya shilingi bilioni 4.638.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika maswali ya nyongeza.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, na ninashukuru kwa majibu ambayo nimeyapata. Hata hivyo, ninasikitika kwamba mradi huu ni wa siku nyingi sana. Mradi huu ni ahadi ya Marehemu Mheshimiwa Rais Magufuli; ni ahadi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais, alipopita na Mawaziri wawili wa Maji waliopita, Mheshimiwa Mbarawa akiwepo. Je, ni lini mradi huu utatekelezwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Tuna mradi mwingine wa Igongwi ambao nao ni wa muda mrefu. Ni mradi ambao umekamilika kwa 90% lakini hakuna maji. Je, ni lini mradi huu wa Igongwi unaokwenda kwenye kata zaidi ya nne utakamilishwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninamshukuru sana Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini kwa kazi kubwa ya kuendelea kuwasemea Wananjombe Mjini na kwa kazi kubwa ya kutoa ushirikiano kwa Wizara ya Maji. Hivi karibuni Mheshimiwa Mbunge ameongelea miradi hii, na amefanya mazungumzo na Mheshimiwa Waziri wa Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua kama Serikali mradi huu wa kifanya ni ahadi za viongozi wa Kitaifa; na ahadi za viongozi wa Kitaifa ni lazima zitekelezwe. Sisi kama Serikali kupitia Wizara ya Maji ninamwahidi Mheshimiwa Mbunge, kwa sababu *feasibility study* imekamilika, usanifu wa kina umefanyika na sasa tumesha-*establish* gharama ambazo ni shilingi bilioni 4.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba mradi huu tutaanza kutekeleza kwa awamu na kwa kufanya *rescoping* ili kuhakikisha kwamba usisimame kama ambavyo amesema kwamba ni ahadi ya zamani ya viongozi wa Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swali la pili, kuhusu mradi wa Igongwi, ni kweli kabisa mradi huu ambao una gharama ya shilingi bilioni 4.8 umefikia takribani 90% ya utekelezaji wake. Tunatambua kwamba bado kuna mahitaji ya fedha. Kazi kubwa iliyokuwa imefanyika zaidi ni kuweka mabomba takribani kilomita 60 na sasa tuko katika hatua za mwisho. Kinachohitajika ni shilingi 200,000,000 ili mradi huu uweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba ndani ya miezi hii tutapeleka fedha milioni 200 ili kwenda kuhakikisha kwamba mradi huu unakamilika kwa sababu umefikia hatua nzuri za utekelezaji. Lengo ni kwamba uanze kutoa matokeo na wananchi wapate huduma ya maji safi na salama.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Sylvia Sigula, swali dogo la nyongeza.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya Mheshimiwa Rais ni kuwatua ndoo wanawake wa Tanzania na kuwapa tabasamu, lakini hali ya upatikanaji wa maji katika Mji Mdogo wa Namanyere ulioko Wilaya ya Nkansi, Mkoa wa Rukwa ni duni sana na kumekuwa na ahadi za viongozi wengi lakini mpaka sasa changamoto ni kubwa. Kwa kuwa tumepitisha bajeti, je, ni lini tatizo hilo litatatuliwa?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na nimshukuru sana dada yangu Mheshimiwa Sylvia kwa kuendelea kuwasemea wananchi wa Katavi na Rukwa, kwa sababu ni eneo ambalo linapitiwa na Ziwa Tanganyika; pia tunatambua kuna maeneo ambayo bado yana changamoto, hasa Mji Mdogo wa Namanyere ambapo pia tulikuwa na miradi iliyokuwa inaendelea, lakini haikukamilika vizuri na hasa kwenye hili suala la Mji Mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imepanga mpango wa kuhakikisha kwamba tunaenda kutatua, na Mheshimiwa Mbunge ameshiriki kutupitishia bajeti yetu ya maji ya shilingi trilioni 1.102, na ya maendeleo ambayo imeongezeka kwa takribani shilingi 205,000,000,000. Hii ni ishara kwamba Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imedhamiria kwenda kuhakikisha kwamba tunaenda kutatua changamoto za maji, hasa katika Mji wa Namanyere. Nimtoe hofu, tunaenda kulipa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, alisema kwamba kipaumbele cha Wizara kwa sasa ni kwenda kuhakikisha kwamba miradi viporo vyote tunaenda kuvimaliza, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea. Sasa ninamwita Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda aulize swali lake.

Na. 314

**Ujenzi wa Mabwawa ya Maji Bunda**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa mabwawa ya maji Mihingo, Tingirima, Salama, Lakana, Kambubu na Nyaburundu?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Jimbo la Bunda kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekamilisha ujenzi wa Bwawa la Mihingo lililopo Wilaya ya Bunda Mkoani Mara, ambapo lina uwezo wa kuhifadhi maji lita milioni 207.145. Aidha, katika mwaka wa fedha 2026/2027 Serikali itafanya mapitio ya usanifu wa kina kwa mobwawa ya Tingirima, Salama A, Lakana, Kambubu na Nyaburundu, ili kupata gharama halisi na kazi zitakazotekelezwa katika mabwao hayo, kwa kuwa usanifu wake umepitwa na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya usanifu wa mabwawa hayo kukamilika, Serikali itatafuta fedha za kuanza utekelezaji wa mabwawa husika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, maswali ya nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe tu, wakati maswali yanapojibiwa hapa Bungeni, hatujibiwi sisi Wabunge, wanajibiwa wananchi. Kama hili suala la Mihingo kwamba anasema limekamilika, mimi ninamheshimu sana Mheshimiwa Waziri. Je, ni lini sasa ataenda Mihingo, mimi na yeye ili tukutane na wataalamu wake waliomwandikia mambo hayo ili tujue kwamba hili jambo limekamilika au bado?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Haya mabwawa yamekuwepo toka 2017/2018, na nilikaa na Wizara nzima Waziri akiwa Mbarawa, Bwira akiwepo. Wakatembelea jimbo zima kwenye vijiji 30 vya Tarafa ya Chamliho, wakasema mabwawa sita haya tutayachimba, upembuzi yakinifu ukafanyika. Je, ni lini sasa haya mabwawa yatachimbwa ili wananchi wale ambao walipisha maeneo yao ili waweze kupata maji?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa, na mimi ninampongeza kwa kazi nzuri anayoifanya na hasa kwa kufuatilia miradi inayotekelezwa ndani ya jimbo lake, na kwa kuendelea kuwasemea akina mama na kuendelea kuunga mkono falsafa ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kumtua mama ndoo kichwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kabisa kwamba Serikali ipo tayari kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge kwenda jimboni kwake na kuhakikisha kwamba tunatembelea Bwawa hili la Mihingo. Mimi nitakuwa mtu wa kwanza kumpa ushirikiano kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji. Baada ya Bunge hili la bajeti niko tayari kwenda mpaka Bunda ili tukajionee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema, haya mabwawa ambayo ameongelea *feasibility study* ilifanyika, *detail design* ikafanyika, ni mwaka 2016/2017. Kwa kawaida katika utekelezaji wa miradi ya maji, muda ukishapita, kuanzia miaka mitano, ni lazima tufanye mapitio ya ule usanifu ili tu-*establish*

gharama halisi ili tuweze kwenda kutekeleza kulingana na mabadiliko ya ongezeko la watu na mabadiliko ya kifedha ya gharama ya manunuzi ya vitu ili tuhakikishe kwamba mradi huu tukishaanza kutekeleza tunaenda kuutekeleza katika uhalisia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluh Hassan kwa sababu ya ununuzi wa mitambo ya kuchimbia mabwawa. Nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge, baada ya kufanya mapitio ya hii miradi ambayo iko katika jimbo lake, tutakwenda kutumia mitambo ambayo Mheshimiwa Rais aliinunua kwa ajili ya kuchimba mabwawa ili sasa ifikie mwisho wa huu mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatambua kwamba umekuwa mradi wa muda mrefu, lakini nimtoe hofu kwamba sasa tunaenda kuhakikisha tunafikia mwisho katika hili.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Mashimba Ndaki. Swali dogo la nyongeza.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninawapongeza sana Wizara ya Maji kwa kutekeleza miradi mingi kwenye Jimbo la Maswa Magharibi. Tatizo ni moja tu, mkandarasi aliyejenga mradi wa maji Kata ya Zanzui, Kata ya Mwamashimba na anayejenga mradi wa maji Kata Malampaka hawajalipwa fedha zao. Ni lini fedha zao hawa wakandarasi watalipwa ili mkandarasi wa mradi wa Malampaka aweze kuendelea na kazi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na nimshukuru sana na kumpongeza sana kaka yangu Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Jimbo la Maswa Magharibi. Ni kweli kabisa tunayo madai mengi ya wakandarasi, lakini tunajaribu kupitia pia zile hati za madai na kujiridhisha na kazi ambayo imefanyika kule *site*. Baada ya kujiridhisha sasa Serikali inaandaa malipo kwa ajili ya kumlipa mkandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge, hili tunaenda kulipa kipaumbele kuhakikisha kwamba mkandarasi huyu analipwa kwa haraka iwezekanavyo ili aweze kuendelea kuutekeleza mradi huu na ukatoe matokeo chanya ambayo yanatokana na sauti kubwa na ya kutosha ya mwakilishi wa Maswa Magharibi. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa tunaendelea, sasa ni Wizara ya Nishati. Ninamwita Mheshimiwa Hasnain Gulamabbas Dewji, Mbunge wa Kilwa Kusini, aulize swali lake.

Na. 315

**Maendeleo ya Uchimbaji wa Gesi Asilia Songo Songo**

**MHE. HASNAIN G. DEWJI** aliuliza:-

Je, mpaka sasa Visima Vingapi vya Gesi Asilia Vimechimbwa katika Kisiwa cha Songo Songo, na upi mpango wa kuongeza uzalishaji wa gesi?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Hasnain Gulamabbas Dewji, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kitalu cha Songo Songo kina jumla ya visima 12 ambapo Serikali kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania *(TPDC*) imechimba visima tisa na Kampuni binafsi ya *Pan African Energy Tanzania* imechimba visima vitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kitalu cha Songo Songo kinaendelea na uzalishaji wa gesi asilia ambapo kinazalisha wastani wa futi za ujazo milioni 84.7 kwa siku kulingana na uhitaji. Aidha, kutokana na leseni ya sasa kufikia ukomo mwezi Oktoba 2026, Timu ya Majadiliano ya Serikali *(GNT)* inafanya majadiliano na Mwekezaji Kampuni ya *Pan African* kuhusu uwezekano wa kuongeza kipindi cha pili cha leseni ya uendelezaji wa gesi asilia katika kitalu hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara baada ya majadiliano kukamilika, *TPDC* na *Pan African* wataendelea na mpango wa uchorongaji wa visima zaidi. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hasnain Gulamabbas Dewji, maswali ya nyongeza.

**MHE. HASNAIN G. DEWJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya kuongeza. Ninamuuliza Naibu Waziri, Songo Songo ilikuwa inapata mrabaha wa Serikali, lakini tangu 2019 mrabaha huo haujapatikana. Nimeongea na Halmashauri yangu ya Kilwa, mrabaha haujapatikana, na kijiji husika hakijapata *20%* yake. Ninataka nijue, huu mrabaha utapatikana lini kwa Wilaya yetu ya Kilwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Songo Songo kuna adha kubwa ya maji. Ni kisiwa ambacho kina asili ya mwamba, hivyo kuna adha kubwa ya maji. Ninataka nijue, kwa kuwa uwekezaji mkubwa umefanyika Songo Songo, kwa adha hiyo, Serikali inasemaje kwa ajili ya wananchi wangu wanaopata shida sana ya maji? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. Ujibu swali la kwanza, swali la pili ameuliza upatikanaji wa maji, anaweza akalileta kama swali la msingi likaelekezwa kwenye Wizara husika.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Mbunge, kwa kuwa na ufuatiliaji wa karibu wa namna ambavyo gesi asilia inaweza kuwanufaisha wananchi wa jimbo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Kilwa imekuwa ikinufaika na *CSR*, fedha ambazo zinatokana na uwajibikaji wa mwekezaji katika maeneo husika. Tumekuwa na makubaliano ya kulipa *CSR* na kwa miaka mitatu mfululizo, na tumeshalipa zaidi ya shilingi 900,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kwa sababu ni haki yake kama mwakilishi wa wananchi kuweza kupata taarifa hizi, ninawaelekeza Wizarani waniletee kikokotoo cha malipo ya *CSR* ambazo zimefanyika hizo shilingi 900,000,000 katika eneo la Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na kwenda kwenye kijiji, mara baada ya *TPDC* kupeleka kwenye halmashauri, halmashauri inao wajibu wa kugawa sasa fedha hizo kutokana na jinsi ambavyo watakubaliana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge ameuliza vizuri kuhusiana na kisima, ni kwa sababu *TPDC* kama sehemu ya *CSR* imechimba kisima cha maji. Tunafahamu pale kuna changamoto kubwa sana ya ile pampu kwamba ni ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetenga shilingi 400,000,000 kwa ajili ya kupeleka pampu mpya na tuweze kuzalisha maji zaidi ya lita 100,000. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, sisi kama Serikali, nia yetu ya dhati ni kuwatumikia wananchi na kuwafanya wanufaike na rasilimali zilizopo ndani ya nchi, na tutahakikisha kwa kufanya hivyo, tunawekeza kwenye miradi mbalimbali ya jamii kama sehemu ya kurudisha kwa wananchi kutokana na gesi ambayo tunaipata kwa ajili ya matumizi na kuendeleza uchumi wa nchi yetu. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Najma Giga, maswali ya nyongeza.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mradi wa gesi asilia ni mradi mkubwa katika Taifa letu, na

endapo utakamilika, utakuwa na manufaa makubwa kwa nchi yetu. Nini changamoto ya Serikali kwa mradi huu mpaka leo umeshindwa kukamilika na umekwamisha kazi hii ambayo ni ya muda mrefu?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Najma Giga, tafadhali rudia swali lako.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa gesi ni mradi mkubwa katika Taifa letu na umekuwa wa muda mrefu na ukikamilika utakuwa na manufaa makubwa kwa Taifa letu. Nini changamoto ya Serikali ambayo inakwamisha mradi huu usiweze kukamilika hadi leo?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Najma Giga, amekuwa mshauri mzuri wa Wizara yetu ya Nishati kuhakikisha kwamba tunakamilisha mradi wa gesi asilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, mradi huu umefika katika hatua ya mwisho kabisa. Pia, kama ulisikia wakati Mheshimiwa Waziri akihitimisha hoja yake wakati wa bajeti yetu ya Wizara ya Nishati, ameshakutana na wawekezaji kwenye mradi huu, wanamalizia hatua za mwisho za kisheria ili tuweze kwenda kuanza kuzalisha mradi huu. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, sisi kama Wizara tunatamani sana kuona mradi huu unatokea kwa sababu tunajua ni mradi wa kimkakati ambao utaleta mapinduzi makubwa sana kwenye sekta ya gesi na maendeleo ya mikoa ya kusini.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea. Sasa ninamwita Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba, aulize swali lake.

Na. 316

**Usambazaji wa Gesi Asilia Majumbani Nanyamba**

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA** aliuliza: -

Je, lini usambazaji wa gesi asilia majumbani katika Jimbo la Nanyamba utaanza?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya usambazaji wa gesi asilia nchini hususan katika Mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani na Dar es Salaam ambapo hadi kufikia Aprili, 2026 jumla ya nyumba 2,512 zimeunganishwa na miundombinu ya gesi asilia katika mikoa tajwa. Aidha, jumla ya nyumba 1,000 zimepangwa kuunganishwa kwa mwaka huu wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa miradi hii ni endelevu, na unatarajiwa kufika sehemu mbalimbali nchini ikiwemo katika Jimbo la Nanyamba kwa Mheshimiwa Mbunge, kwa kuzingatia mahitaji, umbali kutoka ilipo miundombinu ya usafirishaji wa gesi asilia na upatikanaji wa fedha za kutekeleza miradi. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, maswali ya nyongeza.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa mahitaji ya matumizi ya gesi ya majumbani ni makubwa kuliko Serikali inavyotenga fedha, je, haioni sasa ni muda mwafaka Serikali kushirikiana na sekta binafsi kwa ajili ya usambazaji wa gesi majumbani? Hilo moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kilometa 25 kutoka Mkuza gesi ilipo ambayo inatoka Madimba kwenda Dar es Salaam kuna kongani ya viwanda vya korosho pale Maranje Halmashauri ya Mji wa Nanyamba, na sasa hivi kuna wawekezaji wakubwa wawili wanajenga viwanda vya ubanguaji wa korosho takribani tani 200,000. Je, Serikali haioni umuhimu sasa kupeleka gesi asilia katika eneo hilo ikiwa kama motisha kwa wawekezaji? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Abdallah Chikota, yeye ni mbobevu katika sekta hii ya nishati ya gesi asilia na tunasambaza gesi majumbani kwa namna tofauti tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Serikali kupitia *TPDC* inatandaza mtandao wa bomba la gesi kwa ajili ya kuhudumia majumbani na Serikali kwa kuona umuhimu na gharama kubwa sasa hivi Serikali imeshafikisha kwenye nyumba zaidi ya 2,000 na nyumba zaidi ya 1,000 zitasambaziwa katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumradhi. Ili kuweza kuongeza kasi, Serikali kupitia ushirikiano na sekta binafsi, tumeshaingia mkataba na kampuni zaidi ya tano ambazo zinasambaza gesi kupitia magari madogo *(mini-LNG)* na hii itaongeza kasi kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameshauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake la pili, ni kweli kabisa Serikali imetoa maelekezo maeneo yote ambayo yana kongani za viwanda ambazo zina vichocheo vikubwa vya kiuchumi, tuhakikishe gharama za uzalishaji wa bidhaa zinazozalishwa kwenye viwanda zinakuwa ndogo na zinaweza kuwa ndogo kama tu kutakuwa kuna gharama ndogo za nishati ya uzalishaji wa bidhaa hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Serikali, tunavyo vipaumbele vya kuhakikisha kwamba kwenye maeneo ambayo tunaweza tukapeleka mtandao wa bomba la gesi, tutapeleka ili gharama za

uzalishaji ziwe chini. Ninakuhakikishia Mheshimiwa Mbunge, mara baada ya kumaliza Bunge hili tutakuja kukagua na kuona uwezekano wa kupeleka bomba la gesi katika kongani hii ya viwanda ili kuweza kuchechemua uchumi wa maeneo ya Nanyamba na mikoa yote ya Kusini mwa Tanzania.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Zacharia Paulo.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Tunaipongeza Serikali kwa hatua kubwa inayochukua ya uunganishaji wa gesi katika taasisi ambazo zina watumiaji wengi na makundi makubwa. Katika Jimbo la Mbulu Mjini tuna shule nne ambazo kila shule ina wanafunzi zaidi ya 1,500. Shule za kidato cha tano na sita; Kainam, Chief, Tlawi, na Gehandu. Shule hizi ni lini Serikali itazifikia ili kuwaunganisha na mitungi ya gesi kwa ajili ya mapishi?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba taasisi zote zinazohudumia wananchi zaidi ya 100, zinaachana na kutumia kuni na mkaa na kwenda kutumia nishati ambayo ni safi. Suala hili limeanza kutekelezwa na Serikali mpaka sasa tumeshafikia zaidi ya taasisi 52. Tumetenga fedha katika mwaka huu wa fedha 2026/2027 kuweza kwenda kwenye taasisi nyingi zaidi. Nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge, pole pole ndiyo mwendo, lakini naamini tutafika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii na jukwaa hili kuwaalika watu wa sekta binafsi, tunazo taasisi nyingi sana kama minada, masoko, bado wanatumia nishati ambayo siyo safi, jambo ambalo linawadhuru wale watumiaji, kuchafua mazingira na linawachelewesha kiuchumi. Milango yetu ipo wazi, wale wanaotaka kuwekeza waje ili tuweze kuhakikisha kwamba taasisi hizi zote ifikapo 2030 zinatumia nishati iliyo safi. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea, na Wizara ya Kilimo. Ninamwita Mheshimiwa Mecktridis Fratern Mdaku, Mbunge wa Malinyi, aulize swali lake.

Na. 317

**Wananchi wa Malinyi Kuongezewa Maeneo ya Kilimo**

**MHE. MECKTRIDIS F. MDAKU** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaongezea maeneo ya kilimo Wananchi wa Malinyi baada ya maeneo yao kuingizwa kwenye Hifadhi?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Serikali kupitia Tangazo Na. 64 la tarehe 24 Februari, 2023 ilitangaza baadhi ya maeneo ya Wilaya za Malinyi, Ulanga na Kilombero kuwa sehemu ya Pori la Akiba la Kilombero kwa ajili ya kuhifadhi vyanzo vya maji vya Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere. Kutokana na hatua hiyo, baadhi ya wananchi waliokuwa wakilima mpunga waliathirika baada ya maeneo yao kuingia kwenye Hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imeweka mkakati wa kupanua na kuboresha skimu za umwagiliaji za Itete hekta 850 na Bonde la Usangule hekta 12,000 ili kutoa maeneo mbadala ya kilimo chenye tija kwa wananchi walioathirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi hii ambapo ujenzi wa skimu ya Itete umefikia 64% na upembuzi yakinifu wa bonde la Usangule umefikia zaidi ya 80%. Skimu hizi zikikamilika zinatarajiwa kunufaisha wakulima zaidi ya 9,000.

Sambamba na hilo, Wizara itaendelea kutoa elimu ya kilimo bora ili kuongeza uzalishaji na tija kwa wakulima.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mecktridis Fratern Mdaku, maswali ya nyongeza.

**MHE. MECKTRIDIS F. MDAKU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini pia ninaipongeza Serikali kwa jitihada zake inazozifanya katika Jimbo la Malinyi kwa kuboresha na kuanzisha kilimo cha umwagiliaji. Hata hivyo, nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali haioni kuwa siyo vizuri kuchukua maeneo ya wananchi na kuyaingiza kwenye Hifadhi za Taifa kabla ya kuwapa maeneo mbadala kwa ajili ya kilimo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nimpongeze Mheshimiwa Mecktridis Fratern Mdaku, Mbunge wa Jimbo la Malinyi kwa swali lake zuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia *concern* yake kuhusu wananchi wake, lakini moja nimhakikishie, Serikali inapokuwa inachukua eneo lolote, ni lazima inakuwa imeshafanya utaratibu wa kuhakikisha tumewashirikisha wananchi, lakini nia kubwa inakuwa ni kuwasaidia wananchi wenyewe. Kwa hiyo, hata ukiangalia kwenye hili bonde, lengo kubwa ni kuhakikisha tunahifadhi kwa ajili ya kupata vyanzo vya maji vya mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere. Hilo ndilo lengo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kikubwa cha kumkuhakikishia Mheshimiwa Mbunge, Serikali chini ya Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan iliunda Kamati ya Mawaziri nane, ambayo moja ya jukumu alilotupatia ni kuhakikisha tunapotengeneza mradi wowote, Wizara zote za kisekta zinazohusika katika eneo husika, yaani kwa mfano kwenye hilo bonde, kuna Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya

Maji, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi na zile Wizara zote za kisekta zinakuwa zinahusika katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimthibitishie tu kwamba sisi kama Wizara za kisekta tutakaa pamoja na kuangalia yale maeneo ambayo tunapaswa kuwasaidia zaidi wananchi ili kuhakikisha tunapata tija ambayo inaleta matokeo kwa wananchi na Serikali kwa ujumla.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Nilikuona Mheshimiwa Ado Shaibu Ado, swali dogo la nyongeza.

**MHE. ADO S. ADO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa changamoto hii ya maeneo ya kulimia inayowakabili wananchi wa Malinyi inafanana kabisa na changamoto ambayo inawakabili wananchi wa Vijiji vya Twendembele na Naluwale Wilayani Tunduru ambapo maeneo yao pia yalitwaliwa kutokana na masuala ya uhifadhi; na kwa kuwa viongozi mbalimbali waandamizi wamekuwa wakiwapa ahadi, *especially* kwa wenzetu wa Twendembele, kwamba maeneo yataongezwa, nini kauli ya Serikali sasa katika kutekeleza ahadi hizi za viongozi ili wananchi wa vijiji hivyo vya Twendembele na Naluwale wapate maeneo ya kulima, kwa sababu *pressure* ya kuongezeka kwa watu imekuwa kubwa na maeneo ya kulima ni madogo?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze vilevile ndugu yangu Mheshimiwa Ado Shaibu kwa swali lake la msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo moja tu nimwambie Mheshimiwa Ado, kauli ya Serikali ni kwamba, Serikali inachokiahidi lazima itakitekeleza, na maana yake huwa tunafanya tathmini na kuna vikao ambavyo kila hatua huwa tunavifanya. Tukishamaliza hatua zote za vikao ambavyo tumevifanya, maana yake tutakuja kuwaonyesha wananchi ni eneo gani wanapaswa sasa walilime hususan katika eneo hilo la Twendembele, Tunduru ambako ameliainisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuwathibitishie tu kwamba ahadi ya Serikali iko palepale na itatekelezwa mara baada ya kumaliza hatua zote za kiutaratibu.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Sasa ninamwita Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrew, Mbunge wa Viti Maalum, aweze kuuliza swali lake.

Na. 318

**Kuangalia Upya Gharama za Uzalishaji wa Tumbaku**

**MHE. JACQUELINE K. ANDREW** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaangalia upya gharama za uzalishaji wa Tumbaku ili Mkulima apate faida?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kuwa gharama za uzalishaji wa zao la tumbaku zimekuwa changamoto kwa wakulima, hususan kutokana na kupanda kwa bei za pembejeo, gharama za nishati hasa kuni na makaa kwa ajili ya kukaushia tumbaku pamoja na riba za mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Bodi ya Tumbaku na wadau imeanza kupitia mjengeko wa gharama za uzalishaji ili kuainisha maeneo ambayo yanaweza kupunguza gharama za uzalishaji ikiwemo pembejeo, tozo za vyama vya ushirika na mikopo ya benki. Aidha, Serikali imeanza vikao na benki zinazotoa mikopo kwenye zao la tumbaku kwa lengo la kujadili uwezekano wa kupunguza riba ya mikopo na gharama zinazohusu mikopo hiyo. Lengo ni kuhakikisha kuwa wakulima wa zao la tumbaku wanapata faida kupitia kilimo cha zao hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrew, swali la nyongeza.

**MHE. JACQUELINE K. ANDREW:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kupata nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Ninaipongeza Serikali kwa majibu mazuri, lakini kwa kuwa sasa masoko tayari yameshaanza, na bei iliyoko sokoni inaendelea kuwa chini, tofauti na hata bei elekezi iliyowekwa na Serikali ambayo ni dola 1.95, na sasa mkulima anapata dola 1.4, je, Serikali haioni kama mwananchi huyu anazidi kupata hasara zaidi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili. Kwa kuwa bei ya uzalishaji haiko sawa na bei halisi ya uzalishaji ya sasa. Je, Serikali haioni kuna haja ya kuweka ruzuku ya haraka kama ilivyowekwa kwenye mafuta ili kumnusuru mwananchi huyu?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza dada yangu Mheshimiwa Jacqueline Kainja kwa maswali madogo mawili ya msingi kabisa yenye tija na faida kwa wakulima wa zao la tumbaku. Ni kweli anachokieleza ni kwamba kumekuwa na changamoto ya bei kama ambavyo nimeainisha katika jibu la msingi. Ni kweli kwamba bei ya tumbaku imekuwa ikibadilika kila nyakati, na sisi kama Serikali tumekuwa ni watu ambao tunaliangalia hilo ili kuhakikisha kwamba tunaongeza tija kwa mkulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunatambua kuna nyakati mkulima anaweza akapata bei pungufu ambayo inaweza kumpelekea hasara kidogo kulingana na mabadiliko ya kibei, lakini wajibu wetu sisi kama Serikali, ni kuhakikisha tunatengeneza mazingira bora na sahihi ambayo yatamsaidia mkulima kupata tija ikiwemo kupunguza bei kwenye pembejeo za zao la tumbaku ili kuhakikisha walau ana-*cover* ile gharama ambayo amekuwa ameingia. Kwa hiyo, kwa mfano, hili suala la bei; dola 1.9 na dola 1.4 maana yake sisi kama

Serikali tutakaa na tutafanya tathmini upya ili kuangalia ni namna gani tunaweza kumsaidia yule mkulima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuweka ruzuku, ni jambo ambalo Serikali imekuwa ikifanya. Tumefanya kwenye mazao mengi na kwenye tumbaku kuna wakati tulishajaribu. Bado tunaendelea kufanya tathmini na tukishamaliza hiyo tathmini tutakuja kuainisha kwa wadau wa zao la tumbaku ili kuona namna gani tunaweza kusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kwa kifupi ni kwamba, tumeanzisha Mfuko wa *Agriculture Development Fund*, mfuko wa pembejeo kwa ajili ya kilimo. Lengo la mfuko ule ni kusaidia changamoto hizi ambazo zinakuwa zinajitokeza hasa katika nyakati ambazo mkulima anakuwa hajatarajia kupata anguko la kibei.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, na sasa ninamwita Mheshimiwa Edibily Kazala Kinyoma, Mbunge wa Kasulu Vijijini, aulize swali lake.

*(Hapa mic ilizima)*

**MWENYEKITI:** Jaribu kuwasha *mic*.

Na. 319

**Utatuzi wa Mgogoro wa Ardhi – Kasulu Vijijini**

**MHE. EDIBILY K. KINYOMA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kumaliza mgogoro wa ardhi kati ya *TFS* na *TAWA* dhidi ya wananchi wa Jimbo la Kasulu Vijijini?

**MWENYEKITI:** Majibu ya Serikali Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Edibily Kazala Kinyoma, Mbunge wa Kasulu Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Kasulu Vijijini kuna Kitalu cha Uwindaji cha Makere - Uvinza ambacho kimetengwa na kusimamiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu. Baada ya kutengwa kwa kitalu hicho ulijitokeza migogoro kwa baadhi ya wananchi kuanzisha shughuli za kibinadamu kama vile makazi na kilimo ndani ya eneo la kitalu ikiwemo Kitongoji cha Katoto kilichoanzishwa ndani ya kitalu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Kamati ya Mawaziri nane wa kisekta ilitoa maelekezo kuwa kitongoji hicho kihamishwe baada ya kubaini kuwa kimeanzishwa nje ya mipaka ya Kijiji mama cha Kagerankanda. Serikali ya Mkoa wa Kigoma ilitekeleza maelekezo hayo na kusimamia zoezi la kuwahamisha wananchi hao kwenda kwenye Kijiji cha Kagerankanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Oktoba, 2025 uongozi wa Mkoa wa Kigoma kwa kushirikiana na uongozi wa Wilaya ya Kasulu ulifanikiwa kuhamisha wananchi wote kutoka Kitongoji cha Katoto na kwenda Kitongoji cha Nyantuku katika Kijiji cha Kagerankanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha huo, endapo kuna changamoto nyingine zinazotokana na mwingiliano wa matumizi ya ardhi kati ya wananchi na kitalu hicho, Wizara ipo tayari kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge na Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu kutafuta ufumbuzi na kuondoa changamoto hizo. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Edibily Kazala Kinyoma, maswali ya nyongeza.

**MHE. EDIBILY K. KINYOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ninashukuru. Ninaomba tu kusema kwamba majibu yanakinzana na

swali langu la msingi. Kwa hiyo, ninaomba Serikali initafutie majibu mengine mbadala tofauti na hayo. Ahsante na sina swali la nyongeza.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Tunakushukuru Mheshimiwa Naibu Waziri. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ujenzi. Sasa ninamwita Mheshimiwa Thomas Kampala Maganga, Mbunge wa Katavi, aweze kuuliza swali lake.

Na. 320

**Barabara ya Inyonga – Majimoto hadi Kibaoni Km 162**

**MHE. THOMAS K. MAGANGA** aliuliza: -

Je, lini ujenzi wa kiwango cha lami utaanza kwa barabara ya Inyonga – Majimoto hadi Kibaoni (km 162) kwa kuwa upembuzi yakinifu ulishakamilika?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Thomas Kampala Maganga, Mbunge wa Katavi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanza ujenzi wa barabara ya Kibaoni – Majimoto – Inyonga yenye urefu wa kilometa 152 kwa awamu ambapo mpaka sasa vipande vyenye urefu wa kilometa 9.3 vimekamilika katika *center* za vijiji vya Usevya kilomita 2.5, Majimoto kilomita 2.6 na Inyonga kilomita 4.2. Kwa sasa, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa barabara yote kwa kiwango cha lami.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Thomas Kampala Maganga, maswali ya nyongeza.

**MHE. THOMAS K. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Kwa kuwa barabara hii ni muhimu sana kwa wananchi wa Jimbo la Katavi, Kavuu na Mikoa ya Sumbawanga, Kanda ya Magharibi kwa jumla, je, Serikali haioni sasa kuna umuhimu wa kuweka fedha za kutosha ili hii barabara ikamilike kwa wakati na kuwaondolea usumbufu wananchi wa mikoa hiyo?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua sana umuhimu wa barabara hii, na ndiyo maana tayari tumeshakamilisha usanifu na tumeshaanza kujenga barabara kwenye ile miji mikubwa kwa kiwango cha lami. Pia ninamkumbusha Mheshimiwa Mbunge kwamba ndiyo maana tuna madaraja mawili ambayo tunajenga likwepo lile la Kavuu ili kuweza kuhakikisha kwamba tunapitisha malori makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu amefanya ziara, alitoa maelekezo kwa Wizara kuhakikisha kwamba katika bajeti hii tunayoiendea, tuweze kuijenga hiyo barabara kwa kiwango cha lami, maelekezo ambayo Wizara inayafanyia kazi.

**MWENYEKITI:** Ahsante, nilikuona Mheshimiwa Kijakazi Mohamed, swali dogo la nyongeza.

**MHE. KIJAKAZI Y. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuweza kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Barabara ya Mingoyo – Masasi kwa muda mrefu sana imekuwa mbovu na Serikali imeliona hilo, tayari mkataba umesainiwa, mkandarasi amepatikana na amepewa *site* kwa muda mrefu, lakini mpaka sasa kazi haijaanza. Ninaomba *commitment* ya Serikali, ni lini mkandarasi yule ataanza kazi na kukamilika kwake?

**MWENYEKITI:** Jibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli barabara hii ya Mingoyo – Masasi imechakaa, lakini ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tunavyoongea sasa hivi, ile barabara tunaifanyia ukarabati mkubwa ambao ni sawa na kuijenga upya kuanzia Mtwara – Mingoyo na Mingoyo – Masasi. Tumegawa katika *lot* mbili, kutoka Mtwara – Mingoyo na kutoka Mingoyo – Masasi kilometa 200 ambapo mkandarasi tulishampata, yupo kwenye maandalizi ya kuanza hiyo kazi tukisaidiana na wenzetu wa *World Bank*.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Bonnah Kamoli, swali la nyongeza.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuuliza, Serikali ina mpango gani na Mkoa wa Dar es Salaam kwa kuwa kuna barabara sasa hivi mbovu sana? Je, kuna mpango wa dharura ili barabara ziweze kutengenezwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Jibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiachia mbali mipango ya Serikali ya kawaida, lakini pia tumeainisha barabara nyingi ambazo zimepata athari katika kipindi hiki ambacho mpaka sasa hivi mvua zinaendelea kunyesha, kuzikarabati kwa dharura tukiwa tunasubiri mpango wa kawaida wa kuzifanyia matengenezo makubwa barabara za Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna mpango mkubwa wa barabara nyingi ambazo tumeziweka katika mpango wa kuzijenga ili pia kupunguza foleni ikiwa ni pamoja na kujenga barabara nyingi kwa kiwango ambacho kinapitika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zile ambazo tunahakikisha siyo lazima mtu apite kwenye barabara zile kubwa, basi hizi barabara ambazo zinakwenda zinaunganisha wananchi na wananchi ziweze kujengwa ili zitumike pia kama sehemu ya kupunguza msongamano mkubwa katika Mji wa Dar es Salaam.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Wahehsimiwa Wabunge. Waheshimiwa tunaendelea, na sasa ni Wizara ya Afya. Ninamwita Mheshimiwa Mohamed Mussa Utaly, Mbunge wa Lindi Mjini, aulize swali lake.

Na. 321

**Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Lindi**

**MHE. MOHAMED M. UTALY** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Lindi?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, ninaomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Mohamed Mussa Utaly, Mbunge wa Lindi Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Lindi unatekelezwa kwa awamu. Awamu ya kwanza na ya pili zimekamilika kwa gharama ya shilingi 4,000,000,000 ambapo sakafu ya kwanza imekamilika na inatoa huduma. Aidha, Wizara imeingia Mkataba kwa ajili ya ukamilishaji wa awamu ya tatu ambapo Mkandarasi ameanza kazi mwezi Novemba, 2025 kwa Mkataba wa miezi 12 na unatarajiwa kukamilika kabla au ifikapo mwezi Desemba, 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa Mkandarasi ameshalipwa kiasi alichoomba jumla ya shilingi 812,000,000 kama hati ya malipo ya awali *(Advance Payment)*. Aidha, Serikali itaendelea kusimamia ujenzi huo ili kuhakikisha unakamilika kama ilivyopangwa. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mohamed Mussa Utaly, maswali ya nyongeza.

**MHE. MOHAMED M. UTALY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwanza ninaipongeza Serikali kwa namna ambavyo inashughulikia suala hili la Hospitali ya Rufaa ya Lindi. Hata hivyo, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa hospitali hiyo inatarajiwa kukamilika mwezi Disemba mwaka 2026, tuliokuwa nao, je, Serikali imejipangaje kuhakikisha kuwa mambo muhimu kama vifaatiba, mashine za kisasa, wataalamu bobezi wa afya wanapatikana mara tu ujenzi utakapokamilika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa Mkoa wa Lindi ni miongoni mwa mikoa inayokua kwa kasi kutokana na Uchumi wa Bluu na mradi wa Mkakati wa Gesi, je, Serikali imezingatia ukubwa wa hospitali hiyo kuendana na ongezeko la watu na mahitaji ya huduma za afya za baadaye? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Jibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Mbunge Mohamed Utaly kwa kazi nzuri anayofanya kuwapigania wananchi wa Lindi. Kama nilivyosema, kwenye swali langu la msingi, Hospitali ya Lindi ni hospitali mpya ambayo imeanza kufanya kazi mwezi wa 12 kwa kuhama kwenye majengo ya zamani kwenda kwenye majengo mapya. Sisi kama Serikali tumejipanga kuhakikisha kwamba hospitali hii itakapoisha inakuwa na vifaa kamili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa hospitali hii inavyo vifaa muhimu vya kufanya uchunguzi wa radiolojia kwa maana ya *ultra sound machine, X-Ray machine*, na *CT-Scan* na vyote hivyo vinafanya kazi. Hospitali hii inayo maabara ya kisasa yenye uwezo wa kupima vipimo vyote vikubwa kwa maana ya kibingwa. Inayo *bio-chemistry machine*, *Cell Dyn* pamoja na *Haematology Analyzer.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali hii ya Lindi inatoa huduma za kibingwa katika fani tatu, lakini inayo wataalamu watano. Serikali imejipanga kupeleka watumishi sita kwenda kusoma ili tuweze kupata wataalamu wa kibingwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tumejipanga Hospitali ya Lindi kutoa fani za kutosha. Lengo letu ni kwamba ifikiapo 2030, Hospitali hii ya Lindi iweze kutoa fani za kibingwa 17 kama ambavyo Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, alielekeza alipohutubia Bunge mwezi wa 11 mwaka 2025 kwamba tunatakiwa kufika katika huduma hizo za kibingwa 17. Kwa hatua za haraka, tutafanya msawazo wa wataalamu wa kibingwa ili waweze kufika Lindi kuendelea kutoa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili linataka kujua tumejipanga vipi? Lindi inakua, Lindi ni mkoa wa kimkakati, na Serikali imejipanga kuendana na ukubwa wa mkoa huo. Ndiyo maana tumeihamisha kutoka hospitaki kongwe ambayo ilikuwa na eneo dogo na majengo chakavu, na tumeipeleka kwenye eneo jipya ambalo lina ekari 100. Hivyo, ninakuthibitishia Hospitali ile ya Lindi tunaweza kuipanua kwa kadiri tunavyotaka kwa sababu tayari eneo linatosha kuweza kutoa huduma hizo tarajiwa. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Rashid Shangazi, swali dogo la nyongeza.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tanga Bombo, ni miongoni mwa hospitali za kwanza kabisa hapa nchini ikiwa imejengwa mwaka 1901, na sasa ina takribani miaka 125. Hospitali hii ni chakavu sana, wodi zake za Galanosi pamoja na Mwapachu na Sokoine zina hali mbaya sana. Hii Galanosi ni wodi ya mama na mtoto na iko katika hali mbaya sana ambayo zinahitaji kujengwa upya. Ni upi mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba wodi zake zinajengwa kwa haraka ili kuweza kuipa hadhi ya kuwa ya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa Shangazi kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuwapigania wananchi wake wa Mkoa wa Tanga. Ni kweli kabisa Hospitali ya Bombo ni moja ya hospitali chakavu, lakini ninakuthibitishia, pamoja na uchakavu wake, inafanya kazi vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Bombo ni moja ya hospitali ambazo zinatoa huduma za kibingwa 10. Kwa hivyo inafanya vizuri sana. Sisi kama Serikali tumejipanga kuendelea kuboresha miundombinu ya Hospitali ya Bombo kwa kujenga wodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bajeti hii, tumetenga shilingi 1,000,000,000 ambayo itaenda kuanza ujenzi wa wodi za wagonjwa katika Hospitali ya Bombo. Siyo hivyo tu, tumetenga pia shilingi bilioni 1.6 ili kuweza kumalizia ujenzi wa Jengo la Damu Salama. Hivyo ninakuhakikishia, Serikali imejipanga kuendelea kukarabati hospitali kongwe zote ili ziweze kutoa huduma kulingana na wakati wa sasa.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Alan Thomas Mvano, swali dogo la nyongeza.

**MHE. ALAN T. MVANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada nzuri za Serikali yetu, kutoka Kigoma kwenda Bugando ama kuja Dodoma kufuata huduma za rufaa, imekuwa ni mbali sana. Dodoma zaidi ya kilometa 700, Mwanza Bugando zaidi ya Kilometa 600. Kwa kuwa Setikali imekuwa na mpango wa kujenga Hospitali ya Rufaa katika Mkoa wa Kigoma, ni lini sasa ujenzi wa Hospitali ya Rufaa katika Mkoa wa Kigoma utaanza?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Ninampongeza Mheshimiwa Alan Mvano, Mbunge wa Kakonko kwa kazi nzuri anayofanya. Mkoa wa Kigoma unayo Hospitali ya Rufaa ya Mkoa kwa maana ya Maweni Hospitali ambayo

inafanya vizuri na inatoa zaidi ya huduma 10 za kibingwa. Hata hivyo, Serikali kwa kuelewa mkakati wa Mkoa wa Kigoma, imetenga fedha shilingi 8,000,000,000 kwa ajili ya kujenga Hospitali ya Kanda katika Mkoa wa Kigoma ili kuendelea kudumisha huduma bora katika kanda hiyo ya Mkoa wa Kigoma. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa maswali na majibu na sasa …

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika…

**MWENYEKITI:** Ninaomba niwatangazie wageni waliopo Bungeni asubuhi ya leo.

Tunaanza na wageni waliopo Jukwaa la Spika ambao ni wageni sita kutoka Bunge la Msumbiji ambao ni Kamati ya Ulinzi na Usalama. Yupo Mheshimiwa Fransisco Velentino Cabo, Mwenyekiti wa Kamati na Kiongozi wa Msafara; Mheshimiwa Isaura Antonio Julio, Mjumbe wa Kamati; Mheshimiwa Jafete Caetano Eurico, Mjumbe wa Kamati; Mheshimiwa Virginia Kwavateka Gondola, Mjumbe wa Kamati; Mheshimiwa Jose Tomas Chidudo, Mjumbe wa Kamati; na Ndugu Pendegrencio Paulo Cossa, Katibu wa Kamati. Karibuni sana Wabunge wa Bunge la Msumbiji ndani ya Bunge letu. *(Makofi)*

Wapo pia wageni wa Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, Waziri wa Afya. Yupo Ndugu Lulu Mohamed, Mdau wa Sekta ya Afya. *(Makofi)*

Wapo pia wageni wanne wa Mheshimiwa Mchengerwa ambao ni Wawekezaji kutoka Hospitali ya Mloganzila Jijini Dar es Salaam. Yupo Ndugu Miayo Yingyang, Mwekezaji wa Vifaa Tiba na Dawa; Ndugu Lyu Yinghua, Mtafsiri wa Lugha; Ndugu Su Zhou, Mkurugenzi wa Ndani; na Ndugu Victor Tesha, Mtaalamu Mshauri wa Mradi. *(Makofi)*

Wapo pia wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Yupo Mgeni wa Mheshimiwa Steven Lemomo Kiruswa, Naibu Waziri wa Madini ambaye ni Dkt. Godluck Ole-Medeye, Mratibu wa Jukwaa la Mawaziri Wastaafu. *(Makofi)*

Pia yupo mgeni wa Mheshimiwa Revocatus Clayton Chipando, ambaye ni Mstahiki Meya wa Kigoma Ujiji, Mheshimiwa Mussa Maulid. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, ni Ndugu Dkt. Karanta Simwanza, ambaye ni Mshauri wake wa Afya. *(Makofi)*

Wapo wageni wanne wa Mheshimiwa Dkt. Regina Christopher Malima ambayo ni familia yake kutoka Shinyanga na Kilimanjaro wakiongozwa na binti yake (Mtoto wake) Dkt. Benzeni Makaranga. *(Makofi)*

Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati ambao ni Madaktari Bingwa wa Magonjwa ya Wazee kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wapo wageni tisa wa Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli, hawa ni marafiki zake kutoka Ilala Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wapo wageni 11 wa Mheshimiwa Anna Richard Lupembe ambao ni Wanamaombi kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wapo pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya Mafunzo. Yupo Ndugu Sabato Nahol Paulo kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Kelvin Msuya kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wapo pia Wanafunzi 25 Wanachama wa Klabu ya Afya ya Chuo Kikuu cha Dodoma. *(Makofi)*

Wapo Wanafunzi 70 wa Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine *(SUA)* kutoka Mkoani Morogoro. *(Makofi)*

Wapo pia Wanafunzi 12 wa Shahada ya Mipango na Usimamizi wa Mazingira wa Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wapo pia Wanafunzi 70 wa Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi kutoka Chuo Kikuu cha Kiislamu Morogoro. *(Makofi)*

Wageni wetu wote karibuni ndani ya Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*.

Waheshimiwa Wabunge, ninayo matangazo yanatoka kwa Katibu wa Bunge. Waheshimiwa Wabunge wote mnakumbushwa kuwa Wizara ya Afya imeandaa Programu Maalumu ya Kutoa Huduma za Afya katika viunga vya Bunge kwa Wabunge na Watumishi. Huduma hiyo ilianza kutolewa tangu tarehe 10 na itaendelea hadi leo Jumanne tarehe 12 Mei, 2026.

Waheshimiwa Wabunge, huduma hizo zinatolewa na Watalamu wa Afya kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Taasisi ya Tiba ya Mifupa na Ubongo Muhimbili, Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, Taasisi ya Saratani *Ocean Road,* Hospitali ya Rufaa ya Kanda Benjamini Mkapa, Hospitali ya Rufaa ya Kanda *(KCMC)*, Hospitali Maalumu ya Taifa ya Afya ya Akili (Mirembe), Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu, na Hospitali ya Rufaa ya Kanda Bugando.

Waheshimiwa Wabunge, aidha, huduma zinazotolewa ni uchunguzi na ushauri wa kitaalamu kuhusu magonjwa ya moyo, mifupa, mgongo, afya ya wanawake na uzazi, macho, ngozi, magonjwa ya ndani, figo, afya ya akili, saratani, afya ya kinywa na meno, pamoja na tiba asilia. Hivyo, Waheshimiwa Wabunge, mnaombwa kutembelea mabanda hayo ili kupata huduma na ushauri wa kitaalamu.

Waheshimiwa Wabunge, lipo tangazo lingine kutoka kwa Katibu wa Bunge. Waheshimiwa Wabunge wote mnatangaziwa kuwa siku ya Jumanne tarehe 12 Mei, 2026 kutakuwa na Semina kuhusu namna ya

kukabiliana na wanyama wakali na waharibifu pamoja na namna ya mfumo wa ulipaji wa kifuta jasho na kifuta machozi unavyofanya kazi, itakayotolewa na Wizara ya Maliasili na Utalii. Semina hii itafanyika saa Saba mchana katika Ukumbi wa Msekwa mara baada ya kusitisha Shughuli za Bunge.

Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kuhudhuria Semina hii muhimu ili iwasaidie kutoka elimu kwa wananchi na kuwa Mabalozi kwa umma kuhusu uhifadhi endelevu na utangazaji wa utalii nchini…

**MHE. EDIBILY K. KINYOMA:** Mwongozo wa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Mwongozo, Mheshimiwa Edibily Kinyoma.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. EDIBILY K. KINYOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kwa mujibu wa Kifungu 79 ya Kanuni za Bunge. Wakati Mheshimiwa Waziri anajibu swali langu Na. 319 jibu lake lilikuwa linakinzana na swali langu la msingi. Kwa hiyo, nikawa ninaomba Mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Edibily Kinyoma ameomba Mwongozo kwa mujibu wa Kanuni ya 79 kuhusiana na swali lake Na. 319 ambalo lilipatiwa majibu na Serikali, na baada ya kupitia hapa, ni ukweli kwamba swali lake la msingi halijapata majibu stahiki. Hivyo, ninaelekeza swali hili lijibiwe upya na Serikali.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano ya Wizara ya Afya na sasa tunaendelea na uchangiaji. Ninamwita Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, ajiandae Mheshimiwa Mwita Waitara, na Mheshimiwa Dkt. Lembulung' Lukumay.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza siku ya leo niweze kuchangia hii Hotuba ya Wizara ya Afya ambayo ni Wizara muhimu sana kwa Taifa, na kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya na uzima, nimeweza kusimama hapa siku ya leo kuchangia hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nimpongeze sana Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kweli anafanya kazi kubwa na nzuri kuhakikisha kwamba wananchi wa Tanzania wanapata huduma bora na siyo bora huduma. Kwa kweli tunampongeza mama na mimi binafsi naendelea kumwombea, Mwenyezi Mungu ambariki, amjalie afya njema aweze kuendelea kutupambania sisi Watanzania, na sisi tuko nyuma yake tunamsaidia katika majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Afya, kaka yangu, ndugu yangu Mohamed Mchengerwa pamoja na Naibu wake dada yangu Dkt. Samizi kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanaifanya kwenye Wizara bila kumsahau Katibu Mkuu kwenye Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa simtendei haki Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Kitete Tabora, huyu ndiye ambaye nimekuwa nikifanya naye kazi kwa karibu sana kipindi chote, na hata ninapokuwa sipo, Ofisi yangu imekuwa ikifanya naye kazi kwa karibu

mno kuhusiana na changamoto za wananchi katika Jimbo la Tabora Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumbuka Hospitali ya Kitete ni Hospitali ya Mkoa, lakini iko kwenye Jimbo la Tabora Mjini. Kwa hiyo, ninafanya nayo kazi kwa karibu kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo mimi ninaomba niseme maneno machache kuhusiana na hii Wizara ya Afya. Pamoja na pongezi nilizowapa, nilikuwa ninaomba sana pamoja na yote, mnafahamu kila siku kilio chetu kikubwa hospitali yetu imekuwa ni hospitali ya muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya kitete imeanzishwa mwaka 1906, wakati huo wale wenzetu walikuwa wakipata majeraha, au nini, wanapelekwa pale. Majengo ya hospitali ile kwa kweli siyo rafiki sana. Ningeomba sana, Serikali imesema itafanya *structure* mpya kwa ajili ya ujenzi wa hospitali mpya pale katika Hospitali ya Kitete. Kila nikiangalia naona kama bado tunahitaji hospitali na tunahitaji eneo kubwa ili kuweza kujenga hospitali yenye hadhi ya Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mtakumbuka, Tabora tuna watu zaidi ya milioni tatu ambao wengi wanategemea hospitali ile, lakini kumekuwa na changamoto kubwa sana ya upatikanaji wa huduma mbalimbali katika hospitali ile. Watu wakifika pale wengine wanaambiwa nendeni Bugando, wengine wanaambiwa nendeni Benjamini Mkapa. Kwa kweli hii hali siyo sawasawa kabisa

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachohitaji sisi kama watu wa Tabora ni kuhakikisha huduma zote zinapatikana katika Hospitali yetu ya Rufaa ya Mkoa wa Tabora, kwa sababu kuna watu wengi, na wengi wanahitaji huduma, na wananchi wanatufuata sana kutuuliza ni kwa namna gani ambavyo mtaweza kuboresha huduma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri kuhakikisha kwamba fedha zinapelekwa kwa ajili ya kumalizia

jengo la Mama na Mtoto. Mheshimiwa Naibu Waziri atakumbuka hiki ni kilio changu cha muda mrefu. Ninajua watakavyokuja kutujibu hapa kutakuwa kuna majibu mazuri na sisi watu wa Tabora tupate kupumua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kutuletea fedha kwa ajili ya kuanza kwa ujenzi wa jengo la *ICU* kwa ajili ya watoto. Ninamwomba sana Mheshimiwa Naibu Waziri, jengo hili ujenzi wake umeshaanza, lakini fedha zipelekwe kwa wakati ili jengo hili liweze kukamilika kwa wakati kama ambavyo wametuahidi sisi watu wa Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Yambe kwa kazi kubwa anayoifanya, amekuwa akitumia mapato ya ndani kuhakikisha kwamba anaboresha changamoto zinazopatikana pale kwenye hospitali yetu. Ameweza kuboresha baadhi ya majengo ya wodi, lakini pia ameweza kununua vifaa tiba vya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi pale katika Hospitali ya Kitete ameweza kutuwekea *gym* kuhakikisha kwamba yale magonjwa yasiyoambukiza yanapungua kwa watu kuweza kufanya mazoea ya kufanya mazoezi ili kuweza kuondoa ama kupunguza magonjwa yasiyoambukiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nizungumzie kuhusiana na suala zima la Bima ya Afya. Kwanza kabisa, ninampongeza sana Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uamuzi wake thabiti wa kuhakikisha kwamba Watanzania wote tunakuwa na Bima za Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakubaliana na mimi kwamba kila mara sisi Wabunge tumekuwa tukipata changamoto za wananchi wetu kupata maradhi na mwisho wa siku kuwa hawana uwezo wa kwenda kupata huduma. Tumekuwa tukiwasaidia kwa matibabu mara kwa mara, lakini Mheshimiwa Rais ametuletea hii Bima ya Afya na sisi Wabunge tumuunge mkono kwa kuhakikisha tunashauri vizuri katika suala zima la Bima ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu ni kwa namna gani Serikali inapambana kuhakikisha wana-*finance* hii Bima ya Afya. Hata hivyo, kunakuwa kuna changamoto. Niwaambie Wizara, wananchi wa Tanzania wako tayari kuchangia hii Bima ya Afya lakini ambacho wanakutana nacho ni cha upungufu wa vifaa tiba, na upungufu wa dawa kidogo, kinawachanganya. Wanaona akienda pale na bima yake hata *panadol* anambiwa nenda kanunue nje. Hili jambo siyo sahihi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana na ninaishauri Serikali kuhakikisha kwamba, kwa mfano kwa sasa hivi kuna vijana ambao wana mtandao wao, na jana nilikuwa nikimsikia kaka yangu hapa Mheshimiwa Kingu amezungumzia jambo hili, na mimi ninaomba niungane naye kwa dhati ya moyo wangu kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa vijana ambao wana *platform* yao kupitia *mobile network*; Wizara ingeamua kujiunga katika hii *mobile network* na wao wakawa na akaunti yao maalumu kuhakikisha kwamba Watanzania (wananchi) wanachangia kidogo kidogo ili kuweza kupata huduma bora za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu Serikali ina mambo mengi, ina changamoto nyingi. Kwa hiyo, ni imani yangu kwamba ikifanya hivi, itakusanya fedha nyingi ili kusaidia huduma bora za afya na siyo bora huduma na wananchi wengi huko kabisa watajiunga katika hii Bima ya Afya katika kumuunga mkono Mheshimiwa Rais wetu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda umekwisha?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ndiyo muda wako umekwisha.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika tano?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umeisha, unga mkono hoja.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunachangia kwa dakika sita, wachangiaji ni wengi sana. Sasa ninamwita Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara ajiandae Mheshimiwa Johannes Lukumay.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa nafasi. Nilikuwa nimejiandaa kuchangia kwa dakika 10, lakini nitazingatia maelekezo ya Kiti. Mambo tunayochangia hapa ni mambo ambayo ama tumekutana nayo au tunapata kutoka kwa wananchi wetu katika maisha ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, la kwanza ningependa niseme tu kwamba Mheshimiwa Waziri wa Afya amekuwa anafanya kazi nzuri, na Jimbo la Tarime Vijijini ameacha alama tangu amefanya ziara akiwa Waziri wa Maliasili. Kwa Wabunge wengi hawana wasiwasi na uwezo wake mahali popote ambapo amepelekwa amekuwa *bulldozer,* anafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nisaidiwe, sisi Wabunge hapa tuna bima, maana unaanza kujitetea wewe mwenyewe halafu unaenda maeneo mengine. Wabunge hapa tunapata huduma ya bima kwa maana ya Mbunge, mke au mume na watoto, lakini wazazi wetu hawamo kwenye ile bima. Nimekaa hapa kipindi chote sijapata maelezo ya maana kwa nini Wabunge wazazi wetu hawatibiwi na bima hii ambayo tunapata hapa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo Wabunge hapa vijana wengine hawajaolewa, wengine hawajaoa, wengine ni wagane na wengine ni wajane. Kuna watu ambao wana wazazi wao ambao watoto wao hao vijana waliopo humu Bungeni nikiwepo na mimi, wazazi wetu walilima kahawa, wakawinda wanyama tukasomeshwa, lakini mzazi

anagua, Mbunge anahangaika na mzazi wake. Hili jambo limeleta taharuki katika familia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba Mheshimiwa Waziri aniambie ni sababu gani imezuia Wabunge wazazi wetu wasitibiwe kwa bima zetu? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, wagonjwa wakienda hospitalini wanaenda kumwona daktari, kuna kitu kinaitwa *consultation fee*, yaani ili Mganga amsikilize, analipia. Sasa mgonjwa huyu akishamaliza kupata maelezo ya daktari, anaenda pale dirishani anatakiwa achangie gharama ya matibabu, fedha ile ameshamaliza. Hawa watumishi madaktari wanalipwa na kodi za Watanzania hawa hawa; ni sawa na walimu, sawa na watumishi wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini mgonjwa alipe fedha ndiyo aelezwe ugonjwa wake? Kwa nini isigeuzwe, mgonjwa akishaelezwa ugonjwa wake aende dukani, fedha aliyonayo achangie matibabu? Kwa hiyo, ningeomba jambo hili Mheshimiwa Waziri pia uliangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, Jimbo la Tarime Vijijini watumishi waliopo ni 36.9% tu, zaidi ya 60% hakuna watumishi katika maeneo yale. Tuna vituo vya afya kama Mtana miaka mitatu sasa; Bumela, Sirari, Magoma, Gibaso, Kerende hivi vituo vyote vya afya vimekamilika, ni majengo yako pale buibui ndiyo wanaishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Waziri anisaidie namna ya kufanya kazi. Kituo cha afya kisifanye kazi ya zanati na wananchi wa Tarime Vijijini wasiendelee kuangalia majengo badala ya kupata huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne ni Hospitali ya Rufaa ya Musoma, kwa Baba wa Taifa. Tunapozungumza, kuna mkataba waliingia mwaka 2024 wa shilingi 14,000,000,000, Mkandarasi amelipwa shilingi 4,000,000,000 tu. Majengo ambayo yanatakiwa kujengwa pale ni muhimu sana. Yaani kule hakuna huduma ya macho, hakuna huduma ya meno, hakuna huduma ya mionzi, hakuna wodi za wagonjwa na mkandarasi anafanya kazi hajalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Mheshimiwa Waziri atoe hadhi na heshima kubwa kwa Mkoa wa Mara. Wagonjwa wa Mkoa wa Mara wanatumia gharama kubwa kwenda Bugando siku hizi, kuja Benjamin Mkapa na kwenda Muhimbili kwa sababu ya huduma hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yule Mandarasi *Prince Limited* apewe fedha yake ile hospitali ikamilike. Mnavyozungumza utalii wa kimatibabu ni pamoja na Mkoa wa Mara; ukitibiwa, umepona, kabla ya kurudi ulikotoka unaenda Butiama kwa Baba wa Taifa unaangalia mandhari, halafu unarudi kwako. Kwa hiyo, ninaomba utusaidie kwenye huduma hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri ana mipango mizuri ya kuboresha Muhimbili. Sina shida na hiyo, lakini ninashauri ikiwezekana kupeleka huduma hizi, magonjwa mengine ni ya kawaida tu. Unaenda kwenye zahanati, hata ule mzani wa kupima mtoto tu uzito wake haipo. Hata mabenchi hayapo! Tuboreshe huduma kwenye zahanati, kwenye kituo cha afya, tuboreshe huduma halmashauri za wilaya, huduma za hospitali za rufaa za Mikoa, msangamano wa hospitali kubwa hizi utapungua. Tukifanya hivyo, itasaidia Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakushukuru sana kwa kazi. Nimeanza kusema Waziri hajawahi kushindwa kwenye Wizara yoyote. Anafanya kazi nzuri, lakini atusaidie kutoa huduma ambayo ni nzuri na Hospitali ya Muhimbili, tunaunga mkono kuboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshauri Mheshimiwa Waziri, pamoja na majengo ya ghorofa, tuwekeze kwenye utaalamu bobezi. Tuwekeze kwenye vifaatiba katika maeneo yetu, hata kama itakuwa chini ya mti, lakini kifaa kikifanya kazi, watu wakapata huduma ya matibabu, Mheshimiwa Waziri atakuwa ameacha alama kwa Watanzania na itamsaidia Mheshimiwa Rais kusaidia huduma za Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ninaunga mkono hoja. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Johannes Lembulung' Lukumay. Ajiandae Mheshimiwa Josephine Tabita Chagula na Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza.

**MHE. JOHANNES L. LUKUMAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kunipa nafasi hii ya kuchangia. Ninaanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kwa kuniwezesha kusimama katika Bunge lako Tukufu kuchangia Bajeti ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Arumeru Magharibi kwa kutoa kura nyingi kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na pia kwa kunipa kura nyingi, leo imesababisha nisimame hapa kuongea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua nafasi hii kuishukuru Wizara ya Afya kwa ujumla kwa kazi nzuri. Jana Mheshimiwa Nkingwa amemsema Waziri Mchengerwa, lakini Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa kweli ni mzalendo, amewasilisha vizuri. Huyu ni mzalendo kweli, amenitembelea, amefanya ziara katika Jimbo langu la Arumeru Magharibi. Alipofika, ameweza kusaidia kupatikana kwa barabara ya lami kama kilometa mbili hivi kwenda hospitali ya wilaya. Pia, ameshuhudia uwekezaji wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika hospitali la wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu ni mzalendo na wananchi wanampenda kweli. Ameahidi kwamba, atapeleka *ambulance* katika hilo Jimbo la Arumeru Magharibi. Watumishi wale ambao wamepungua atahakikisha kwamba, wanapatikana ili waweze kuwasaidia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umesema dakika sita tu. Ninaomba ni-*declare interest,* mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI. Ninaomba unipendelee dakika 10,

kama jana walivyokuwa wanafanya, ili niongee kidogo tu, kama utaridhia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa wengi jana wamechangia kuhusu Bajeti ya Afya. Ninawapongeza sana kwa kuchangia kuhusu Hospitali ya Muhimbili. Sina haja ya kurudia, ninawapongeza tu Waheshimiwa Wabunge, huu ni mradi mkubwa, ambao utaenda kubadilisha sura ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Muhimbili itapata ithibati ya Kimataifa. Kwa hiyo, tutaimarisha utalii, tunaita Tiba Utalii katika hospitali yetu, tutaimarisha mafunzo ya madaktari wetu, tutaimarisha tafiti katika nchi hii na tiba ya kisasa kutokana na mitambo mikubwa, ambayo imewekezwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, itaenda kutumika katika hospitali hii. Ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwamba mmeunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia na Mheshimiwa Dkt. Samizi, amekuwa kiungo kizuri sana, tulipotembelea na kufanya ziara, akiongozwa na Mheshimiwa Mchengerwa. Ninashukuru kwa kazi nzuri ambayo wameifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Afya imefanya kazi nzuri sana kwenye kinga. Ukiangalia suala la homa ya ini na shughuli nyingine wamefanya kazi nzuri, nawapongeza, lakini ninasema hivi tuimarishe kinga, Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana amesema Mheshimiwa Mahera, tuelekeze kwenye *primary health care,* ambako ndiko kuna hospitali ya wilaya, kuna vituo vya afya na kuna zahanati, watu wako kule kwa wingi. Ikiwezekana kama bajeti itaruhusu, hebu tuendeleze kuimarisha vituo vya afya. Akina mama wengi sasa hivi ndiyo wanajifungulia kule, tuimarishe kwa vifaa na kwa watumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nimeomba dakika 10 kwa sababu, mimi ni Mwenyekiti wa Kamati, nimalize tu. Kwa hiyo, ninaomba hilo la kinga Mheshimiwa Waziri lizingatiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, nitakuwa sijatenda haki nisipoongea kuhusu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya nini katika nchi hii? Ndiyo nikakuomba hizo dakika tatu hivi nimalizie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais amefanya mambo mengi katika nchi hii. Kwanza kabisa ukiangalia hospitali za Wilaya, amejenga hospitali 119, vituo vya afya 649, zahanati 2,700, ajira mpya 5,000, watumishi wa afya na madaktari bingwa na bobezi amewasomesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan hakuishia pale, katika vifaa vya tiba, ninaomba tusikilize tu kidogo; ukiangalia *MRI,* mnasikia watu wanasema, amekuta saba, amepeleka mpaka 13; *CT-Scan* amekuta 13, sasa hivi ziko 45; *Ultrasound* amekuta 476, sasa hivi ziko 970. *Cath Lab* ni mtambo mkubwa wa kupasua moyo kwa matundu madogo na mishipa ya damu, amekuta mbili sasa hivi ziko nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tu uvumilie kidogo. *Digital X-Ray*, zile za kisasa kabisa, unajua mambo aliyofanya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni vyema Watanzania wafahamu na tunasemea hapa.  Kuna *Min Lab* nzuri sana ziko nne, lakini *PET Scan* ameleta Hospitali ya *Ocean Road*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nivumilie dakika moja. Ukiangalia Hospitali ya…

*(Hapa, Kengele Ililia Kuashiria kwisha kwa Muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. JOHANNES L. LUKUMAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Josephine Tabitha Chagula.

**MHE. JOSEPHINE T. CHAGULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi hii, niweze kutoa mchango wangu katika hotuba hii ya Wizara ya Afya iliyoko mbele yetu. Ninaanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kunijalia afya njema na kuweza kusimama hapa leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa jinsi anavyopambana kuhakikisha Watanzania na nchi yetu inasonga mbele. Nampa hongera sana Mama yetu kipenzi kwa kazi nzuri. Pia, ninampongeza sana Waziri Mkuu pamoja na Baraza lote la Mawaziri kwa jinsi wanavyomsaidia Mheshimiwa Rais. Hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Waziri wa Afya, Mheshimiwa Mchengerwa, pamoja na Naibu Waziri, wifi yangu. Hongera sana kwa kazi nzuri wanazofanya kuhakikisha afya za Watanzania zinakaa imara. Hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na muda, ninaenda moja kwa moja kwenye mchango wangu. Katika Mkoa wa Geita tuna Hospitali ya Kanda ambayo iko Chato. Hospitali hii imekuwa ni msaada mkubwa sana katika ukanda ule. Wananchi wengi wameweza kunufaika pale. Hospitali ile inatoa huduma mbalimbali nzuri, na pia huduma za kibingwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweza kushuhudia wananchi wengi wanatoka sehemu mbalimbali, wengine kutoka Uganda, kuja katika hospitali ile kupata huduma. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuweza kutujengea Hospitali ya Kanda katika Mkoa wa Geita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto kidogo kuhusu upungufu wa madaktari bingwa. Kwa sasa tuna madaktari bingwa wawili. Ninaomba sana Serikali iweze kutupatia madaktari bingwa wa

kutosha kulingana na mahitaji ya pale. Wagonjwa ni wengi na huduma ni nzuri sana. Ninaomba sana Mheshimiwa Waziri aweze kuliona hilo na kutupatia madaktari bingwa ambao watatosheleza mahitaji ya hospitali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisemee Hospitali yangu ya Mkoa wa Geita. Hospitali ya Mkoa wa Geita inatoa huduma nzuri sana. Tunamshukuru sana Mganga Mkuu wa pale, lakini pia, tunawashukuru sana Madaktari Bingwa wa Watoto, Daktari Bingwa wa Akinamama, pamoja na madaktari wengine wote, wanafanya kazi nzuri sana kwa kiwango cha juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto iliyopo pale ni ukosefu wa jengo la mama na mtoto. Jengo la mama na mtoto bado halijakamilika, ujenzi wake umesimama kutokana na upungufu wa fedha. Pia, *mortuary* haijakamilika. Ninamwomba sana Waziri, Mheshimiwa Mchengerwa, alione hilo, atupatie fedha ambazo zitaweza kukamilisha jengo hili, ili akinamama na watoto wawe na jengo lao kwa sababu, kwa sasa wazazi inabidi wachanganyike na wagonjwa wa kawaida, kitu ambacho ni hatari sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza. Ajiandae Mheshimiwa Jesica Yuda Mbogo na Mheshimiwa Hamis Shabani Taletale atafuatia.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kupata nafasi ya kuchangia katika Wizara ya Afya. Awali ya yote, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Dkt. Samizi, kwa kazi nzuri wanayofanya. Mimi nakiri kwamba Mheshimiwa Waziri ni mfano bora wa uwajibikaji katika Sekta ya Umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na muda, ninaomba kipekee nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Yako mambo mengi ambayo ameyafanya ndani ya Mkoa wa Songwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyofahamu, Mkoa wa Songwe ulikuwa ni mpya, lakini ndani ya miaka mitano ya Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan tumepata hospitali ya mkoa, inafanya kazi; tumepata Hospitali ya Wilaya ya Songwe, imekamilika inafanya kazi; tumepata hospitali ya Mji wa Tunduma, inafanya kazi; na tumepata Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Momba, inafanya kazi. Vilevile tumepata jengo jipya la mama na mtoto katika Hospitali ya Wilaya ya Mbozi, jengo ambalo awali lilikuwa limechakaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mafanikio haya makubwa ambayo Mkoa wa Songwe tumepata kupitia Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, yako mambo machache ambayo natamani niishauri Serikali ili iweze kuyafanyia kazi na kufikia malengo ambayo anataka wananchi wa Mkoa wa Songwe waweze kuyapata kwenye Sekta ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ni kwenye Hospitali yetu ya Mkoa wa Songwe. Hospitali ile pamoja na kwamba, inafanya kazi, lakini kuna changamoto ndogo, kwamba jengo la wanawake na watoto bado halijakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Bunge la Kumi na Mbili Wabunge wa Mkoa wa Songwe tuliomba Serikali iweze kutoa fedha ili kukamilisha jengo la mama na mtoto. Tunaishukuru sana Serikali kwa sababu, mwezi wa 10 mwaka 2025 ilituletea shilingi 3,000,000,000 ambazo kimsingi zimesaidia sana kujenga *structure* ya ghorofa tatu. Vilevile, zitasaidia sana kumalizia miundombinu yote ya *floor* ya kwanza, ambayo kimsingi tutapata pale *operation room* mbili kwa ajili ya wanawake, na vilevile itatusaidia kupata vyumba vitano vya wanawake kujifungulia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Serikali, ninaomba sana Mheshimiwa Waziri atusaidie kwenye Hospitali ya Mkoa wa

Songwe. Bado shilingi 3,000,000,000 ambazo zikitolewa, zitasaidia sana kuweza kukamilisha jengo la mama na mtoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwenye Hospitali yetu ya Mji wa Tunduma, Mji wa Tunduma ni lango la *SADC*. Pale tunalo jengo la mama na mtoto ambalo kimsingi, bajeti yake ni shilingi bilioni 2.7, lakini mpaka sasa hivi, kwa masikitiko makubwa, tumepokea shilingi 300,000,000 tu ambazo zimetuwezesha kuanza kujenga msingi. Kwenye bajeti yetu ya mwaka huu imetengwa shilingi 100,000,000 ambayo kimsingi ni fedha ndogo, itachukua muda mrefu sana kuweza kukamilisha jengo la mama na mtoto kwenye Mji wa Tunduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Mji wa Tunduma ni lango la *SADC*. Tunaishukuru Serikali, ndani ya Awamu ya Tano tumepata vituo vya afya sita. Kwenye vituo hivyo, kituo kimoja cha afya cha Tunduma kinazalisha watoto 800 kwa mwezi, siyo kwa mwaka. Kituo kimoja cha Chapwa kinazalisha watoto 300 mpaka 400 kwa mwezi. Hospitali ya Mji wa Tunduma kwa mwezi inazalisha watoto 400 mpaka 500. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi hii ni kubwa sana kwa sababu, hospitali ile inahudumia siyo tu Watanzania, lakini pia watu kutoka kwenye Mataifa mengine. Ninaomba, changamoto kubwa ambayo inatukumba kwenye Mji wa Tunduma ni ukosefu wa watumishi. Watumishi wanaofanya kazi kwenye vituo vya afya hivi vipya vya Mji wa Tunduma wanafanya kazi kwenye mazingira magumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru Rais wetu kwa sababu, juzi ametoa kibali cha kuajiri watumishi 5,000. Tunashukuru kwa sababu, kwenye Wilaya ya Ileje mmetuletea watumishi, lakini bado kwenye Mji wa Tunduma hatujapata mtumishi hata mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri, tunafahamu uwajibikaji wake, tunafahamu uchapakazi wake, ninaomba aangalie Mji wa Tunduma kwa jicho la tofauti. Bahati nzuri mtendaji wa Wizara hii alimewahi kuwa *RAS* wa Mkoa wa Songwe.

Kaka yangu Shekilage ninamwomba sana, akumbuke Mkoa wa Songwe, aangalie Mji wa Tunduma kwa jicho la tofauti. Afanye atakavyofanya atuletee watumishi katika Mji wa Tunduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Hospitali ya Wilaya ya Momba, ambayo nayo imekamilika, tunashukuru. Jengo la Mama na Mtoto limekamilika na huduma pale zinaendelea, lakini bado tuna idadi ndogo sana ya watumishi. Tunahitaji vilevile kuweza kupata mtaalamu wa mionzi pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninataka nizungumzie ni kuiunga mkono Serikali kwa jambo lake ambalo imeleta la kujenga upya Hospitali ya Taifa ya Muhimbili. Hospitali ile ni ya Taifa, siyo ya wilaya, siyo ya mkoa, siyo ya kanda, ni Hospitali ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na historia ya Hospitali ya Muhimbili ambayo muda hautoshi siwezi kuielezea, lakini kutokana na uchakavu wa miundobinu wa hospitali ile na msongamano wa watu, ninachelea kusema kwamba, sisi kama Taifa tumechelewa sana kuijenga Hospitali Mpya ya Muhimbili.

*(Hapa, kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Waziri aweze kuangalia namna gani ambavyo...

**MWENYEKITI:** Muda wako umeisha Mheshimiwa.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba, Mheshimiwa Waziri amesema kwamba, Hospitali ya Muhimbili itakamilika ndani ya miaka mitano. Tunatamani hii ndiyo iwe *legacy,* ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan atatuachia Watanzania. Ndani ya miaka mitano tunaomba hospitali iweze kukamilika.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile waweze kutusaidia zile shilingi 3,000,000,000 ambazo zimetengwa kwa ajili ya kumalizia Hospitali ya Mkoa wa Songwe. Tutakapopitipisha bajeti yake hapa leo, aweze kuzitoa hizo fedha na Hospitali yetu ya Mkoa wa Songwe iweze kukamika, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilimtaja Mheshimiwa Jesica Yuda Mbogo.

**MHE. JESCA Y. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Awali naenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa kibali cha kuweza kufika hapa leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Mkoa wa Dodoma tusiposema, tutakuwa wachoyo wa fadhila. Sisi Mkoa wa Dodoma Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametutendea haki sana. Ametutendea haki kwa majengo mazuri, kwa vituo vingi kutoka 2021 vituo 429, mpaka Aprili mwezi uliopita vituo 699. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunayo haja ya kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Dodoma tunampongeza na tunamshukuru sana kwa kumwangalia mama na mtoto kwenye mkoa wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameondoa vifo vya mama na mtoto katika Mkoa wa Dodoma, ameendelea kuwa kinara kwa kuwasaidia akina mama wa Mkoa wetu wa Dodoma. Amehakikisha mazingira mazuri ya mwanamke wakati anakwenda kujifungua kwa kutoa vifaatiba, na mazingira ambayo yanamfanya mwanamke awe *comfortable*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda pale *General Hospital* sasa hivi ninaipongeza sana Wizara ya Afya, wameweza kuboresha, wameweka kitengo rasmi cha *emergence,* mwanamke akifika pale

anaangaliwa huyu aende kwenye operesheni, au aende wapi? Kwa kweli wameboresha sana hospitali yetu ya *General*. Zamani ilikuwa changamoto ni kubwa, tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo changamoto za watumishi, kwenye mkoa wetu, mahitaji ni makubwa sana ya watumishi wa afya. Tuna uhitaji wa watumishi wa afya 10,000 lakini sisi tuna watumishi 4,000. Unaenda kwenye hospitali za Wilaya unakuta Daktari mmoja anahudumia eneo kubwa mpaka unajiuliza, huyu Daktari anapumzika saa ngapi? Maana usiku unamkuta yeye, asubuhi unamkuta yeye. Kwa hiyo, changamoto hii ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana wale vijana ambao wamewapa ajira za kujitolea, basi wawapatie ajira hizi, kwa sababu wanajitolea muda mrefu kwenye idara hiyo, lakini hawapewi hizo nafasi za kwenda kuhudumu kama waajiriwa kwenye sekta hiyo ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana, wapo vijana wetu kwenye Wilaya wanajitolea muda mrefu, miaka mitatu, minne wanajitolea, lakini wakija, wanaajiriwa wengine kwenye idara hiyo ya afya. Kwa hiyo, ninaomba sana kwenye idara hii ya ajira mtufikirie sana watumishi wa afya Mkoa wa Dodoma, ingawa tunashukuru, wapo, lakini tunaomba sana mtusaidie kutuongezea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hii sera ya matibabu bure, wenzangu wengi wamezungumza, na mimi nizungumze. Mkoa wangu wa Dodoma bado sera hii haitufikii vizuri wanawake. Unakwenda kujifungua, unaambiwa utalipia matibabu, lakini bado unaambiwa utajifungua kwa kuchangia na vifaatiba vingine. Utakuta mzigo ni mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanamke wa kijijini ukimwambia atoe shilingi 250,000 kwa operesheni ni fedha nyingi sana. Shilingi 250,000, bado atoe shilingi 250,000 hiyo, lakini bado anaambiwa alete na vifaa vingine! Tunaomba sana Wizara iangalie jambo hili. Jambo hili limekuwa likiwasumbua sana wanawake wakienda kujifungua. Jambo

hili linafanya wanawake wengi wanajikuta sasa wanazalia nyumbani kitu ambacho siyo kizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko vijijini kwetu mtu anaona bora aende akazalie nyumbani. Ninaomba sana watuangalie Wizara ya Afya, hasa kwenye jambo hili la vifaatiba, kwani ni jambo ambalo mwanamke yeyote anatamani kujifungua akiwa salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie habari ya uhaba wa vitanda. Kuna maeneo, kwenye hospitali nyingine ukienda bado vitanda havitoshelezi kwa wanawake. Unakuta wanawake wengine bado wanajibanabana kwenye vile vitanda. Kwa hiyo, ninaomba Wizara iendelee kutufikiria katika kuboresha mazingira haya ya kumsaidia mama na mtoto, basi tuhakikishe kwamba vitanda vinatosheleza katika kumsaidia mwanamke kujifungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Hamisi Shabani Taletale, ajiandae Mheshimiwa Zena Maulidi Katambo, na Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi atafuatia.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaanza na neno la pongezi kwa Waziri wa Afya, babu yangu Mheshimiwa Mchengerwa. Pia ninampongeza Katibu Mkuu wake, na vilevile nisiache kumpongeza na Mganga wetu Mkuu, dada yangu. Ndugu yangu, Mheshimiwa Mchengerwa, Wizara yake imeenea na mambo yako meupe kama suti yake ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mkazi wa Mkoa wa Morogoro, Mkoa wetu wa Morogoro kwa ujumla kwa nchi hii ni Mkoa namba mbili kwa ukubwa. Kaka yangu, Mheshimiwa Mchengerwa anajua, mwaka 2023/2024 tulipokea ugeni wa Mheshimiwa Rais, alikuja, na nilisimama nikaomba kwa Mheshimiwa Rais kwamba hospitali yetu ya Mkoa wa Morogoro hali yake siyo nzuri, *traffic* ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tuna *traffic* kubwa, amezungumza jana kaka yangu Mheshimiwa Shabiby hapa, sawa tunapata huduma vizuri, lakini je, majengo yale mimi tangu mtoto yapo vilevile, ndugu yangu Mheshimiwa Mchengerwa, kweli! Mimi ninamfahamu Waziri, ni mtu wa viwango, mtu wa vitendo, nikizungumza kwenye hili, ninajua nimemgusa moyo wake, ataenda kuiangalia Hospitali ya Mkoa wa Morogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii sisi tunaitazama *SGR* kama jambo kubwa sana....

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Clayton Chipando, kwa mujibu wa Kanuni, hauruhusiwi kumkatisha msemaji, ninaomba urudi ulipotoka.

Mheshimiwa Hamisi Taletale, endelea. *(Makofi)*

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii sisi wakazi wa Morogoro na Watanzania kwa ujumla tunaitazama *SGR* kama ndiyo jambo letu la utalii. Tunaangalia sisi wakazi wa Morogoro, hospitali tunayoitegemea, amezungumza dada yangu pale Mheshimiwa Juliana Shonza, ni Muhimbili. Muhimbili ni *National Hospital,* lakini siyo kila mtu anaweza akakodi ndege, siyo kila mtu anaweza akachukua *ambulance* kutoka Morogoro kwenda Muhimbili. Tuangalie leo hii tumeletewa *SGR,* kwa nini tusije na *ambulance* ndani ya ile *SGR*? Tunashindwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaamini Rais wetu ni msikivu, atalifanya hili kiurahisi. Tutengeneze, tufanye *modern*, vitu kama hivi wenzetu ng'ambo wanaweza, kwa nini tusiwe sisi? Je, lini linaweza kufanyika hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mdau mkubwa na mdau namba moja wa Hospitali ya Muhimbili. Kwa nini nasema hivyo? Mimi ni kama balozi wa ile hospitali. Nimemsikia Mheshimiwa Mchengerwa akizungumzia bajeti yake hapa; mimi sitakaa kumshikia shilingi, wala kushikia shilingi bajeti, ila ninaweza nikaomba ikiwezekana tuiongezee hata fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi Muhimbili ninaifahamu vizuri, wagonjwa wetu wanaotokea Morogoro vijijini wakitoka *referral* wanapelekwa Muhimbili. Sasa leo hii Muhimbili ina changamoto ya magari ya wagonjwa, ana ushahidi Mheshimiwa Mchengerwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wagonjwa kutoka Muhimbili kwenda Mloganzila, kuna magari mawili tu. Kwa nini? Kwa nini tuna magari mawili? Labda wafanyakazi wake wanamwogopa kumwambia, aende akatembee Muhimbili, magari ya wagonjwa *(ambulance)* yapo mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninao ushahidi, juzi wakati ninahangaika na mwenzetu mmoja wa muziki, gari zipo mbili. Wagonjwa wapo wawili pale! Haiwezekani. Tuangalie nini kifanyike? Ninampongeza Mheshimiwa Mchengerwa, huko nyuma alishawahi kunipa mpaka gari la *ambulance,* basi nenda akaongeze *ambulance* Muhimbili. Hili kwetu linawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, lakini siyo la umuhimu. Tunayo changamoto, amesema jana kaka yangu Mheshimiwa Shigongo hapa kuhusu homa ya ini. Hili gonjwa ni kubwa sana. Leo hii mtu akipata homa ya ini anakula *RV* kama vile ni chai. Sasa nani wa kututazama katika hili? Huko nyuma tulikuwa tunafanya chanjo pale Muhimbili, sijui kama mpaka leo bado ipo, lakini na ile *awareness* ya watu kujua kama kuna tatizo la ugonjwa wa homa ya ini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wengi wanakufa na wengine wanakufa ghafla na *stress* kwa sababu akianza kutumia *RV* anajiona ooh! Kushnei (kwisha habari yake); lakini kama tunaweza kusimama kama Wizara ya Afya kwenda kuwaelimisha vijana, kuna shida na kuna changamoto la gonjwa la homa ya ini, hili litatusaidia na kupunguza namba ya maambukizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugonjwa huu una kinga kwa chanjo ya mara tatu. Mheshimiwa Mchengerwa sisi tunamwita Mtu Kazi. Mtu Kazi haswa, na kama nilivyosema mwanzo, suti yake nyeupe, ina kitu ndani

yake. Aende akaokoe vijana, maana homa ya ini mtu akipiga chafya tu anaipata. Homa ya ini siyo mpaka watu wajamiiane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunajazana kwenye madaladala, tunajazana kwenye mwendokasi kwenye kugombea kuingia, mwisho wa siku watu tunaambukizana huu ugonjwa na watu hawafahamu kwa sababu hawana elimu. Hili jukumu linatoka wapi kama siyo kwa Wizara ya Afya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mchengerwa awaambie wataalam wake wasimame wainue Taifa. Taifa linaangamia kwa sababu ya kutokupata maarifa ya gonjwa la homa ya ini. Hili lipo chini ya Wizara ya Afya, tokeni simameni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimekuwa nikizungumza hili suala, na hata humu ndani kuna Wabunge hawajachanja chanjo ya homa ya ini. Basi tuletewe watu pale wachanje ili hili suala liishe. Tunaogopana hapa kwa sababu hili gonjwa lipo, na kama halipo, watu wanatakiwa wafahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema haya machache, ninamwomba kaka yangu Mheshimiwa Mchengerwa, hospitali yetu ya Wilaya inafanya kazi vizuri, lakini bado kuna changamoto ndogo ndogo. Niliongea vizuri na Mheshimiwa Katibu Mkuu, naomba ikipendeza waje Morogoro vijijini watutembelee. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Zena Maulidi Katambo.

**MHE. ZENA M. KATAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa nafasi hii uliyonipatia na mimi niweze kushiriki katika kutoa maoni yangu katika mchango wa mapendekezo ya bajeti ya Wizara hii ya Afya ya Mwaka 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Waziri wa Afya, Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa. Sisi wote na wananchi kwa ujumla tumeshuhudia katika hiki kipindi kifupi ambacho ameshika

Wizara hii, amefanya mambo makubwa, ametekeleza miradi mikubwa na ametuletea dira ambayo inaonesha kwamba nchi yetu kama tutaenda kutekeleza hii miradi ambayo Wizara hii inatuomba fedha leo, tunakwenda kwenye ile nchi ya ahadi kwa upande wa sekta ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Samizi ambaye kwa pamoja na Mheshimiwa Waziri wamekuwa wakishirikiana kuhakikisha kwamba Wizara hii inakwenda vizuri. Mheshimiwa Dkt. Samizi ni mtu mkarimu sana kwa kweli, Mwenyezi Mungu ambariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninapenda kuipongeza Serikali kwa uwekezaji mkubwa ambao umefanywa katika sekta ya afya. Katika sekta hii, wote ni mashahidi kwamba Serikali imejenga miradi mbalimbali ya kutolea huduma za afya kuanzia Hospitali za Rufaa za Mikoa, Hospitali za Mikoa, lakini na vituo vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika huduma hizi za hii miradi ambayo Serikali imetekeleza kwa Mkoa wa Lindi, tunashukuru sana kwa kuletewa ule ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ambapo kwa sasa Mkoa wa Lindi tumepata hospitali ya rufaa na wananchi wanakwenda pale kupata matibabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, tunafahamu sera ya nchi hii kwa sekta ya afya ni kuhakikisha kwamba kila Kata inakuwa na kituo cha afya. Kwa upande wa Mkoa wa Lindi hali yetu siyo nzuri kwa upande wa miundombinu ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakutolea mfano wa huduma za vituo vya afya. Kwa mfano kwa Wilaya ya Nachingwea tuna vijiji 129, kati ya vijiji 129 tulivyonavyo, tuna zahanati 49 pekee, lakini pia kwa upande wa vituo vya kutolea huduma za afya Wilaya ya Nachingwea ina Kata 36 ambapo kata hizi zote kama ile sera ya kituo cha afya katika kila Kata ingetekelezwa, tungekuwa na vituo vya afya 36. Kwa sasa ninasikitika kusema kwamba, Wilaya ya Nachingwea inavyo vituo vya afya viwili ambavyo vinafanya kazi *effectively,* vituo vingine vya

afya viwili vinaendelea kujengwa, lakini vinajengwa kwa mapato ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kwamba hizi Halmashauri zetu hali ya uchumi siyo nzuri. Kwa hiyo, utekelezaji wa ile miradi unasuasua. Kwa hiyo, wananchi wa Mkoa wa Lindi tunamwomba Mheshimiwa Waziri atuangalie kwa jicho la pekee tuongezewe vituo vya afya, tuongezewe zahanati ili na sisi tuweze kuhudumiwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika suala la miundombinu ya huduma za afya nina ushauri kidogo. Ninaishauri Serikali ibadilishe sera yake ya majengo hasa ya vituo vya afya. Zile *labour* ambazo akina mama tunazitumia tukiwa katika kipindi cha kujifungua, zipo kama ma-*hall* yaani kwamba ni ukumbi, kila mtu anaingia. Ni vitanda tu vimepangwa, tunakosa staha wakati tukiwa tunajifungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, suala la kuboresha ile miundombinu ni suala rahisi, halihitaji gharama kubwa. Kwa kupitia Wizara tunaweza tukaelekeza kwa kushirikiana na TAMISEMI angalau vile vituo ambavyo tayari vipo, tukaenda kuboresha ile miundombinu ili ituwezeshe katika kile kipindi cha kujifungua, tujifungue kwa staha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninaipongeza Serikali kwa sera ya Bima ya Afya kwa Wote. Katika sera hii ya Bima ya Afya kwa Wote, sisi wananchi wa Lindi ambao tunatumia ushirika katika mazao yetu tulikuwa tunaomba, tunavyofanya biashara za mazao...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, muda wako umekwisha.

**MHE. ZENA M. KATAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyofanya biashara za mazao, kuna ushuru. Kule tunakatwa na zile *agency* ambazo zinapata ule ushuru. Wale ni watu ambao wanatuhudumia sisi wanachi wa Mkoa wa Lindi. Tunaomba Mheshimiwa Waziri akae

nao kwa sababu ni wa kwetu. Kama watakaa pamoja, hawatakataa kuchangia angalau shilingi 15 kwa kilo ili kusudi wakulima wa Mkoa wa Lindi tunufaike na Bima ya Afya moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, ajiandae Mheshimiwa Kijakazi Yunus Mohamed.

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba kusisitiza, tukisikia kengele ya pili, tafadhali uwe umemaliza ili wachangiaji wengine wapate nafasi.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye bajeti hii muhimu ya Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuamua kwa dhati ya moyo wake kuweka fedha katika Hospitali ya Muhimbili. Ninampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu kwa jambo hilo alilolifanya, ni jambo kubwa kwa afya za Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninapenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Afya, Naibu Waziri wa Afya, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu, nitaanza na Hospitali ya Temeke. Hospitali hii ina idadi ya wagonjwa ambao wamepitia katika hospitali ile kwa mwaka 2005, wamefikia 605,772. Akina mama wajawazito walioenda kujifungua ni 6,190; wagonjwa wa afya ya akili na mengineyo ni 5,124 lakini bado kuna wagonjwa wengine ambao wanatoka katika hospitali mbalimbali ikiwemo hospitali ya jimboni kwa Mheshimiwa Waziri, wagonjwa wote wa Rufiji, Mkuranga wote wanafikia kwenye Hospitali ya Temeke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali yetu ya Temeke ni hospitali ya Mkoa ambayo waliitwaa kutoka katika Halmashauri ya Temeke. Kinachoshangaza ni kwamba, tokea wameitwaa hospitali ile hakuna mwendelezo. Wodi sasa zimekuwa kama vibanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri, ameona changamoto mbalimbali zinatokea katika Hospitali ya Temeke. Mara *X-Ray* imezimwa, mara wananchi wanalalamika hivi, mara kuna changamoto kibao. Hayo yote nayo yanatokana na kwamba pale Temeke bado, kumekuwa kama hospitali ya Kijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Serikali imejenga Hospitali ya Zakhem, lakini ikapime Hospitali ya Zakhem, ni kituo cha afya tuseme, na ile hospitali ya pale Ilala inafanana na hospitali ya Mkoa wa Temeke! Haifanani. Hospitali ya Mkoa ni hospitali kubwa, inatakiwa iwe ina mambo mengi, iwe ina majengo mazuri, iwe na wataalamu, iwe na watumishi wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona waliyoyafanya, wameingia pale Hospitali ya Temeke, wameunda Tume, Tume imefanya kazi; wamebadilisha uongozi, lakini pamoja na kubadilisha uongozi ili tumsaidie Dkt. Mfaume, waboreshewe na mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madaktari wanadai hizo *service call* zao za kufanya kazi. Wanafanya kazi za ziada, lakini hawana mapato, hawalipwi. *Service calls* zao hazipatikani. Kwa hiyo, madaktari wa Temeke wapo, wanakwambia, mama sisi hapa Temeke shilingi 5,000 kwetu, kwenda *cafe* kula, daktari anaona yaani hawezi. Haiwezekani, Temeke ni mjini. Temeke ina wakazi 570,00 kwa mujibu wa sensa. Kwa hiyo, bado tunahitaji maboresho pale Temeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapotaka kulijua jambo lako liko bovu kiasi gani, nenda Amana, nenda Mwananyamala; kule mambo ni mazuri. Hapa Temeke kuna nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa waziri kwa moyo wake mzima kabisa aisaidie Temeke. Temeke bado inahitaji msaada, inahitaji maboresho makubwa sana. Nimwombe, na ninamtambua, na Mheshimiwa Naibu Waziri na Waziri, kwamba wote wao ni Wanatemeke. Basi sina mashaka kabisa kwamba wataitendea haki Hospitali ya Temeke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije kwenye Hospitali yetu ya Muhimbili. Hospitali ya Muhimbili jamani leo kuja kuletwa hapa, kwamba inataka kujengwa upya, ni jambo kubwa. Ndugu zangu ni jambo kubwa. Hospitali ya Muhimbili ipo pale tangu mwaka 1905, wakati wa Vita ya Maji Maji hadi leo hii, hivi kwelli ni stahiki yake! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumpongeze Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuamua kwa dhati. Wapo watu wanaelezea eneo la Hospitali ya Muhimbili ni *square meter* 176,000 lakini maboresho yanakwenda kufanyiwa katika *square meter* 46 tu. Majengo ya ghorofa yapande juu, yaende sambamba na hospitali zile za kanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitaka kujua, simama pale Muhimbili, angalia dakika tano hiyo inakuja *Ambulance* ya Halmashauri ya Handeni; dakika tano hiyo inakuja *ambulance* sijui ya halmashauri gani, zinaingia pale kwa sababu wagonjwa wale wanatoka rufaa katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pamoja na kutaka mambo mengi, tuna mambo ya *AFCON* na nini, lakini je, Tanzania ina hospitali ya Kitaifa? Hapana, hospitali ya Kitaifa ijengwe. Pamoja na kuwa nami ni mwana-*heritage* nimeona kwamba yale majengo ya Mwaisela, Kibasila, Sewa Haji yatabakia kama majengo ya kihistoria. Kwenye *by laws* ya *culture heritage* na *historical* inasema hivi, nayo yanaweza kukarabatiwa ilimradi yasibadilishwe muundo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba, pamoja na kujenga hospitali mpya, na zile wodi za Mwaisela, Sewa Haji ziingie katika ukarabati mkubwa, ilimradi wasibadilishe ule muundo wake.

Mimi ninaomba tuienzi hospitali yetu. Kila mmoja amepitia, kama sio wewe, ndugu yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muhimbili kuna changamoto; mtu anatolewa *OPD* pale jirani na wazazi, anabebwa kwenye baiskeli. Tusione kuwa sisi tuna magari; kwa kutumia baiskeli anapelekwa nginjangija hadi Mwaisela. Hivi ni kweli kuwa Hospitali ya Taifa inatakiwa iwe hivyo! Hapana, ni lazima ijengwe, na niseme kwamba tumechelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuamua kwa dhati ya moyo wake. Mama huyu ni wa huruma, wa upendo, nimwambie mama yangu chapa kazi, chapa kazi, Watanzania watakukumbuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walisema *SGR,* leo *SGR* hiyo inatubeba wote. Bwawa la Mwalimu Nyerere…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako, muda wako umekwisha.

**MHE. MARIAM N. KISANGI: …** leo hiyo changamoto ya umeme imeondoka. Kwa upande wa bandari; mimi natoka bandari *TMK*, makontena…

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa

**MHE. MARIAM N. KISANGI: …** yamejaa, bado nusu, jimbo langu lote mwisho litapotea. Haya tuyaulize kule nyuma…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam Kisangi muda wako umekwisha.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** …alikuwa wapi kama siyo *DP World? (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam Kisangi, muda wako umekwisha.

**MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilimtaja Mheshimiwa Kijakazi Yunus Mohamed. Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete, na Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma wajiandae.

**MHE. KIJAKAZI Y. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara hii muhimu sana kwetu sisi Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote na mimi nitumie nafasi hii kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Lindi na wananchi kwa ujumla, wamenituma nimshukuru na nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa mengi aliyoyafanya katika sekta kwenye Mkoa wetu wa Lindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea, ninampongeza sana babu yangu, mtani wangu Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, pamoja na Naibu wake, Waziri na Watendaji wote wa Wizara ya Afya wakiongozwa na Katibu Mkuu, wanafanya kazi nzuri, kazi kubwa, kazi iliyotukuka. Tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianzia, pale katika mkoa wetu wa Lindi, imewekezwa takribani shilingi 9,000,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya rufaa ya mkoa pamoja na vifaatiba. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Lindi na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nimshukuru sana Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, kwa sababu baada ya majengo yale kukamilika ulipita muda kidogo kabla ya kuanza. Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa baada ya kuteuliwa tu kuwa Waziri, alifanya jitihada kuhakikisha kwamba hospitali ile ya rufaa inaanza kazi. Tunashukuru sana. Pamoja na kwamba hospitali ile imeanza kazi,

tunazo changamoto, majengo hayajakamilika kwenye hospitali ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti iliyopita, tuliahidiwa au ilitengwa shilingi bilioni 5.4 ambayo hadi sasa haijaenda. Inawezekana fedha ile ingeenda, ingeweza angalau kukamilisha baadhi ya majengo. Ilitoka *almost* shilingi 1,000,000,000 tu ambayo ilienda kumlipa mkandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, changamoto ni kubwa kwa sababu moja kati ya changamoto ni majengo ya kulaza wagonjwa *(Wodi)* ambapo kwa sasa majengo ambayo yanayotumika ni ya *OPD* pamoja na jengo la *ICU*. Wodi hizo ni pamoja na wodi ya mama na mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja ku-*wind up* atuambie wananchi wa Mkoa wa Lindi ni lini majengo yale yatakamilika? Ninaomba *commitment* ya Serikali, kwa sababu nimesikia asubuhi Mheshimiwa Naibu Waziri akieleza kwamba mwaka huu Disemba hospitali ile itakamilika. Kwa hiyo, tunaomba *commitment* ya Serikali na watwambie mipango na mikakati ipi ambayo wataitumia kuhakikisha kwamba hospitali ile muhimu kwa wananchi wa Mkoa wa Lindi inakamilika. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Muda wako umeisha.

**MHE. KIJAKAZI Y. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete.

**MHE. GHATI Z. CHOMETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi ya kuchangia. Nami nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa, kazi nzuri

anayoifanya katika sekta hii ya afya. Pia ninampongeza Waziri wa Afya, Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa; tunapenda kumwita Mtu Kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri akiwa kwenye Wizara, ni kweli anaisimamia vilivyo. Tumemwona akiwa katika Wizara tofauti tofauti, anafanya vizuri na Wizara inachangamka. Hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri. Ni yeye pamoja na Naibu Waziri, dada yetu Florence na wafanyakazi wote wa Wizara ya Afya, tunawapongeza kwa namna wanavyofanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze pia wote wanaofanya kazi katika sekta ya afya kwa Mkoa wangu wa Mara. Tumeona kwa namna wanavyowahudumia wananchi wa Mkoa wa Mara katika sekta hii ya afya. Nimesema ninampongeza Rais kwa namna anavyotuletea fedha za miradi ya sekta hii ya afya katika Mkoa wetu wa Mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa muda mrefu Hospitali ya Mwalimu Nyerere ilikuwa haifanyi kazi, lakini kwa huruma za Mheshimiwa Rais, ameleta fedha nyingi, na sasa hospitali ile inaendelea kufanya kazi kwa kuwahudumia wananchi wa Mkoa wa Mara na maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo, bado kuna changamoto. Tunashukuru tumepokea miradi tofauti tofauti. Tumepokea mradi wa Kituo cha Damu Salama kwa shilingi 1,000,000,000, tumepokea mradi wa umeme kwa shilingi 4,000,000,000, pia tumepokea mradi wa wodi ya watoto wenye changamoto ya uzito kwa shilingi 1,000,000,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, bado tuna changamoto. Fedha ambazo nimezisema hapo hazijaletwa. Bado tunaomba shilingi 14,000,000,000 kwa ajili ya kumalizia Hospitali ya Mwalimu Nyerere, bado fedha hizo hazijaletwa. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri, yeye ni kijana wa Mwalimu Nyerere, tumemsikia mara nyingi kwenye nukuu

zake akinukuu nukuu za Mwalimu Nyerere, na hospitali ile ni jina la Mwalimu Nyerere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba shilingi 18,000,000,000 ambazo zinahitajika kwenda kumaliza miradi kwenye ile hospitali, azipeleke ili Wanamara waendelee kupata neema. Siyo Mara tu, hospitali ile inahudumia wananchi kutoka Kenya, Simiyu, na maeneo mengine yaliyouzunguka Mkoa wa Mara. Ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri, kwa unyenyekevu mkubwa akaitazame hospitali ile ili kusudi fedha ziende, miradi ile iweze kukamilika *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, tuna daktari pale wa saratani ambaye yupo pale, lakini hatuna maabara ya saratani. Wagonjwa wengi wa Mkoa wa Mara ambao ni mama zangu, wana saratani ya matiti, saratani ya damu, na saratani ya utumbo. Hatuna maabara. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri alitazame hilo. Sambamba na hilo sisi Wanamara tunamtegemea sana Mheshimiwa Waziri katika huduma hizi ambazo anatarajia kuzifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kuisemea huduma ya bima ya afya ambayo ni kielelezo kikubwa cha Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Anatamani kila Mtanzania aweze kupata huduma hiyo ya bima ya afya. Tunaomba elimu kubwa itolewe kwa watu wa chini, ili waweze kuelewa maana ya huduma hiyo ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, pale wanapoenda kupata huduma, wapate huduma ya vifaatiba, viwepo kwenye vituo, na huduma ya dawa iwepo kwenye vituo. Siyo kwamba mtu awe na bima ya afya halafu anapofika kwenye kituo, anakosa huduma hiyo, siyo jambo jema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee pia kumsifia na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa ujenzi unaotarajiwa kufanyika wa Muhimbili mpya. Ni jambo ambalo kila Mtanzania anatamani Muhimbili mpya ijengwe; na hii Mheshimiwa Rais ametamani kuwaletea Watanzania na kuwaacha na tabasamu.

Itakapojengwa Muhimbili mpya, ataleta tabasamu na kuwaachia Watanzania tabasamu kubwa katika Muhimbili mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma. Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, na Mheshimiwa Naomy Dancan Mwaipopo wajiandae.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia. Nitaanza alipoishia Mheshimiwa Ghati. Tunapozungumzia suala la Muhimbili mpya, hili jambo kama itakumbukwa, tangu mwaka 2020 lilishaanza kusemwa. Kwa hiyo, ninampongeza Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mapenzi yake dhidi ya afya ya Watanzania kwa kuamua kuendelea na mradi huu wa Muhimbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati umefika sasa tuipate Muhimbili mpya, kwani majengo yake ni ya muda mrefu sana, yamechakaa. Pia majengo haya ya Muhimbili yamechoka, yana umri takribani wa miaka 100. Yaani ukiuchukua umri wa mzee wetu Kabudi humu ndani na yale majengo ya Muhimbili, Muhimbili ni kubwa kuliko umri wa Mzee Kabudi. Kwa hiyo, tunahitaji kama Watanzania Muhimbili mpya. Rais wetu ana mapenzi na afya ya watu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha, atupe maelezo ya kina, mchanganuo wake umekaaje? Kiasi gani kinaenda kwenye ujenzi; na kiasi gani kinaenda kwenye vifaa? Tuseme sisi kama Watanzania tuna kiu kubwa sana ya mradi huu, kwa sababu siyo jambo jipya, ni jambo ambalo limeshakuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi nina imani kubwa naye, anafanya kazi kubwa na nzuri. Watu wa Rufiji ni mashahidi katika hilo, na ndiyo maana wakampa jina la Mchengerwa (Mtu Kazi). Pia anaye Naibu Waziri mzuri ambaye anafikika, Naibu Waziri ambaye

anachukua matatizo ya Watanzania, ni hodari kupokea simu. Mheshimiwa Dkt. Samizi ni mwepesi kwenye simu, hata saa saba usiku amekuwa akipokea simu na akitusaidia changamoto za afya za wananchi wetu. Ninampongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kumsaidia Waziri wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka sasa kuzungumzia *NCDs,* yaani magonjwa yasiyoambukiza. Tishio la magonjwa yasiyoambukiza limekuwa likiongezeka kwa kasi kubwa nchini; na bajeti kubwa ya Wizara hii ya Afya imekuwa inaenda kutibu magonjwa haya yasiyoambukiza, hali ambayo inasababishia mzigo mkubwa kwa Mfuko wetu wa Bima ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano. Kwa mwaka 2025/2026 51% ya malipo yameenda kulipia magonjwa haya yasiyoambukiza. Sasa, inabidi hatua za haraka zichukuliwe, vinginevyo tutaufanya Mfuko wetu wa Bima ya Afya kujiendesha kwa nakisi. Nasi tunatamani mfuko huu ufike mahali, ujiendeshe kwa ziada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana *DG* wa mfuko huu wa *NHIF,* dada yangu Irene Isaka, anafanya kazi nzuri sana yeye na watendaji wake, hususan wale watendaji waliopo hapa ndani ya Bunge, Flora pamoja na mwenzie Neema, wanafanya kazi nzuri sana kwa kushirikiana na Wabunge wanapokuwa na changamoto za wananchi wao au wanapopata changamoto za bima ya afya kwenye hospitali mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfuko umekuwa ukiendelea kuendeshwa kwa nakisi kwa mfululizo wa miaka mitatu, lakini mpaka nusu ya mwaka huu tuliokuwanao mfuko umeanza kufanya vizuri kwa kutengeneza ziada. Ndiyo maana ninamwomba Mheshimiwa Waziri, kwenye suala la magonjwa yasiyoambukiza inabidi kazi ya ziada ifanyike. Nitaiomba Wizara itoe elimu kwa Watanzania juu ya masuala ya kuwasaidia Watanzania kujua visababishi vya magonjwa yasiyoambukiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa pili kwenye suala hili, ili tupunguze magonjwa yasiyoambukiza, kwa sababu bajeti kubwa inaenda kutibia huko, ni pamoja na ile kampeni waliyoianzisha ya jua namna yako. Ile kampeni ni nzuri sana. Ninachokiomba itembee kwenye mikoa yote na kwenye wilaya zote. Watanzania tunatakiwa tuwe makini na lishe, kwa sababu tusipokuwa na lishe iliyokamilika ndiyo mwanzo unaotupelekea kuwa na uzito mkubwa, presha, na sukari. Matokeo yake Wizara inabeba mzigo mkubwa wa kwenda kutibia magonjwa haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, vingine nitavileta kwa maandishi. Ahsante sana kwa kunipa nafasi, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, ajiandae Mheshimiwa Naomy Dancan Mwaipopo.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza tunawapongeza watendaji wa wizara hii, tukianzia na Waziri, Mheshimiwa Mchengerwa anajiita *Castron*. Mtendaji mzuri sana huyu, tulikuwanaye tangu zamani, tunamjua, anafanya kazi vizuri. Msaidizi wake Naibu, anafanya kazi, wamemtaja watu wengi sana. Mimi sikumjua huyu mama, kumbe kuna watu wengine humu ndani wamejificha ni wazuri sana. Mama ni mzuri kupita kiasi, anapokea simu usiku na mchana, anamsaidia sana Waziri kwa kweli, anafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katibu Mkuu, anafanya kazi vizuri, Mganga Mkuu wa Wizara anafanya kazi vizuri, na watendaji wote wa Wizara tunawapongeza. Tunawapongeza watendaji wote na waganga wote wa Benyamini Mkapa, wanafanya kazi vizuri sana, kwa sababu wao ndio wanaotupokea hapa na wanatutibu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwenye hoja. Huwa ninajiuliza mambo mengi kwamba, tuna bei elekezi ya pamba,

tuna bei elekezi ya mafuta. Ni nini hakitokei tukawa na bei elekezi ya dawa? Sielewi hapa. Yaani hapo sielewi. Kwa sababu leo *Asprin* sijui *Panadol,* huyu anauza mia tano, huyu mia mbili. Kuna gharama kubwa za dawa bila sababu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini hatutengenezi *project*; au hata kitengo cha kuangalia ubora wa dawa zetu, lakini kiweke bei elekezi? Tuna kosa gani kuweka bei elekezi ya dawa? Kwa sababu sasa watu wengine wanauza dawa wanavyotaka. Leo ukienda kwenye duka, kuna maduka wanakwambia tunakuuzia dozi, kuna mwingine anakwambia tunakupa kidonge kimoja. Yaani vidonge navyo vinauzwa kama pipi. Kwa nini hatutengenezi mfumo ambao watu wetu wanaweza kutibiwa vizuri? Kwa hiyo, ninafikiri kwamba hili nalo walichukue wakaliweke vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, suala la ujenzi wa Muhimbili mimi hata ningeambiwa usiku wa leo, kwamba jamani eeh hela imepatikana ya kujenga Muhimbili nipo tayari ku-*support* kwa asilimia mia moja. Wakati fulani huwa tunawaza sana juu ya ujenzi wa hela. Wanasema vitu vitamu na vitu vizuri vinaenda na noti. Leo nenda India Apollo zipo mia ngapi? Niliuliza juzi India, moja inajengwa pale Apollo, dola sijui milioni ngapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda kwenye nchi za watu tunarudi hapa, nchi fulani imeendelea, nchi fulani imeendelea, Tanzania hatuendelei. Tukitaka kujenga, ooh bei kubwa, bei ndogo. Hakuna hiyo, ajenge; tumekubaliana ajenge. Wala mimi siulizi gharama, ajenge, tunaitaka Muhimbili. Tena hiyo Muhimbilii iandikwe Samia Muhimbili mpya, kwa sababu ndiyo Zawadi ambayo mama ndiyo atakuwa ametuachia. Zawadi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo unasema maneno hapa, kesho ukiwa Muhimbili, wakikuhudumia utatoka unaangalia majengo, unapiga makofi kwamba, na mimi nilikuwa Mbunge, niliruhusu hapa. Kwa hiyo, tuombe, katika vitu ambavyo ni vya maana, tuweke hilo jengo ili lijengwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna uwezo wa Mheshimiwa Mchengerwa kukopa fedha tukajenga Muhimbili sasa, ajitahidi apate uwezo wa kukopa fedha kama zile zile, tujenge zahanati zote za vijiji, na tujenge vituo vya afya vyote vya kata. Aombe hizo fedha, tunazitaka kujenga Muhimbili. Tumekubali ajenge, lakini aende akaombe fedha nyingine, kama ni huko huko aombe. Tunataka sera ya Serikali itekelezeke, vijiji vyote viwe na zahanati na kata zote ziwe na vituo vya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Mchengerwa suala moja hapa lingine. Ninawashukuru sana, sana sana Wizara ya Afya, Hospitali yetu ya kongwe ilikuwa na shida kubwa ya *X-Ray*. Jengo tu la *X-Ray* lilikuwa limeshindikana, hata jana kabla sijaja hapa nimeuliza kule, wanasema mafundi wako pale wanatengeneza *X-Ray* kwa *speed* ya *4G*. Ninawashukuru sana kwa hilo, ninamshukuru mama kwa kutupatia hiyo *X-Ray* na kujenga jengo hilo kongwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine la kumalizia. Ninamwomba Mheshimiwa Mchengerwa, hizi habari za bei kuona mganga kijijini shilingi 5,000; kumwona mganga sijui mkoa shilingi 10,000; sijui kumwona nani elfu ngapi, kwa nini? Hivi kweli vijijini kuna waganga jamani? Yaani hata tukimwona *nurse* tu shilingi 5,000? Shilingi 5,000 kijijini unaitoa wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba hili suala la kumwona mganga liangaliwe mara mbili mbili. Kama mnahitaji waganga wa vijijini wapate hela, tuwawekee kwenye mishahara yao, tuwaache wananchi wapate msaada. Leo mtu anakwenda hana shilingi 5,000 anatoa wapi shilingi 5,000 ya kuweka hapo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukienda Benjamin Mkapa, juzi nimeuliza wanasema Jumatatu mpaka Ijumaa wanatoza shilingi 25,000 kumwona mgonjwa, Jumapili na Jumamosi shilingi 70,000; hospitali ile ile ya Serikali. Hapo hatutaki, twendeni kama ni shilingi 25,000 ya Muhimbili, iwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja, ahsanteni sana. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, ahsante kwa mchango wako. Sasa ninamwita Mheshimiwa Naomy Duncan Mwaipopo, ajiandae Mheshimiwa Santiel Eric Kirumba, atafuatiwa na Mheshimiwa Mary Daniel Surati.

**MHE. NAOMY D. MWAIPOPO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa pumzi, lakini kipekee ninashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia kwenye Wizara hii muhimu na nyeti kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze kwa pongezi kwa Wizara, kwa Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa wanayoifanya kuhakikisha miundombinu na pia madawa na vifaatiba vinapatikana kwenye hospitali zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa, ninaomba niishukuru Wizara pamoja na Rais kwa kuamua kujenga hospitali ya kanda katika Mkoa wa Kigoma. Kigoma ni mkoa wa pembezoni, lakini Kigoma ni mkoa wa kimkakati. Kwa nini ninashukuru?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kigoma tumepakana na Burundi na Congo. Hii hospitali ikikamilika tutakuwa na utalii tiba. Watu watatoka Congo kuja kujifunza, lakini watakuja kutibiwa kwenye hospitali hii ya kanda. Kwa hiyo, nishukuru na nipongeze kwa jitihada kubwa za Serikali ambazo zimeifanya hospitali hii kujengwa kwenye Mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ninashukuru kwa bajeti ambayo imetengwa ya shilingi 8,000,000,000 kwa ajili ya ukamilishaji wa hospitali hii. Ninaomba kwenye bajeti ya mwaka 2025 tumeona ilitengwa, lakini fedha hazikuja. Kwa hiyo, kipekee kabisa Mheshimiwa

Waziri tunaomba hii fedha ije ili tukamilishe ujenzi wa hospitali ile ya kanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa tu, Kigoma kunajengwa Chuo Huria cha Muhimbili. Kupitia hospitali hii, itakuwa rahisi kwa wanafunzi wa Chuo cha Muhimbili kwenda kufanya mafunzo kwa vitendo kwenye hospitali ya kanda pale Kigoma. Kwa hiyo, hii inaonesha ni namna gani hii fedha inahitajika ije haraka kukamilisha kuendana na kasi ya ujenzi wa chuo, lakini iende sambamba na ujenzi wa hospitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, sisi Wanakigoma, tunaomba hizi kasi za maendeleo ambazo Serikali imeamua kuzifanya kwenye mkoa wetu, tunashukuru, lakini tunaomba utekelezaji uwe kwa kasi kidogo. Ninaamini umenisikia na Mheshimiwa Waziri atalichukua; ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninaomba nizungumzie suala la ugonjwa wa ini. Kama nilivyosema, Kigoma tuko pembezoni. Ugonjwa wa ini Kigoma unamaliza ndugu zetu. Ugonjwa wa ini Kigoma unatafuna majirani na marafiki zetu. Ninaiomba Wizara, wakati Mheshimiwa Waziri anakuja ku-*wind up* atuambie amejipangaje kutoa elimu na kutokomeza ugonjwa huu kwenye Mkoa wa Kigoma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanakufa. Ninaiomba Wizara ije na mpango mkakati wa namna ya kuelewesha wanawake, lakini pia wananchi wa Mkoa wa Kigoma kujikinga, lakini pia kuwa makini na ngono zembe kwenye suala hili la ugonjwa wa homa ya ini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wengi hawana elimu, lakini Wizara ikichukua jitihada za makusudi kama zilivyochukuliwa kwenye VVU na UKIMWI, ninaamini kabisa elimu itafika kwa wahusika na watu watachukua tahadhari. Ninaiomba sana Wizara ije na mpango mkakati, tunatokaje kwenye suala hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, ninaomba kwenye suala la watu wa figo, gharama za kufanya *dialysis* kwenye huu

ugonjwa zimekuwa kubwa. Kwenye *Private Sector* huko watu wakienda watu wanakosa huduma kwa sababu ya kukosa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaiomba Wizara ije na namna nzuri ya kuwasaidia hawa watu kwa sababu mtu akishakuwa mgonjwa, hana uwezo wa kuingiza uchumi, hana uwezo wa kupata fedha kama alivyokuwa mzima. Kwa hiyo, Serikali ikiona namna ya kupunguza kidogo au kubeba hizi gharama itasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hayo, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ninakushukuru kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Santiel Eric Kirumba, ajiandae Mheshimiwa Mary Daniel Surati.

**MHE. SANTIEL E. KIRUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ningependa kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mambo makubwa aliyofanya katika Mkoa wa Shinyanga. Ameweza kutujengea hospitali kubwa kuanzia mkoa hadi kwenye ngazi ya wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tunavyoongea kwa sasa hivi Mheshimiwa Rais ameweza kuidhinisha fedha za kujenga maabara kubwa ya kisasa katika hospitali yetu ya rufaa pamoja na wodi ya mama na mtoto. Hiyo ni hatua kubwa sana sana kwa Mkoa wetu wa Shinyanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ninapenda kuendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya. Hili jambo alilokuja nalo la Bima ya Afya kwa Wote, sisi kama Wabunge nina imani tunaenda kushikamana kwa pamoja kuitangaza bima hii ya afya. Tutahakikisha wananchi wanajiunga kwa wingi, maana kwa hali ya kawaida mgonjwa anapoenda hospitali kupata huduma ya *cash,* ni gharama kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alisema hapa Bungeni, nitakapomaliza kipindi change, ninatamani kumwona kila mwananchi akiwa na tabasamu kwenye uso wake. Hili linaenda kumfanya mwananchi anakuwa na tabasamu kwenye uso wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wake pamoja na Mganga wetu Mkuu. Jamani mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni. Ni wachapa kazi na wamekuwa rahisi kufikika. Licha ya uchapakazi wao, sisi Mkoa wa Shinyanga bado tuna changamoto katika magonjwa yasiyoambukiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza kuongelea ugonjwa wa figo, ugonjwa huu umekuwa ni tatizo, lakini kwa Mkoa wetu wa Shinyanga hatuna mashine za *dialysis*. Ninakupa mfano, mtu ambaye anatoka Jimbo la Ushetu, Ubagwe atalazimika kutembea kilomita 300 mpaka 400 kwenda kuifuata huduma hii ya figo ya kusafishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii kupelekea baadhi ya watu ambao wanauguza watu hawa kwenda kufilisika kiuchumi kwa sababu ukiangalia huduma hii kwa wiki, anafanya mara tatu, na kwa Mkoa wa Shinyanga hakuna. Hawezi kwenda akatembea kilomita 300, 400 kuifuata huduma hii Mwanza na baada ya siku mbili, tena atarudi na mkoa wetu hauna huduma hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya Chama cha Mapinduzi ilielekeza vyema kwamba, itahakikisha inashusha huduma ya afya katika kila mkoa, huduma bora. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri, mtu anayeumwa figo huyo huyo anaweza akaumwa kisukari, huyo huyo anaweza akaumwa *pressure*. Pia, magonjwa haya yote yanaambatana kwa pamoja, na sasa hivi, hili limeshakuwa ni janga, watu wanaumwa magonjwa yasiyoambukiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Wizara inatakiwa kwa sasa hivi ipambane kutoa matamko kuelimisha watu namna bora ya

kuweza kujikinga na magonjwa haya. Maana *lifestyle* ya maisha inatupelekea kwenda kupata magonjwa haya yasiyoambukiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hata watoto wadogo sasa hivi wamekuwa wakipata magonjwa haya yasiyoambukiza. Kama iliwezekana katika Virusi vya UKIMWI kufanya matangazo mara kwa mara, hata haya magonjwa yasiyoambukizwa ni wakati sasa hivi kuweza kuweka matangazo ya kutosha na elimu ya kutosha, kwa sababu hata mfuko huu wa bima ya afya tutakapokuwa nao pia utatulazimu kutumia gharama nyingi sana kwa hawa watu ambao watakuwa wanaumwa magonjwa haya ya figo na *cancer*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Waziri na ninategemea kwa sababu tuna zahanati zetu hata za kata huwezi ukakuta hili tangazo la jinsi ambavyo unaweza ukajilinda, ukajikinga usipate magonjwa haya yasiyoambukiza. Ninajua nia ya dhati ya Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Rais kuhakikisha tunajenga Muhimbili mpya ya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapojenga Muhimbili mpya ya kisasa bado tutahitajika tuwekeze pia katika hospitali za rufaa, hospitali za kikanda ili kuipunguzia mzigo Muhimbili. Pia, kituo cha *dialysis* kwa Mkoa wa Shinyanga ni milioni 300 tu. Ninaomba tuidhinishiwe hizi fedha, kwa sababu takribani kwa mwaka wagonjwa 300 wanasafiri kwenda kupata huduma hii kwenye mikoa ya jirani. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ninakushukuru kwa mchango wako. Sasa ninamwita Mheshimiwa Mary Daniel Surati, ajiandae Mheshimiwa Cornel Lucas Magembe.

**MHE. MARY D. SURATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa fursa hii. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na kaka yangu Mheshimiwa Mchengerwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitakuwa mchoyo wa fadhila kama pia sitampongeza Naibu Waziri wetu na wafanyakazi wote wa Wizara

hii ya Afya. Kiukweli wanafanya kazi nzuri na sisi tunayaona hayo wanayoyafanya. Pia ninaendelea kupongeza zaidi mageuzi makubwa katika hii Wizara ya Afya ambayo yanakwenda kutokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nimesimama, kwanza kabisa ninaunga mkono hoja, hicho ndicho cha kwanza. Ninalo jambo langu ambalo ninalichukulia kwa ubinafsi na linaniumiza sana kwamba, Serengeti nimepokea jumla ya watumishi 25, ninashukuru sana kwa hilo, lakini mpaka ninavyosimama hapa mbele yako jumla ya watumishi 21 wamehama bila kubadilishana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo ikumbukwe Serengeti kama jimbo linahudumia wananchi, lakini pia nina watalii. Sambamba na hayo, Mheshimiwa Rais alivyoandaa Filamu ya *The Royal Tour,* ameweza kutambulisha utalii na kuweza kuongeza idadi ya wakazi na watu ambao wanazidi kufika Serengeti. Sasa angalia hali ya afya ambayo mimi kama Mbunge wa Jimbo la Serengeti na wananchi wa Serengeti tunapata wakati mgumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba jambo moja, kwamba wakati wanapangwa watumishi wapya, basi sisi tunaopatikana pembezoni tuongezewe idadi, kama unanipatia watumishi 25, au 21 wanaondoka, haya ni mambo ambayo kiukweli yanahuzunisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, mimi pia niungane na Mheshimiwa Ghati Chomete, dada yangu kuhusiana na suala la Hospitali inayobeba hadhi na jina ya Baba yetu wa Taifa. Tunaomba sana, hospitali hiyo iangaliwe kwa upekee mkubwa sana, kwa sababu ukiangalia, sambamba na kwamba Serengeti tunapokea watalii, Hospitali ile ingekuwa imeimarishwa, baadhi ya watalii wangekuwa hawaendi kutibiwa nje ya nchi, wangekuwa wanaishia hapa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizingatia tayari Mheshimiwa Rais amekuja na maono ya kutengeneza uwanja wa Kimataifa wa Serengeti ambao pia unakwenda kuongeza idadi ya watalii, kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri kaka yangu mtu kazi tafadhali

azingatie sana jambo hili na atusaidie watu wa Serengeti na Tanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa leo sina mengi ya kusema, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, na hongera kwa mageuzi makubwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante kwa mchango wako. Sasa ninamwita Mheshimiwa Cornel Lucas Magembe, ajiandae Mheshimiwa Grace Elias Mkoma.

**MHE. CORNEL L. MAGEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi pia ninaomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hotuba hii ya Wizara ya Afya. Kwanza nianze kwa kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa upendo wake mkubwa kwa Watanzania kwa kuendelea kusimamia afya za Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Mkoa wa Geita na Wilaya ya Chato alitupatia heshima kubwa katika kipindi chake hiki cha kukamilisha ujenzi wa Hospitali kubwa ya Rufaa pale Chato. Tunamshukuru sana wananchi wa Chato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninaomba nitumie nafasi hii kumpongeza kwa kazi nzuri Mheshimiwa Waziri wa Afya pamoja na Naibu Waziri na watumishi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoendelea kuitekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Rais anaomba kura alipokuwa anapita kwetu kule alikuwa anasema katika siku 100 anakwenda kutoa Bima ya Afya kwa Wote kwa kuanzia makundi maalum. Sasa nilipokuwa nasikiliza hotuba zake nikaanza kujiuliza kwamba ni kweli anakwenda kufanya! Ni nani anakwenda kupewa Wizara ile kwenda kusimamia? Bahati nzuri alipokuwa anataja Baraza la Mawaziri, alipomtaja Mheshimiwa Mchengerwa kwamba ndio anakwenda kuwa Waziri wa Wizara hiyo, nikasema hapa ameweza, ameshika penyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamfahamu Waziri kwa sababu kwenye mambo ya msingi huwa anasimama. Ndiyo maana katika siku 100 haya mambo yamekwenda kutekelezwa. Akiwa TAMISEMI pale na mimi nikiwa *DC* kwa kweli tulinyooka, tukaenda tukafanya kazi vizuri na ninajua hata alipopelekwa kwenye afya watu wa afya watanyooka. Hongera sana Mheshimiwa Waziri, endelea kupiga kazi na mambo yatakwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizi, tumeona kwenye bajeti ya Wizara ya Afya, Wizara imeomba fedha za maendeleo, na moja ya fedha ambazo zimeombwa ni pamoja na ujenzi na upanuzi wa hospitali yetu kubwa ya Muhimbili. Niungane na wenzangu wengine ambao wamesema kwa kweli ninaunga mkono jambo hili kwa asilimia mia moja kwa sababu linakwenda kurejesha afya zetu sisi hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, Wizara pamoja na kwenda kuendeleza hospitali yetu kubwa ya Muhimbili, mimi nilikuwa na ushauri ufuatao: Jambo la kwanza ni kutekeleza ile sera ambayo imewekwa na nchi yetu ya kuhakikisha tumepata zahanati kwa kila kijiji, na kuhakikisha tunapata vituo vya afya kwa kila kata na hospitali za wilaya kwa kila wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tukienda kwenye Halmashauri yangu ya Chato na Wilaya ya Chato, tuna kata 23 kwenye Wilaya nzima ya Chato. Vituo vya afya ambavyo viko, vinafanya kazi mpaka sasa hivi vilivyokamilika viko vituo vya afya vitano tu katika kata 23. Sasa ukiona tofauti ya kata 23 kuwa na vituo vya afya vitano vinavyofanya kazi vizuri, maana yake hii ni hatari kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokifahamu, wananchi walio wengi 74% mpaka 80% wanakaa kule kwenye vijiji na kwenye kata. Sasa tukishindwa kuboresha vituo vyetu vya afya ambavyo ndiyo vinakwenda kusaidia watu wengi wanaoishi huko kwenye kata na kwenye vijiji, ninadhani tunakuwa tunafanya kazi ambayo siyo sahihi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri na Wizara ijikite kwenda kuhakikisha inakamilisha vituo vya afya kwenye kata zetu. Kwa mfano, mimi nina vituo vya afya vinne kwenye jimbo langu lenye kata 14, ambavyo vituo hivi vya afya vilianzishwa, lakini mpaka sasa hivi havijakamilika na kuanza kutoa huduma kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunacho Kituo cha Afya cha Katende ambacho hakitoi huduma yoyote kwa sababu miundombinu na vifaatiba havijakamilika. Tuna Kituo cha Afya cha Nyabilezi - Bukome nacho kimeanza kufanya kazi, lakini siyo kwa weledi ule ambao unatakiwa. Tuna Kituo cha Afya cha Ilemela, Kituo cha Afya cha Bwina, Kituo cha Afya cha Butarama Kata ya Kigongo, vyote vile vilianzishwa, lakini miundombinu yake haijakamilika na vifaa tiba havijafika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Waziri kwenye mpango wake wa maendeleo wa kupeleka fedha kwenye ukamilishaji wa vituo vya afya, vituo vyangu vya Butarama, Bwina, Ilemela pamoja na Katende vizingatiwe na kingine cha Ilyamchele ambavyo vyote havijapata fedha ya kuweza kwenda kukamilika ili wananchi wa maeneo yale waweze kuwa wanapata huduma zinazostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kwamba Wizara hii ndiyo inasimamia sera, lakini iko Wizara ya TAMISEMI ambayo yenyewe inakwenda kutekeleza. Pia kuna ushirikiano mkubwa kati ya Wizara ya Afya pamoja na TAMISEMI, na fedha nyingine nyingi zinapitia kwenye Wizara ya Afya. Zitoke fedha kutoka Wizara ya Afya zipelekwe kwenye TAMISEMI ili vituo hivi viende kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Grace Elias Mkoma, ajiandae Mheshimiwa Kassim Hassan Haji.

**MHE. GRACE E. MKOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami nichangie katika Bajeti hii ya Wizara ya Afya. Kwanza, ninaomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema nami kusimama mahali hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninaomba nichukue nafasi hii kumshukuru au kuwapongeza Waziri wa Wizara ya Afya, lakini Naibu Waziri wa Wizara ya Afya na Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya kwa kazi nyingi ambazo wanazifanya katika Wizara hii na tuliona mchango wao mkubwa sana katika Wizara hii wanaoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichukue nafasi hii pia kumpongeza Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, hasa kwa fedha nyingi ambazo amezileta katika Mkoa wetu wa Singida, takribani shilingi bilioni 5,140, ili kutekeleza miradi ya Wizara ya Afya katika Mkoa wetu wa Singida. Fedha hizo zimetumika kuboresha miundobinu katika Mkoa wetu wa Singida; kujenga zahanati katika Mkoa wetu wa Singida, ambapo zahanati hizo zilikuwa hazijakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichukue nafasi hii kupongeza sana watumishi wetu wa Mkoa wa Singida ambao baada ya fedha hizi kuletwa, wao walizisimamia na kuhakikisha zahanati na vituo vya afya vikakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na fedha hizo kuletwa katika Mkoa wetu wa Singida, lakini bado tuna changamoto nyingi sana. Katika Mkoa wetu bado tuna changamoto za watumishi, takribani 58%. Watumishi hao ni madaktari wa usingizi, waganga na manesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna siku nilitembelea zahanati mojawapo katika Mkoa wetu wa Singida, zahanati hiyo ya Bomani, nilikutana na nesi mmoja, anatoa chanjo, lakini pia anawasaidia wanawake wajawazito hasa pale ambapo wanapata uchungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wetu wa Singida changamoto ya watumishi ni kubwa sana. Ninaomba Serikali, kupitia Waziri wetu wa Wizara ya Afya, alichukue hili na akajaribu kuitatua changamoto hii hasa kwa Mkoa wetu wa Singida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mkoa wetu wa Singida bado kuna ukosefu wa magari ya kusambazia chanjo. Mfano, katika Wilaya ya Ikungi bado kuna changamoto kubwa sana, Wilaya hiyo haina kabisa gari la kusambazia chanjo. Pia, Mkalama nako kuna changamoto kubwa sana, hakuna gari kabisa la kusambazia chanjo. Nina imani kubwa sana na Waziri wetu wa Wizara ya Afya, ninaomba alione hili, ili sasa hawa wananchi na wenyewe wakapate gari la kusambazia chanjo, katika Mkoa wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mkoa wetu wa Singida bado kuna changamoto kubwa sana, na changamoto hiyo bado kuna kata takribani 78, hazijapata vituo vya afya. Ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri wetu wa Wizara hii ya Afya, alichukue hili na alione kwa uzito sana. Ukiangalia Mkoa wetu wa Singida na wilaya zake zote, uko *scattered* sana. Wananchi wa Mkoa wa Singida wanaishi *scattered* sana, na wanapata changamoto kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Waziri alichukue hili na aliangalie kwa uzito, sasa na wananchi wa Mkoa wa Singida wakajengewe hospitali ili tuweze kutatua changamoto ya watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapongeza sana Wizara hii kwa kazi nyingi inayoendelea kufanya, lakini kuna ujenzi wa Hospitali ya Muhimbili. Ninaunga mkono hoja kwa huu ujenzi mkubwa wa Hospitali ya Muhimbili, kwa sababu Hospitali hii ya Muhimbili inaenda kulitangaza Taifa la Tanzania kwa upya. Pia inaenda kutatua changamoto nyingi ambayo sasa wananchi wengi walikuwa wanatoka kwenye mikoa yetu ya Tanzania, wanaenda kulundikana katika Hospitali ya Muhimbili. Mlundikano unakuwa ni mkubwa, lakini

hospitali hii ikienda kujengwa wananchi wengi wataenda kufaidika na hii hospitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana, nami ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Sasa ninamwita Mheshimiwa Kassim Hassan Haji, ajiandae Mheshimiwa Lucy Edward Mwakyembe.

**MHE. KASSIM HASSAN HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Nami nianze kwa kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa maono yake. Nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa ya utekelezaji wa maono ya Mheshimiwa Rais, ambayo mimi ninasema sasa hivi washafikia 100%, kwa kwenda kuijenga ile Muhimbili mpya. Tayari 100% zimekamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze tu kwa kuipongeza Serikali, ilikuwa ina dhamira nzuri, njema, yenye tija katika Taifa letu ya kuondoa chakula kukipeleka *TBS*. Bado tunaona kuna shida nyingine ambayo sasa hivi imejitokeza. Watu ambao wanafanya biashara ya chakula, udhibiti wao umekuwa mdogo, yaani udhibiti wao umekuwa hafifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana, na tunaiomba Serikali, hii dhamana ya kudhibiti chakula irudi tena kwa *TMDA*. Taasisi hii ilipata ithibati kubwa sana, na uaminifu duniani kote, kwa sababu tu ya udhibiti mzuri ambao tulikuwa tunaenda nao Tanzania. Sasa hivi tunaomba tena warejeshewe majukumu haya, waendelee nayo wao, ili tuendelee kuwa na hadhi ile ile kama dunia ilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi zote zina *FDA,* kwa maana ya kwamba, wao ndio wadhibiti wa chakula na dawa. Naomba sana Serikali yetu sikivu hii, irejeshe mambo haya katika *TMDA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa biashara ya *supplement* imehamia kwenye mitandao. Ukifungua mtandao wa Mheshimiwa Waziri hapo, dawa zote, *supplement* zote zinauzwa kwenye mitandao. Mbali ya hilo, tayari wale ambao wanauza, wao wanajiita madaktari. Dozi zinatolewa kwenye mitandao, *supplement* hizo zinauzwa kwenye mitandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna vijana wazuri tu sasa hivi, sasa hawa wanaouza hizi *supplement* kwenye mitandao, na wao waweze kwenda kuchangia huu Mfuko wa Bima ya Afya. Tuna vijana wazuri ambao wametengeneza njia nzuri za makusanyo, basi nao walisaidie Taifa hili katika kupeleka fedha hizo, makusanyo hayo kusaidia wenzetu ambao watakuwa wanaenda katika kuisaidia Bima ya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee na jambo lingine. Tuna hospitali nyingi sana ambazo tayari tumeshatengeneza, bado tunahitaji marekebisho na vifaa. Katika bajeti hii, ninamwomba sana Waziri aende akasaidie hospitali hizi. Wenzetu Wabunge hapa wamesimama wakasema, wakatoa na mifano katika maeneo yao. Bajeti hii iende ikatatue changamoto hizo, tukiamini kwamba Waziri ni mtu kazi, atakwenda kuboresha hospitali hizi, walau zifikie malengo ambayo Wabunge hawa na wananchi wale wanatarajia kufikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimalizie suala langu dogo tu kuhusu *DMO,* na *RMO*, wengi wao ni wanaume. Mheshimiwa Waziri, akikaa na Wizara ya TAMISEMI, waende wakaongeze idadi ya wanawake kuwa ma-*DMO na* ma-*RMO.* Tunataka kuondoa vifo vya mama wajawazito na watoto. Tukiwawekea hawa ma-*RMO* na ma-*DMO* ambao watakwenda kuongeza nguvu katika kinga ya mama na mtoto, basi tutakwenda kufikia malengo kabisa ya kuondoa vifo kabisa, kuwe hakuna. Tukatimize hili, idadi yao tumeitazama, ni ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hospitali hizo hizo, tuna hospitali ambazo Mheshimiwa Waziri amesema makusanyo yao yako chini.

Tuna hawa ma-*DMO*, ma-*RMO* ambao wamekaa katika wilaya katika mikoa, kwa kipindi kikubwa. Tayari chochoro zote za wizi, chochoro zote za kuingiza vitu ambavyo havihitajiki, wameshazizoea. Waende wakafanye mabadiliko, watu ambao tayari wamekaa kwa miaka miwili, miaka mitano, miaka 10 katika maeneo hayo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Mheshimiwa Waziri amezunguka katika Wizara nyingi, ndani ya miaka mitano, siyo chini ya Wizara tatu. Basi nao wafanyiwe mabadiliko, kuona angalau tunaenda kuleta tija, lakini angalau tunaweza kwenda kukusanya maduhuli ambayo yatakuwa yanasaidia Wizara katika makusanyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, ninaiomba sana Serikali, tuna ujenzi mkubwa ambao unakwenda kuijenga Muhimbili mpya. Muhimbili mpya ndiyo taswira ya afya katika Taifa letu. Wizara iongeze nguvu, Waziri amesema baada ya miaka mitano, kama kuna uwezekano, Mheshimiwa Rais amesema anataka kuacha furaha kwa Watanzania hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kama kuna uwezekano, ishuke chini baada ya miaka mitano hata iwe miaka mitatu. Mheshimiwa Rais na yeye atimize majukumu haya, aone furaha hii akiwa bado yupo katika madaraka yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nami ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango wako. Waheshimiwa Wabunge, ninaomba niwatambulishe wageni walioko Bungeni mchana wa leo.

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, Waziri wa Afya, ambaye ni Sheikh Abid Mahmood Bhatti, ambaye ni Naibu Amir Taasisi ya Ahmadiyya Muslim Jama'at. *(Makofi)*

Tunao wageni wa Mheshimiwa Mchengerwa, ambao ni wawekezaji wakubwa katika Kongani ya Viwanda jijini Dar es Salaam,

ambao ni Ndugu Miayo Yingyang, Mwekezaji wa Vifaa Tiba na Dawa; Ndugu Lyu Yinghua, Mtafsiri wa Lugha; Ndugu Su Zhou, Mkurugenzi wa Ndani; na Ndugu Victor Tesha, Mtaalam Mshauri wa Mradi. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine wa Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, ambao ni viongozi wa vyama vya kitaaluma; Chama cha Madaktari Tanzania, Chama cha Madaktari Bingwa wa Magonjwa ya Akina Mama na Uzazi, Chama cha Makatibu wa Afya, Chama cha Wafamasia Tanzania, Chama cha Wataalamu wa Maabara Tanzania, Chama cha Wataalamu wa Meno Tanzania, Chama cha Wataalamu wa Mionzi Tanzania, Chama cha Wauguzi Tanzania, Chama cha Huduma za Afya. *(Makofi)*

Tunao wageni 18 wa Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, ambao ni Kwaya ya Utatu Mtakatifu kutoka kanisa la Anglikan Msalato Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, ambao ni wanafunzi 150 na walimu 10 wa Shule ya Msingi Chang'ombe kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Omary Mchengerwa, ni Waziri wetu wa Afya, ambaye ni Dkt. Seif Suleiman Rashid, Mbunge Mstaafu wa Rufiji na Waziri Mstaafu wa Afya. Karibuni wageni wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa tunaendelea. Nilimtaja Mheshimiwa Lucy Edward Mwakyembe, ajiandae Mheshimiwa Janeth Peter Pinda.

**MHE. LUCY EDWARD MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Muhimbili ni kioo cha Tanzania kwenye matibabu. Kwa hiyo, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa dhamira ya makusudi kuijenga Muhimbili mpya. Ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, pamoja na Naibu Waziri wake, na madaktari, wauguzi, watendaji wote wa Wizara ya Afya kwa kazi nzuri wanayoifanya ambayo kila mmoja wetu anaiona, kuhakikisha afya za Watanzania zinakuwa bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Mchengerwa kwa usimamizi mzuri wa huduma za afya, ambazo zinaendelea kupatikana ndani ya nchi, katika kutoa huduma hizi kupitia madaktari bingwa na wabobezi, ambao wanatoa huduma za afya ndani na nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanikiwa kuongeza vituo vya kutolea huduma za afya, kutoka vituo 10,153 mwaka 2021/2022 mpaka kufikia vituo 13,683 mwezi Machi, 2026. Ni hatua kubwa kwa Serikali, tunaomba kuwapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuhakikisha anaimarisha Bima ya Afya, na Serikali imetoa shilingi bilioni 48.8 kwa kuhakikisha wananchi wote wanapata Bima ya Afya, na tayari kaya zaidi ya 200,000, zimeweza kufikiwa katika kupewa Bima ya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijielekeze zaidi katika huduma ya afya, kwa madaktari bingwa na madaktari bingwa mabobezi, hasa katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete *(JKCI)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande huu ninaomba nichangie katika utoaji huduma. Tumeiona *JKCI* inavyopeleka huduma katika mikoa mingi Tanzania. Wanatoa huduma za kliniki ambazo zinawasaidia wananchi wa Tanzania katika kutatua changamoto za magonjwa wa moyo zinazowakumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa, nami ninaomba *JKCI* kupitia Serikali yetu ya Tanzania na msimamizi wake mkuu Mheshimiwa Mchengerwa, kwenye upande wa afya, iwe na dhamira ya makusudi ya kupeleka huduma za afya kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kuanzisha Kituo cha Moyo katika Serikali ya Zanzibar. Huduma hii, ninaamini itakwenda kwa ushirikiano wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii nimeiomba kwa sababu itawarahisishia wananchi, kuwauguza wagonjwa. Wanaposafiri kufika

Muhimbili kwenye kituo cha *JKCI,* itawapunguzia gharama, pia kituo hiki kitakapokuwa kimeanzishwa Zanzibar. Kwa hiyo, ninaomba hili lichukuliwe, kwa ajili ya kuanzisha *branch* kule Zanzibar cha *JKCI*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua suala hili Wizara ya Afya iko Bara, lakini ninaomba ishirikiane na *SMZ*, yaani zinatofautiana kati ya Bara na Zanzibar. Ninaomba zishirikiane na *SMZ* kuanzisha kituo cha afya kwa ajili ya magonjwa ya moyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia Serikali yangu sikivu na ninaamini itashughulikia suala hili kwenye upande wa magonjwa ya saratani. Magonjwa ya saratani yana maumivu makubwa na ni makali sana, yanawaumiza sana Watanzania, lakini gharama zake nazo ni kubwa. Mgonjwa anapofika hatua ya kuanzishwa *chemotherapy*, gharama ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaiomba sana Serikali yangu sikivu ipunguze gharama za matibabu haya ya saratani kwa sababu maumivu ya saratani ni makali, lakini gharama nazo zikiwa kubwa mgonjwa anazidi kupata maumivu makali. Ninaiomba Serikali iliangalie suala hili ili kupunguza gharama hizo kwenye upande wa saratani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, ninaendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa ajili ya kupunguza vifo vya uzazi kutoka vifo 556 kwa vizazi hai 100,000 kufikia 106 mpaka ikamfikia kupata tuzo ya Rais bora katika utoaji wa huduma za afya ya akina mama na watoto kwa kupunguza za vifo barani Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Janeth Peter Pinda, ajiandae Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta.

**MHE. JANETH P. PINDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kuchangia katika hotuba ya bajeti ya Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninaomba nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Waziri wa Afya, Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara, pia watendaji wote wa Wizara ya Afya kwa namna ambavyo wamekuwa wakifanya kazi za afya na katika kuboresha shughuli zote za afya na kuwafanya Watanzania waendelee kupata huduma bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi sana ninapenda kuchukua nafasi hii kumshukuru sana mama yangu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo amekuwa kinara katika kuwafanya akina mama wajawazito pamoja na watoto kuendelea kupata afya bora. Hili kwa kweli sisi tutakuwa ni wachoyo wa fadhila tusipomshukuru sana mama yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, sasa niende moja kwa moja kwenye Mkoa wangu wa Katavi. Ninaomba nishukuru sana katika kipindi hiki tumepokea shilingi bilioni 2.3. Yote hii ni kwa ajili ya kuviwezesha vituo vya kutolea huduma kuweza kutoa huduma za dharura pamoja na upasuaji na kwa ajili ya akina mama wajawazito na watoto wachanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa niende moja kwa moja kwenye suala la ujenzi wa viwanda. Ninaenda kwenye ujenzi wa viwanda kwa sababu tumejengewa vituo vingi sana vya afya, tumejengewa hospitali, sasa kazi itakuja kwenye uhaba wa dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumbe tukijengewa hiki kiwanda cha dawa kitaweza kutuondolea sisi adha ya uhaba wa dawa. Kwa sababu gani? Tunakwenda kwenye Bima ya Afya kwa Wote. Tunapoenda kwenye Bima ya Afya kwa Wote, watu wengi watakwenda kuwa na bima, na wengi watahitaji dawa, na wengi zaidi ni wale ambao wanaweza wakawa na magonjwa yale yasiyoambukiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kukiwa kuna changamoto ya dawa, itakuwa ni shida katika hivi vituo ambavyo tumeweka, watu watakaokwenda kupata huduma watakosa huduma hizi. Kwa hiyo, ninaomba sana katika suala la viwanda tulipe kipaumbele katika bajeti hii ambayo tunakwenda kuitekeleza kwa mwaka wa fedha huu unaokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la Bima ya Afya kwa Wote. Ninawapongeza sana Wizara kwa namna ambavyo wamelichukua na kulipa kipaumbele kama vile Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan alivyoahidi katika siku zake 100 za utendaji wake wa kazi, aweze kutekeleza Bima ya Afya kwa Wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili tumeona limetekelezeka kwa wale watu ambao ni wa kima cha chini au watu wasiokuwa na uwezo. Kwa kweli niwapongeze sana watu wa bima ya afya ambao wamelitekeleza hadi kufikia leo ni kwa 62% ya malengo ambayo yalikuwa yamewekwa katika usajili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba sana Wizara katika mwaka wa fedha unaokuja tuone namna tutaweza kufikia na watu wengine ili waweze na wenyewe kupata bima ya afya. Kikubwa tuendelee kutoa elimu ili kuwafikia wananchi wengi waweze kuelewa bima ya afya ni kitu gani, ili tutakapokuja kwenda katika makundi mengine kusiwe na shida kwa sababu watu wengi watakuwa tayari wameshaelewa hiyo bima ya afya ni kitu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika yote haya, ninaomba sana katika Dira ya 2050 inasisitiza Taifa la watu au wananchi wenye afya njema. Wananchi wakiwa na afya njema, wataweza kuwa wabunifu, lakini watazalisha zaidi na kufanya ushiriki wa Watanzania kwenye shughuli za maendeleo waweze kujiamini kwa sababu watakuwa na afya njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji katika sekta ya afya siyo tu uwekezaji wa kawaida, ni uwekezaji wa kimkakati ambao utaweza kusaidia Watanzania kuwa na afya bora. Ninamwomba Mheshimiwa

Waziri katika utekelezaji wa bajeti hii, ni muhimu kufungamanisha maono ya Dira ya Taifa pamoja na maono ya Mheshimiwa Rais, kwa sababu hayo yote yeye anachokitaka ni Watanzania kuwa na afya bora. Kwa hiyo, tukizifungamanisha tutaweza kutekeleza Dira 2050 ili wananchi waweze kuwa na afya bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inapaswa kuwa chombo kikuu cha utekelezaji wa Dira ya Taifa kwa maana ya kwamba kwa kuendelea kuimarisha huduma za afya ya msingi za vijijini na mijini na pia kuwekeza katika afya ya mama na mtoto hasa mama mjamzito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mkoa wangu wa Katavi, ninashukuru kumekuwa na ule utaratibu wa Thamini Uhai wa Mjamzito na Mtoto. Kwa kweli tunatekeleza katika wilaya zile zote tano na tunayaona mafanikio makubwa sana, akina mama wananufaika sana na huu mradi. Ninaomba hata katika vile vituo vya afya tuweze pia na vyenyewe kuweka utaratibu wa kuweza kwenda kuitekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sitakuwa na mambo mengi, zaidi sana niende kwenye ujenzi wa Hospitali ya Taifa Muhimbili. Ninaweza nikaungana na wenzangu kuona kwamba hii hospitali ni muhimu tukaijenga kwa sababu tumejengewa hospitali mikoani, lakini tumepata vituo vya afya. Ikijengwa hii itaboresha zaidi huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilimtaja Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta na mchangiaji wetu wa mwisho mchana wa leo atakuwa Mheshimiwa Clayton Revocatus Chipando.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu na wananchi wa Urambo kwa jinsi wanavyonipa ushirikiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba yao ninaomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa jinsi ambavyo ametutendea haki kwa upande wa huduma za afya. Ametujengea vituo vya afya na zahanati. Sina mengi ya kusema, zaidi ya kusema Mheshimiwa Rais ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee pia nimshukuru sana Mheshimiwa Mchengerwa, Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara ya Afya kwa kazi kubwa wanayofanya. Kwa kweli Mwenyezi Mungu awabariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa huduma nyingi alizotupa Urambo, tunaomba *ambulance,* kwa sababu sasa kukimbiza wagonjwa Kitete Hospitali ya Mkoa na kwingineko, kwa kweli ni shida. Tunaomba sana *ambulance*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kwa upande wa Mkoa wa Tabora, Mkoa wa Tabora tuna Hospitali ya Mkoa inayojulikana kwa jina la Kitete, lakini kwa upande wa maradhi yasiyoambukizwa, tuna shida sana ya kupata huduma. Malaria na mengine yote, sawa, lakini yasiyoambukizwa ni shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika huduma kubwa ambazo tunazitegemea, 17 katika hospitali ya mkoa sisi tunazo sita tu. Kwa hiyo sasa hivi hata tukipiga simu, utakuta wagonjwa wetu wengi wapo hapa; wapo Benjamin Mkapa, wapo Bugando, wapo Nkinga, kwa sababu huduma za kibingwa kwa kweli zinazotolewa Kitete ni sita tu kati ya 17. Kwa heshima ninamwomba Waziri ambaye ninamjua ni mchapakazi, nimefanya naye kazi sana, atusaidie huduma za kibingwa ziongezwe Hospitali ya Kitete. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo nimshukuru kwamba katika hiyo Hospitali ya Kitete wanajenga wodi ya watoto hasa *ICU* na imeendelea vizuri isipokuwa kwa upande wa wodi ya akina mama, (ya wazazi) haiendelei sana. Kwa hiyo, tunaomba tusaidiwe, inasuasua sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa upande wa Mkoa wa Tabora, tuna shida kubwa sana na hospitali ya kanda. Kwa muda mrefu Serikali ilitupa matumaini kwamba Mkoa wa Tabora utakuwa na hospitali ya kanda mpaka tukatafuta eneo kubwa Buigiri mpaka sasa hivi bado tunaota. Je, Serikali bado inatufikiria? Tunaiomba Serikali isitusahau, ndoto ambayo tumekuwa nayo kwa muda mrefu Mkoa wa Tabora kuwa na hospitali ya kanda iendelezwe kwa sababu ni matumaini yetu kwamba ikiwa hospitali ya kanda huduma itakuwa kubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tunaomba hiyo hospitali isibadilishwe kwa kuwa wazo lilikuwapo la kupeleka Buigiri hospitali ya kanda iendelee. Pia, tuliahidiwa kwamba kutakuwa na Hospitali ya Utengamao ambayo itajengwa Nzega na tayari wameshatafuta eneo. Kwa hiyo, tunaomba Hospitali ya Utengamao ijengwe nzega kama Serikali ilivyotuahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa *TMDA*, kwa muda mrefu *TFDA* ilikuwa inapima vyakula, baada ya kuwa *TMDA* tunaomba irudishwe iwe *TFDA* iendelee na kazi iliyokuwa ikifanya awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, ninashukuru sana kwa nafasi hii, ninamwombea Mungu Rais wetu aendelee, Mawaziri wetu wa Afya waendelee ili tupate afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsanteni.ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante kwa mchango wako. Sasa ninamwita Mheshimiwa Clayton Revocatus Chipando, atakuwa mchangiaji wetu wa mwisho.

**MHE. CLAYTON R. CHIPANDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye Wizara ya Afya. Kwa sababu dakika ni chache, ninaomba nikimbizane, nilikuwa na vitu vingi sana vya kuongea katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ninaomba nichukue muda huu kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Tanzania. Ninataka niwaambieni na hii ibakie kwenye kumbukumbu ya Bunge hili. Kazi aliyoifanya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenye Wizara hii ya Afya itabakia kwenye kumbukumbu za Watanzania milele na milele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimetembea mikoa kwa mikoa nikiwa na kampeni yangu inaitwa "Mama hana deni." Moja kati ya vitu ambavyo nimeshuhudia kwa macho yangu ni majengo mapya ya kisasa yanayojengwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika mikoa yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nimekwenda kushuhudia vifaa vya kisasa na mitambo ambayo watu wote wa mikoani walikuwa wanalazimika kwenda Muhimbili ikiwa inapatikana katika mikoa yetu huko Kigoma, Mwanza na sehemu nyingine tofauti tofauti. Kazi iliyofanywa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan itabakia kwenye kumbukumbu. Kwa wale ambao kazi yao ni kupingapinga, hii inaitwa "Shikeni Adabu, Mama kafanya kazi." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nimpongeze Waziri wa Afya, Mheshimiwa Mchengerwa pamoja na Naibu wake dada yangu Mheshimiwa Dkt. Florence. Ninataka niwaambieni Waheshimiwa Wabunge, hii *combination* ni ya hatari. Tuwe macho kushuhudia kazi inayoenda kufanywa na hawa majemedari wa kazi. Ukisikia Mheshimiwa Mchengerwa anaitwa Mtu Kazi, tunamjua kutokea Wizara nyingine alizotokea huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi kubwa aliyoifanya Mheshimiwa Mchengerwa katika Wizara nyingine inatupa imani kubwa kwamba bajeti hii tumwachie aende nayo ili tuweze kuona matokeo katika Wizara ya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niwaambieni Waheshimiwa Wabunge, moja kati ya vitu ambavyo vitabakia katika kumbukumbu

ya maisha yangu, ni jambo la kutengewa shilingi 8,000,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Kanda Kigoma Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kigoma tuko karibu na Burundi, tuko karibu na Zambia, tuko karibu na Congo. Hizi fedha tunazokopa tunafanyaje? Zinatakiwa zirudi. Ili zirudi, ni lazima tuchukue fedha za Congo, na za Burundi, za Zambia. Lazima Kigoma iwe ndiyo sehemu kama *hub* ya nchi hii kukusanya fedha kupitia Wizara ya Afya. Mwaka 2025 zilitengwa, haikujengwa? Ninaomba mwaka huu tuanze ujenzi, shilingi 8,000,000,000 zianze kufanya kazi katika Jimbo la Kigoma Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka haraka ninaomba sana Wizara ya Afya iweke kitengo cha kutoa elimu mtandaoni. Washauri wa mitandaoni wamekuwa ni wengi, watatumaliza. Unaweza ukalala, ukaamka asubuhi ukakuta umekatazwa kula kila kitu. Kuna mtu anakataza usile ugali. Jamani, mimi nimekula ugali miaka 35. Leo hii ndiyo ukila ugali unaambiwa sasa ndiyo umejimaliza kweli! Hivi watu wa vijijini unaweza ukawapa hiyo *idea* kweli eti mtu asile ugali! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafadhali sana tunawaomba Wizara itenge kitengo maalumu cha kutoa elimu mtandaoni. Hawa wanaongea ovyo ovyo wakamateni. Elimu wanazotoa hizi za ovyo ovyo zinatupotosha. Huyu anakwambia kula maembe, huyu anasema maembe yana sukari. Sukari ni ule utamu, kwa hiyo, hata ukila maembe, yana sukari. Wanatuchanganya, tunaomba mtengeneze kitengo maalumu kwa ajili ya mitandaoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nigusie bima ya afya. Watu wengi wamezungumzia Bima ya Afya kwa Wote, na sisi tunaunga mkono Bima ya Afya kwa Wote kwa sababu tunaamini...

**MHE. KASSIMU A. MBARAKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Clayton Chipando kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Kassimu.

**MHE. KASSIMU A. MBARAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumpa taarifa Mheshimiwa Baba Levo kwamba China imepitisha sheria na utaratibu kuwa mwenye mamlaka pekee ya kuongelea masuala ya huduma mbalimbali za afya na ushauri wa kitaalamu wa kiafya kwenye mitandao ya kijamii ni mtu aliyethibitishwa na mamlaka husika na mwenye vigezo husika. Hiyo taarifa ninampa, na aichukue. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Clayton Chipando unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. CLAYTON R. CHIPANDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea mama na unilindie kamuda kangu. Unajua kengele haitachukua taarifa. Ninaipokea na ninadhani anaunga mkono suala letu la kuhakikisha tunadhibiti waongeaji wa kwenye mitandao ambao wamepitiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, turudi kwenye bima ya afya. Kwanza ninaunga mkono Bima ya Afya kwa Wote. Wabunge wenzangu watakuwa mashahidi hapa, tunaopata shida zaidi ni sisi Wabunge ambao tuko kwenye majimbo yetu. Mwananchi akiugua, hana hela atakuja kwako, lakini kama tukifanikiwa Bima ya Afya kwa watu Wote, tafsiri yake ni kwamba suala la kuanza kutibiana na wananchi litapungua katika miji yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bima hii ya afya tunaomba iunganishwe na *ambulance* kwa sababu mtu anatibiwa bure kutokana na bima aliolipia, lakini akipewa rufaa inabidi achangie mafuta ya *ambulance*. Kwa mfano, Kigoma, na ninashukuru sana niwapongeze uongozi wa Hospitali ya Maweni. Ilikuwa kusafiri kutoka Kigoma mpaka kwenda Dar es Salaam *ambulance* ulikuwa unalipia karibia shilingi milioni mbili na kitu, shilingi 1,600,000 sijui, ambapo kwa ndege *go and return* shilingi 700,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ina maana mgonjwa bora amlipie dokta kwenye ndege inakuwa ni shilingi milioni 1.4 wanaenda wanarudi kwa ndege, wanaachana na *ambulance*. Kwa hiyo, tunaomba kwenye bima iingizwe na *ambulance* ili mgonjwa huyo anayetibiwa kwa bima akipata rufaa *ambulance* imbebe asidaiwe fedha nyingine, kwa sababu tunawajua watu wetu, hali zetu ni ngumu huko mtaani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine kuhusu ujenzi wa Muhimbili, ninashangaa mtu ambaye anapinga ujenzi wa Muhimbili. Mimi nimetembea katika nchi za wenzetu, unaingia hospitali ni kama unaingia katika hoteli ya *five star*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaingia kwenye hospitali unaweza ukajua unaingia *airport*. Safi *(clean)*, za kisasa, mitambo ya kisasa iko mle ndani. Namwomba Mheshimiwa Mzee Mchengerwa, hawa wanaopingapinga atuachie sisi, yeye aende kufanya kazi. Aende akafanye kazi. Sisi tunatoa baraka zote, Mungu amjalie apewe hizo fedha, aende akafanye kazi ili watu waje wajifunze katika Hospitali yetu ya Muhimbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninaomba sana hili mlichukue kwa ukubwa. Kumekuwa na tatizo, watu wanasema madokta wengine wanakimbia kufanya kazi vijijini. Ninaomba sana Mheshimiwa Mzee Mchengerwa aje na mbinu mbadala, waongezee hela madokta wanaofanya kazi vijijini. Mimi ninakuambia kuna watu wanalima dhahabu maporini huko, watu wanatafuta hela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiwaambia kama ukiwa mjini ni shilingi 2,000,000, ukiwa kijijini ni shilingi 4,000,000, utaona wote wa mjini watahamia vijijini kwa sababu watu wanataka hela. Tengeneza mazingira mazuri. Hakuna mtu ambaye hataki kwenda kufanya kazi sehemu ambayo atapata hela nyingi ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hayo, leo nimemaliza kwa wakati. Kwa kusema hayo machache kwenye Jimbo la Kigoma Mjini tuna ombi maalumu la uwezeshaji wa *OPD* pale, fedha zimepelekwa,

ukarabati unaendelea. Tunaomba wale wakandarasi wamalizane kabisa ili tubaki tunawadai kazi na wasibaki wanatudai chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri na Mwenyezi Mungu awasaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa uchangiaji kwa mchana wa leo. Watakaoanza jioni ni Mheshimiwa Jamila Mahmoud Juma, Mheshimiwa Dkt. Zeyana Abdallah Hamid, Mheshimiwa Amina Iddi Mabrouk na orodha itaendelea.

Waheshimiwa Wabunge, tunakumbushwa mara baada ya hapa kutakuwa kuna semina Ukumbi wa Msekwa.

Baada ya kusema haya, ninasitisha Shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 06.58 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**12 MEI, 2026**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano yetu. Tunaanza na Mheshimiwa Jamila Mahmoud Juma, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Zeyana Abdallah Hamid na Mheshimiwa Amina Iddi Mabrouk ajiandae.

**MHE. JAMILA MAHMOUD JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi kwa nafasi uliyonipatia ya kuweza kuwa mchangiaji wa kwanza kwa *session* hii ya jioni. Pia, nisiwe mkosefu wa shukrani, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kwa kutuwezesha kuwa hai mpaka muda huu na kuweza kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninachukua nafasi hii pia, kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mama yetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, mama wa Watanzania, mama wa ukweli, mama mchapakazi. Bila ya yeye hapa sasa hivi tusingekuwa na furaha ya kuchangia Hotuba ya Wizara ya Afya kwa jinsi ya namna alivyowawezesha na kuthamini afya ya Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ninachukua nafasi hii kumshukuru au kumpongeza Waziri wa Afya kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuhakikisha kwamba jamii ya Watanzania inapata huduma ya afya sahihi na kwa wakati. Sio yeye peke yake anayefanya hii kazi, anasaidiana na Naibu wake, Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi, naye pia, anastahili hizi pongezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi hizi zisingeweza kusimama au kutangazika kama Watendaji wa Taasisi na Wizara ya Afya wasingekuwa wanatoa ushirikiano wa karibu kwa Mheshimiwa Waziri na msaidizi wake. Kwa hiyo, ninachukua nafasi hii pia kuwapongeza watendaji wa Wizara ya Afya wakiongozwa na Katibu Mkuu, Dkt. Seif na watendaji wengine wote kupitia vitengo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michango yangu itaangazia maeneo mawili makuu, lakini muda ukiruhusu tutaweza kuangalia na vitu vingine. Jambo la kwanza ambalo nitalizungumzia ni suala zima la ujenzi wa Hospitali ya Muhimbili na pia, nitazungumzia suala zima la Hospitali ya *MOI*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona kwamba, kupitia kiongozi wetu Jemadari, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ametoa bajeti au fedha za kutosha kuhakikisha kwamba ujenzi wa Hospitali ya Muhimbili Mpya unafanikiwa. Naweza kusema kwamba, uazishwaji au ujenzi wa Hospitali ya Muhimbili Mpya lengo lake kubwa ni kutoa huduma za kisasa kwa wagonjwa ambao wapo Tanzania na nje ya Tanzania, lakini pia, ujenzi huu au kupatikana kwa hospitali hii kutapunguza suala zima la rufaa, ambapo mara nyingi tumeona wagonjwa wengi wanatoka Tanzania na kukimbilia matibabu kwenye nchi za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii imetoa fursa kwa Watanzania kuweza kupata huduma sahihi na kwa wakati sahihi. Pia, inatoa fursa ya kuongeza kipato au kuongeza Bajeti ya Wizara ya Afya kwa sababu ya kupitia au kutopitia huduma ya tibautalii. Uwekezaji wa Hospitali ya Muhimbili, pamoja na kwamba, tumeona kutakuwa na majengo ya kisasa na huduma za kisasa, lakini huduma bora hazipatikani kupitia majengo tu, bali kutokana na huduma inayotolewa ya utendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakapokuwa tunajenga hospitali yetu, muhimu ni tunatakiwa tuzingatie rasilimali watu na rasilimali vifaa. Tunahitaji kuwa na madaktari wabobezi na wahudumu ambao wanafanya kazi katika mazingira mazuri, lakini pia, kuwa na vifaa ambavyo vitaweza kuendana na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji kuwa na programu za kuwa na ubunifu na kufanya tafiti mbalimbali. Hivyo basi, ninashauri wakati tunaendelea na ujenzi, basi twende sambamba na utayarishaji wa rasilimali watu kwa kuwapatia mafunzo na pia, kutafuta na kutayarisha vifaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia mafunzo, tunamaanisha, kwa upande wa madaktari na watendaji wake, lakini pia, kwa sababu tunakwenda katika masuala ya teknolojia, tunahitaji kuwa na watendaji ambao wamepata elimu ya kutosha katika masuala ya teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimalizie kidogo kwamba, hivi karibuni kulikuwa kuna suala la mifumo. Kuharibika kwa mifumo ambayo ilisababisha baadhi ya wanafunzi wa *internship* pale Muhimbili kurejea mitihani yao kwa sababu tu kulikuwa na tatizo hilo, mwanafunzi huyu anaweza kupata *report-result* ame-*pass,* akiamka inakuja *result* ame-*fail* na kutakiwa akafanye mafunzo. Sasa hii mifumo kama haitakuwa na wasimamizi imara, basi inaweza ikaleta hitilafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Hospitali ya *MOI* tunashukuru kwamba, imefanya vizuri. Imeweza kuongeza upatikanaji wa huduma. Tumetoka kwenye kuhudumia wagonjwa 8000 mpaka wagonjwa 18,000. Ninaomba tu, kupitia hapa, pamoja na kwamba tunatoa huduma, lakini tunahitaji Hospitali ya *MOI* kuongeza wigo, kuenea katika maeneo mengine ya Tanzania ikiwemo Zanzibar kwa sababu, kule Zanzibar tumekuwa na wagonjwa wengi ambao wanapata matatizo ya kuhitaji huduma za upasuaji, lakini wanashindwa kuzifikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba Wizara iangalie hiyo, kufungua kitengo chake pale Zanzibar. Aidha, kufungua kimoja kwa ushirikiano na hospitali zilizo Zanzibar ili kuweza kuwahudumia Wazanzibari, kwani nao pia ni Watanzania na wana haki ya kupata fursa na manufaa ambayo yanatoka katika Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Ninamtaja Mheshimiwa Dkt. Zeyana Abdallah Hamid. Mheshimiwa Amina Iddi Mabrouk na Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya, wajiandae.

**MHE. ZEYANA ABDALLAH HAMID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha leo kukutana tena kwa siku ya pili kuchangia Bajeti ya Afya. Ninawashukuru sana wachangiaji wengi, hasa wa Kamati ya Afya ambao tumekaa pamoja na Wizara, tunaenda kuandaa mipango mipya ya 2026/2027 itakayohakikisha matumaini, maelekezo, maono ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tunayatendea haki ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametuamini kwenye azma yake hii, na hawa ni wananchi wake wapendwa. Analilea Taifa hili na kipaumbele chake cha mwanzo ni afya. Ninaomba nitoe shukrani pia kwa taasisi mbalimbali ambazo wametu-*host* kipindi cha ziara. Tumeona kwa macho yetu, na ninapenda kutumia sauti hii kuwaambia wananchi kwamba *investment* iliyofanyika Tanzania ni kubwa mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kuna matokeo ambayo tutatolea kama mifano ili sote kama Taifa tufunge mikanda kwamba, safari bado inaendelea chini ya uongozi wake jemedari wetu, mtu kazi. Leo tumesikia jina ambalo wengine hatukulizoea, Mheshimiwa Mchengerwa pamoja na msaidizi wake mahiri sana, Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi. Ukiangalia Wizara ya Afya kwa kweli, ina wataalamu waliobobea. Mimi wenyewe najisikia fahari kuongozwa na Katibu Mkuu, Dkt. Seif Shekalaghe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tumetembelea taasisi tofauti na Wakurugenzi wamekuwa wakituonesha kazi halisi inayofanywa kutoka haya ambayo yanapangwa kwenda kwenye yale ambayo yanatekelezwa. Ninamshukuru sana na ninampongeza sana Dkt. Grace Magembe, Daktari Mkuu; pia, kuna vinara wa Wizara ya Afya, Mkurugenzi wa Muhimbili, ninampongeza sana Dkt. Delilah na Wakurugenzi wengine wa taasisi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi zimewezeshwa kwa wataalamu na vifaa. Kinachohitajika sasa hivi ni tuunganishe nguvu kusindikiza

bajeti ipewe vipaumbele vya *finances*. Tusindikize wafanyakazi, tuwape moyo wafanyakazi, tuangalie changamoto zilizobakia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michango yangu mikubwa ni miwili leo na ninapenda nianzie moja kwa moja kwenye kile ambacho Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametung'arisha nacho ulimwenguni, upungufu wa vifo vya mama wajawazito. Tulioshiriki mikutano ya Kimataifa ukiwaambia tu unatoka Tanzania wanakuambia, Tanzania ile yenye *champion* wa *maternal death reduction*? Unawaambia, ndiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala linalofuata na ambalo ninawasihi Wabunge wenzangu ni kila mmoja wetu kuanzia sasa ajitayarishie kujibu. Tulifanyaje? Kwa sababu, hilo suala tunaulizwa na wananchi wa kawaida, pia wanataka kujua kwani tumefanyaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni *investment* iliyofanyiwa kazi kimkakati. Ninaomba niende kidogo kwenye takwimu na nitakuwa *very brief*. Katika kila vizazi 100,000 Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametushusha kutoka kwenye vifo 556 mpaka 504. Hili ni punguzo la 80%, ni kubwa, ni la kihistoria na linaendelea kushangaza ulimwengu. Sisi Watanzania tunasema tunaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunajipongeza na hili, kuna takwimu ambayo ni pacha ya takwimu hii, ninapenda pia, nizungumzie watoto wanaozaliwa katika hivi vizazi 100,000 wanaofariki, tunawapoteza kwa masikitiko, bado ni 2,400. Sasa tukilinganisha hii 104 ambayo *work was done* na tukitazama hii 2,400 katika 100,000 ile ile, tunajiambia nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi bado iendelee. Huu ni mchango ambao tumekuja kukaa kama kamati na tumeona kuna siri ambayo leo ninaomba Wabunge wenzangu tuipate na nina hakika Wizara nayo inaangalia kwa umakini. Taarifa zimeonesha kwamba, tunajipanga hivyo, lakini vizazi vya watoto vinaweza kupunguzwa sana kwa kuweka huu mwambata wa mama na wachangiaji wenzangu wengi wamezungumza kwamba, pamoja na uchache wa

wafanyakazi tulionao, hatuna sababu ya kumpoteza mtoto huyu mchanga, ikiwa mwambata atakuwa ni sehemu ya uzazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwambata huyu sisi hatuna uwezo wa kumgharimia. Hatumlipi wala hatumsomeshi, lakini kuna taasisi ambayo imefanya utafiti na ninaomba niitaje. "Thamini Uhai", ambayo imeshirikiana na *NMR*. Kuna taarifa za uhakika kwamba, mwambata ana sehemu kubwa ya kum-*save* mtoto mchanga huyu tusimpoteze, baada ya kuwa tumem-*save* mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michoro iliyoandaliwa ni kazi ambayo watu walikaa wakatafakari na wakathamini kumbe kila chumba kinagharimu shilingi 2,000,000, 3,000,000, nyingi ni 4,000,000. Hii siyo gharama kubwa ya kukaa mimi leo nikaizungumza siku muhimu kama leo ya bajeti, lakini kwa vile kuna namna ambayo sote tukikubaliana, tutaweza kuitekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba na ninawasihi Wizara ya Afya na TAMISEMI tuiangalie hii *investment* ndogo, tukaishushe ile 2,400 ya watoto wachanga, ili tupate zawadi nyingine. Mheshimiwa Rais atambulike kushusha kama alivyoshusha vifo vya mama na watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbona ninavyoiangalia hii ni kazi ambayo hata Halmashauri jamani inaweza kuibeba! Kama ni michoro, ipo; kama ni miongozo, ipo; kama ni sheria, ipo; kama ni azma, ipo; na tunajua Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, anatutegemea tukawa-*save* hawa watoto wachanga, basi ninaamini tukishikamana, hili linawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitoe mchango wangu wa pili, nao ninakwenda kwenye mifumo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Malizia, kengele imelia, malizia.

**MHE. ZEYANA ABDALLAH HAMID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimalizie. Wizara ya Afya nawa-*salute* kwa kutuletea mwarobaini wa mifumo kusomana. Pamoja na kwamba, michango mingi ilikuwa inazungumza kama kushauri, ninaomba niwakilishe Wabunge wenzangu, ushauri wote ambao tumeutoa leo, kama utaisoma ile bajeti vizuri kwa kutulia, wamepita kila kwenye mpango unaohitajika, ninauita mwarobaini na ninathubutu kusema hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mkufunzi wa mifumo ya afya katika ngazi ya *Masters* na *Ph.D* na kila tunachokisomesha kwa mifano chungu nzima ya Marekani na Uingereza, Wizara ya Afya imetuwekea. Ninachowasihi wafanyakazi wa sekta ya afya ni kwamba twendeni tukabadilike. Haya ni mabadiliko ya kiutendaji. Tunaweza tukaona ni makubwa, yanaongeza mzigo kwenye mazungumzo yetu ya kazi, lakini hapana, yanakwenda kutufanyia kazi yetu kuwa nyepesi, kuwa ya uhakika, tuka-*save* maisha ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaenda ku-*save* gharama kubwa sana. Tathmini zinaonesha katika kila Dola moja inayokuwa *invested* una-*save* Dola mbili hadi tatu na hizi ni data zilizofanyiwa *research*. Tunaweza kuona ni fedha nyingi tunawekeza, lakini tutakuja kuona gharama ambazo tumeziweka, *within one year* tutakuja kukutana hapa tunapongezana kwa kazi nzuri ambayo Wizara imetufanyia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tu-*support* hii kazi, tusomeshe vijana wetu *digital health transformation,* ndiyo mpango mzima. Ninawapongeza sana Wizara. Ahsante kamati kwa ushirikiano, ahsante kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mheshimiwa Dkt. Zeyana Abdallah Hamid. Nilimtaja Mheshimiwa Amina Iddi Mabrouk, atafuatiwa na Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya na Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo ajiandae.

**MHE. AMINA IDDI MABROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, ambaye ametujalia jioni hii kuwepo hapa, lakini pia, amenijaalia niweze kusimama kutoa mchango wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee ninaomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maono yake na mageuzi makubwa ndani ya sekta hii ya afya. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kipindi chake ameweza kujenga na kuboresha hospitali katika kila Wilaya. Kaweka vifaa tiba, na pia, ameweza kuweka mashine za kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi ninavyokwambia imesababisha huduma bora na nzuri kwa wananchi wote wa Tanzania. Kwa mfano, mwaka 2021 kulikuwa kuna *MRI* saba, sasa hivi ninavyokwambia, mwaka huu 2026, kuna *MRI* 13. *CT-Scan* Mwaka 2021 zilikuwa 13, sasa hivi kuna *CT-Scan* 45. *Ultrasound machine* mwaka 2021 zilikuwa 476, hapa ninavyozungumza zimeongezeka kufikia 970. Kulikuwa na *Digital X-Ray* 147, sasa hivi ninapozungumza kuna *Digital X-Ray* 491.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ni baadhi tu ya vifaa ambavyo nimevitaja, kwa kweli kama nitavitaja vifaa vyote hapa, ninaweza muda wangu wote nikaumaliza. Pamoja na mazuri haya ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameyafanya na anaendelea kuyafanya, tumpe maua yake, tumpe heshima yake kwa kumtambua yeye ni Mama wa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu, sasa ninampongeza Mheshimiwa Waziri Mchengerwa. Mheshimiwa Waziri huyu amefanya mambo makubwa toka kipindi chake. Ninampongeza sana yeye pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri wake na Watendaji wake. Ninaamini kwamba bila ushirikiano wa pamoja, wasingeweza kufanya maendeleo haya makubwa. Ninamuomba sana Mheshimiwa Waziri aendelee kuchapa kazi, sisi tuko pamoja naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatambua kwamba umuhimu wa kujenga hospitali mpya nchini, lakini bado Hospitali ya Taifa Muhimbili ina nafasi kubwa katika utoaji wa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi. Kwa umuhimu huo, ninaomba kusema kwamba bado Watanzania tunahitaji sana ujenzi mpya wa hospitali ya Muhimbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuungana na wenzangu waliotangulia na ninaamini kwamba wananchi wote na Watanzania wote wanatuangalia tunasemaje kuhusu ujenzi huu wa Muhimbili mpya. Ninaomba Waheshimiwa Wabunge tuidhinishe bajeti hii ambayo imetengwa siyo zaidi ya shilingi trilioni 1.2 ili tumpe nafasi Waziri ya kwenda kujenga hospitali ya Muhimbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu, ninampongeza tena Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika siku zake 100 za ahadi tangu kuingia madarakani…

*(Hapa Kengele Ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. AMINA IDDI MABROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha pili cha awamu ya Sita, ameweza kutekeleza Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote Sura 161 ambapo utekelezaji wake ulianzia Januari 26, 2026. Ninawapongeza sana Wizara, tunatambua kwamba tayari wameanza awamu hii kwa kutekeleza kuwasajili wananchi siyo zaidi ya milioni moja. Hii ni hatua kubwa sana, hatua ambayo tunastahili kuwapongeza Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninawaomba sana Wizara ya Afya wajitahidi sana kuendelea kuwatambua wale wananchi ambao hawana uwezo ili waweze kufikia lengo ambalo limekusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninampongeza sana Waziri pamoja na timu yake kwa utekelezaji wa Sheria hii ya Bima ya Afya kwa Wote katika kufanya mifumo kusomeka, kwa kuunganisha mifumo ya vituo

vya kutolea huduma za afya na mifumo ya Kitaifa ya Bima ya Afya. Tayari sasa hivi hospitali 28 za rufaa, za Mikoa, Kanda Maalumu na Taifa zimeanza kusomana. Hii haijapata kutokea. Haya ni maendeleo makubwa kwa Taifa letu, haya ni maendeleo ambayo tutaweka historia ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kengele ililia, nilikuwa ninangojea umalizie tu.

**MHE. AMINA IDDI MABROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana ninaomba kumalizia kwa kusema ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na ninawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu tuiunge mkono bajeti hii ya Waziri. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Amina Iddi Mabrouk. Nilimtaja Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya, atafuatiwa na Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, na Mheshimiwa Eng. Amosy William Maganga ajiandae.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kupata fursa ya kuchangia katika Wizara hii ya Afya. Ninaomba kumshukuru kwanza Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai, kutupa uhai sisi sote ambao tuko humu ndani, kutupa afya njema, kwa kweli yeye ni mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kumshukuru Mheshimiwa Rais. Nisipomshukuru Mheshimiwa Rais sijui ninaweza kujisikia vipi maana ninaweza nisimalize kuchangia. Ninamshukuru kwa mengi sana ambayo ameyafanya katika nchi hii, na mimi ninaamini katika watu ambao wanaamini kabisa katika Rais ambaye atakuja kukumbukwa akimaliza muda wake, ni Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mambo ambayo anayafanya, kwa mambo ambayo ameyafanya na kwa mambo ambayo anaenda kuyafanya. Atatengeneza historia ya kuwa mwanamke shupavu, shujaa, jasiri, mvumilivu, mwenye huruma, na mchapakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema haya? Mheshimiwa Rais kwa muda wa siku zake 200 ameweza kuajiri watu 5,000 kuwa watumishi wa kitengo cha afya peke yake. Siyo hayo tu, Mheshimiwa Rais ameweza kupunguza vifo kutoka vifo 550 mpaka vifo 104 katika *rate* ya idadi ya vifo 100,000. Hili siyo jambo dogo, ni jambo kubwa sana, lazima tumpongeze. Kwa kuwa yeye ni mama, anafahamu machungu ya mzazi, machungu ya mtoto kukosa mzazi, kwa hiyo lazima nimpongeze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitashukuru Bima ya Afya kwa Wote. Bima ya Afya kwa Wote imeanza tarehe 22 Machi na sasa hivi inaenda kutengeneza mkakati wa kusaidia *special groups,* yaani wanawake, makundi maalum, wale wasiojiweza pamoja na watu wenye ulemavu. Kwa nini nisiendelee kumshukuru Mheshimiwa Rais? Nitakuwa mchoyo wa fadhila.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, ninaomba kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuleta mashine au kipimo kikubwa cha saratani ambacho ni cha pili katika *Sub-Sahara Africa*. Unaweza ukaona namna gani Mheshimiwa Rais ameweza kutuheshimisha Tanzania. Siyo hivyo tu, kwa ajili ya kutaka kulinda afya za watu wake ambao wamemchagua, Mheshimiwa Rais, kipenzi chetu ameweza kuandaa mkakati mzuri wa kusaidia magonjwa yasiyoambukiza. Haya magonjwa yote yanaenda kutibiwa bure. Nani kama Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, Mheshimiwa Rais ametuletea mashine zile za kuondoa saratani ya awali kwa watu wenye ualbino, ni nani kama Mheshimiwa Rais? Mashine hizi zipo katika hospitali kadhaa kama *CCBRT*, *KCMC*, Bugando na *Ocean Road* ambayo huduma hii inatolewa bure. Yote hii anaenda kutuongezea *life span* ya mtu mwenye ulemavu wa ngozi au mtu mwenye ualbino. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri, pamoja na yote ambayo nimeyazungumza hapa, Mheshimiwa Waziri,

ni msikivu na watu wote wanaamini ni mtu kazi, ninaomba mashine hizi zisambae Tanzania nzima. Maisha yetu yanategemea hizi mashine kwa sababu unapoona kidogo una kipele, unaweza kwenda kukitoa kipele hiki kabla hakijaleta ugonjwa mkubwa wa ngozi wa saratani. Hii inaenda kutusaidia sisi maisha yetu, nikisema sisi ninamaanisha mimi ni mmojawapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu uwezo wa Mheshimiwa Waziri, nafahamu uchapakazi wake na ninaamini hili anaenda kulibeba na kupeleka Tanzania nzima, na hamna kinachoshindikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine ambalo ninaliomba, kila siku naulizwa na Waheshimiwa Wabunge hapa tunapataje yale mafuta? Ninaomba utengenezwe utaratibu mzuri kupata mafuta ya *sunscreen* kwa ajili ya kulinda afya za watu wenye ualbino. Kwa sababu gani? Bila haya mafuta, sisi hatutembei; bila haya mafuta, hatu-*participate* kwenye majukwaa yetu; bila haya mafuta, hatuwezi kushirikiana na wenzetu. Kwa hiyo, maisha yetu yanategemea mafuta haya. Kwa hiyo, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, ninaomba kupongeza juhudi hizi ambazo zinaenda kufanyika, katika kuandaa mkakati wa kutengeneza viwanda kwa ajili ya madawa. Mwenyezi Mungu awabariki sana. Hii inaenda kuondoa tatizo kubwa la kupatikana kwa dawa katika Tanzania yetu. Ni jambo kubwa sana, hatutaweza kwenda kutegemea tena huko nje kama watatuletea au kama tutanunua huko nje, zitakuwa ni kwa kiwango kidogo sana, lakini tutaweza kutengeneza dawa zetu wenyewe na kutibu wananchi wetu kwa sababu tunafahamu umuhimu wa afya ni jambo la muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hayo machache, ninawashukuru, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya. Nilimtaja Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mheshimiwa Eng. Amosy William Maganga na Mheshimiwa Kassimu Amari Mbaraka, ajiandae.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti ya Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai. Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, ninapenda kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, mwanangu sana huyu tulikuwa naye Kamati ya Katiba na Sheria na Mheshimiwa Dkt. Florence mwanangu pia tulikuwa Kamati ya Maliasili na Utalii, kwa kazi nzuri. Sina wasiwasi nao, ninajua watatenda kazi nzuri na Wizara ya Afya itasonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia kutumia nafasi hii kwa kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri alizozifanya kwenye sekta ya afya kwa Watanzania. Baada ya pongezi hizo, pia ninapenda kutumia nafasi hii kumpongeza Mganga Mkuu wa hospitali yetu ya Mkoa wa Katavi Dkt. Banuba. Ninawapongeza pia wafanyakazi wote nchini Tanzania, Madaktari na Wauguzi. Kazi ya udaktari na uuguzi ni ya wito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niende kwenye mchango kwenye Wizara ya Afya. Pamoja na pongezi hizi, kuna upungufu kwenye mkoa wangu wa Katavi. Kwanza kabisa ninapenda Mheshimiwa Waziri wa Afya afahamu kwamba mkoa wetu wa Katavi hospitali ya rufaa haijakamilika. Hospitali hiyo mwaka 2025 kwenda 2026 kwenye bajeti yake iliomba shilingi 5,000,000,000. Katika hizo shilingi 5,000,000,000, Serikali imeleta shilingi 269,000,000 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizo Mheshimiwa Waziri hazitoshi kumalizia jengo la mama na mtoto ambalo ndiyo kuna wodi ya akina mama, kuna wodi ya watoto, kuna kuna vyumba vya upasuaji na kuna vyumba vya *laundry* kwa ajili ya kufua mashuka ya hospitali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mheshimiwa Mchengerwa mtu kazi, mwanangu, anipatie shilingi 5,000,000,000 kwenye Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Katavi ili iweze kukamilika. Nikiwa nimesimama hapa, wananchi wa Mkoa wa Katavi wamenituma nimwambie Waziri kwamba Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Katavi haina mochwari, wagonjwa wanapofariki kwenye hospitali hiyo, wanatakiwa kusafirishwa kupelekwa kwenye Hospitali ya Wilaya ambayo iko mbali takribani kilometa saba mpaka 12 ambako ndiyo kuna mochwari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii *inconvenience* inayoleta shida kwa wafiwa. Kwanza wanakodi gari la kubeba huo mwili kuupeleka kwenye hospitali, lakini zaidi ya hapo kwenye hiyo Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Katavi hakuna hata chumba hicho cha kuhifadhi hiyo miili. Kuna kijikorido fulani tu kimewekewa pazia, miili hiyo ndiyo huwa inawekwa. Mheshimiwa Waziri, niko chini ya miguu yako, ninaomba hizo shilingi 5,000,000,000 katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Katavi iweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mochwari ni muhimu. Jengo lililoisha pale kwenye Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Katavi, Mheshimiwa Waziri najua kuna siku atafika, ni *OPD* tu ndiyo iliyokamilika ambako kwenye hiyo *OPD* kuna vyumba viwili vya *ICU* ndiyo vinatumika kuwalaza wagonjwa. Mheshimiwa Waziri ninakuja kwako, ninakulilia, ninakuheshimu, wote ninyi wawili ninaomba fedha shilingi 5,000,000,000 kwa ajili ya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukilinganisha pia sisi Katavi tuko mbali kufika kwenye hospitali za rufaa. Tunatembea kilomita zaidi ya 700 kuifikia Hospitali ya Rufaa ya Mbeya au hapa Benjamini Dodoma. *Plan* yetu ya mwanzo ilikuwa ni kujenga hospitali ya Kanda. Kwa bahati mbaya Serikali imeona hospitali ya Kanda ijengwe Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama hospitali ya Kanda imejengwa Kigoma, ninawaomba chonde chonde mtukamilishie hiyo Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Katavi kwa kutupatia shilingi 5,000,000,000 ili tuweze kukamilisha hilo jengo. Umebaki mwezi mmoja

bajeti pesa hizo ziweze kufika huko. Ninaomba sana, tutakapomaliza bajeti yako leo Mheshimiwa Waziri uweze kunifanyia jambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninapenda kulizungumza hapa, pia ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kwenda kufungua utaratibu wa kujenga viwanda vya madawa nchini Tanzania. Hilo ni jambo jema. Tulikuwa na viwanda vya madawa zamani, lakini vile viwanda vilikufa. Bila viwanda vya madawa, hatuwezi kufika popote. Ninashukuru sana na ninapongeza sana kwa jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo na wengine wameweza kulizungumza hapa, ni suala la kuboresha hospitali ya Muhimbili, kuwa Muhimbili mpya. Tunaunga mkono hii hoja kwa mikono miwili. Ombi letu ni zile hospitali za rufaa za mikoa zikamilike basi na hiyo Muhimbili mpya ikijengwa tutakuwa tumekwenda sambamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni Bima ya Afya. Kwenye Bima ya Afya ninaipongeza Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu kuhusu Bima ya Afya, lakini kwenye Bima hii ya Afya ninaomba kutoa angalizo. Mara nyingi watu wamekuwa na Bima ya Afya, wanakwenda hospitali wanaishia kuandikiwa dawa, lakini zile dawa ambazo zina bei, zenye magonjwa makubwa huwa wanaambiwa wakanunue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa bima hii mpya ambayo inakwenda kuanzishwa nchini kwetu Tanzania, ninaomba iangalie hili suala isije watu wakakata hiyo bima mpya, wanapofika pale wanaandikiwa dawa, wanaambiwa wakanunue. Wanaambiwa kwamba hizi dawa hazipo, siyo *package* ambayo ipo kwenye bima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninaomba kusemea gonjwa moja baya ambalo Watanzania wengi wanakufa, ambalo saa nyingine tunakuwa hatufahamu. Kwenye bima hii ya afya, kuna magonjwa ambayo ni ya gharama. Magonjwa kama ya figo ambayo gharama

ya kusafisha kuingia kwenye *session* moja kusafishwa figo pale Muhimbili ni shilingi 180,000; kule Katavi ni shilingi 200,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujua, hii bima ya afya mpya itakuwa pia inawezesha wagonjwa wa figo, wagonjwa wa kansa wanaokwenda kupata matibabu wataweza kutumia hii bima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi, ninaunga mkono hoja ya Wizara ya Afya. Ombi langu ni lile lile mwanangu Mheshimiwa Mchengerwa, nimepiga magoti kwako ninaomba shilingi 5,000,000,000. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Taska Restuta Mbogo. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa *Engineer* Amosy William Maganga, atafuatiwa na Mheshimiwa Kassimu Amari Mbaraka na Mheshimiwa Patrick Adkin Mwalunenge ajiandae.

**MHE. ENG. AMOSY W. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kuweza kunipa nafasi hii ili na mimi vilevile niweze kuwa mchangiaji katika Wizara hii ambayo ni muhimu sana kwa maisha ya Watanzania. Awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kutujalia uzima na afya na hatimaye kuweza kusimama mbele ya Bunge lako hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nianze kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mambo makubwa na kazi kubwa anayoifanya kuona kwamba anajenga ustawi wa sisi Watanzania. Kwa kweli katika jambo hilo, tunamshukuru sana. Amefanya mambo mengi sana, lakini sasa amekuja kugusa kwenye wizara hii ambayo ni muhimu kweli kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimpongeze sana hasa katika kuanzisha afya ya jamii kwa wote. Kwa kweli katika jambo hili tunamshukuru sana kwa sababu hii sasa ndiyo suluhu ya afya kwa Watanzania. Tunasema, mama ahsante sana kwa jambo hili ambalo umetuletea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwa kweli sasa leo nimekubali kwamba zigo zito mpe Mheshimiwa Mchengerwa. Mheshimiwa Mchengerwa ame-*prove* kwamba yeye mambo mazito ndiyo saizi yake. Amefanya mambo mazito kule TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile bado tunaona katika hii Wizara ya Afya bado anaendelea kutenda mambo ambayo ni mema. Amelivaa jambo hili la Bima ya Afya kwa Wote, amelibeba kwa nguvu zake zote. Watu huko wana mashaka kwamba sasa Watanzania wote wanakwenda kuingia kwenye bima ya afya. Je, dawa zitapatikana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ameliona, Mheshimiwa Rais amemwagiza naye amelibeba, akasema sasa anaagiza wawekezaji waweze kuweka viwanda hapa. Tuna imani kubwa sana kwamba sasa Bima ya Afya kwa Wote itawezekana chini ya Mchengerwa. Tunamshukuru sana Mheshimiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninamshukuru sana Naibu Waziri. Nimewashukuru sana watendaji wote wa Wizara kwa kazi kubwa wanayoifanya. Tunaamini watatuvusha. Hatuwezi tukaenda kwenye Taifa la uchumi wa kati tukiwa na Watanzania goigoi. Tunataka twende kwenye uchumi wa kati tukiwa na afya njema, tukiwa wenye afya ndipo hapo tutakapoweza kufanya kazi na kwenda kwenye uchumi wa kati. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, Bima ya Afya kwa Wote imeanza, ni jambo jema sana. Ninachoomba sasa, ianze kwa wote. Wameshaanza kweli kwa hizi kaya za *TASAF,* tunawashukuru. Sasa, waanze na kwa watu wengine wote. Wajue kwamba zaidi ya 70% ya Watanzania ni wakulima, na sisi wakulima, na mimi ni mmojawapo wa wakulima, tunategemea mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ndiyo wakati wa mazao sasa, tunaenda kuuza; tukichelewa tutapishana na gari la mshahara. Hii ni kwa sababu fedha zile tutazitumia kwenye mambo mengine, na hiyo

shilingi 150,000 itakuwa ni changamoto. Kwa hiyo, niwaombe sana kwamba sasa hii hebu ianze mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, bado kuna changamoto ambazo zipo, na hususan tunaotoka kwenye hizi wilaya hizi mbali. Mimi natoka kule Sikonge, tuna changamoto sana ya watumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii katika Jimbo langu la Sikonge, Wilaya ya Sikonge tuna upungufu wa watumishi 191. Nitawaletea hiyo orodha yote ya mahitaji hayo ya wafanyakazi. Nitamletea yeye, nitapeleka TAMISEMI, na vilevile na kule Utumishi, walifanyie kazi. Kama tunataka kuboresha kweli sekta ya afya ni vizuri tukawa na hawa watumishi wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, niishukuru sana Serikali kuhusiana na hospitali yetu ya Mkoa ya Kitete. Ni kweli kwamba kuna uwekezaji mkubwa sana ambao Serikali imeufanya katika hospitali yetu ile, lakini ninaomba, bado kuna mambo ambayo yanatakiwa kufanyika katika hospitali yetu ya Kitete. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza yale majengo ni ya muda mrefu. Mwenzangu amesema hapa, yana zaidi ya miaka 100, yamechakaa sana. Tunaishukuru Serikali wametusaidia kutengeneza *master plan,* tumeipata. Sasa tunaomba fedha zipatikane ili kusudi ile hospitali iweze kujengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile zile huduma za kibingwa, mama yangu, Mheshimiwa Mama Sitta amesema pale, tunazo chache. Kati ya 17 tunazo sita tu. Sasa tunaomba zile nyingine zipatikane. Zikishapatikana, nina imani kwamba Wanatabora tutakuwa tumefanyiwa jambo jema. Ni imani yangu kwamba kila kitu kinaenda hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakokwenda kule mbeleni yawezekana hiyo hospitali sasa ikawa ndiyo hospitali yetu ya kanda, lakini kwa kuanzia, tunaomba kwanza tuimarishe hiyo hospitali iweze kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo machache, ninamshukuru sana Naibu Waziri, nimeongea dakika tano. Kwa hiyo, mchango wangu wote *is almost* ameumaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

*Hapa Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kassimu Amari Mbaraka, wajiandae Mheshimiwa Patrick Mwalunenge, na Mheshimiwa Naibu Waziri atafuatia.

**MHE. KASSIMU A. MBARAKA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia siku ya leo, kuwemo tena katika Bunge hili Tukufu tukiendelea kuwatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa muhtasari, nami ninachangia katika hii bajeti ya Wizara ya Afya hoja kadhaa ambazo zitakuwa na faida kubwa kwa maslahi mapana ya Taifa, halikadhalika Jimbo la Tanga. Kwani ikizingatiwa Mkoa wa Tanga na Jimbo la Tanga Mjini, tunayo Hospitali pale ya Rufaa ya Mkoa maarufu, inaitwa Bombo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa muhtasari, ninataka nipitishe kidogo kwenye historia. Mwaka 1895 Dkt. Fredrick Plan, mtaalamu wa *tropical medicine* au *tropical disease* alijaribu kuangalia na kuona vifo vingi sana ndani ya Mji wa Tanga. Takribani 70% ya vifo vinatokea; akafanya utafiti wake na akabaini kuwa vinasababishwa na *Malaria; Cerebral Malaria* pamoja na *Black Water Fever,* hatimaye akawasiliana na Mganga Mkuu wa wakati huo ambaye ni Dkt. Alexander Baker.

Mheshimiwa Spika, alivyowasiliana naye, ikabidi wafikie maamuzi kujenga hospitali ya kwanza Tanganyika ambayo inaitwa *Bombo Hospital Cliff*. Kitaalamu kwenye maandiko ya historia tunasema *first*

*modern* hospital ikajengwa Tanga ndani ya Taifa hili la Tanganyika. Hiyo ni historia adhimu ninaomba ichukuliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini nimeileta hoja hii ya kihistoria mezani? Ni kwa sababu baadhi ya mambo yasipoeleweka, historia yake huchukuliwa sana kawaida. Hospitali hii ilihudumu kutibu majeruhi wa Vita vya Kwanza vya Dunia, watalamu na wafanyakazi mbalimbali waliokuwa wakipata majeraha kwenye reli, sasa nini kipo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jengo hili la *Cliff* lipo ndani ya Hospitali ya Bombo. Watu wa *TBA* na watu mambo ya kale wamekuja kulikagua na kuliangalia kama ni salama na linaweza kutumika. Lina umri takribani miaka 131, kwa hiyo linafaa kutumika. Sasa niiombe Serikali ilikarabati jengo ili liweze kutumika kwa ajili ya matumizi ya wodi ya mama na mtoto. Wakati tukisubiri kujenga wodi ya mama na mtoto tutumie jengo hili tukilikarabati ili liweze kutumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu *Venice Chatter* ya mwaka 1966 na *Burra Chatter* ya mwaka 1979, zote hizi *international document* kuhusiana na *cultural heritage and monument* zinaruhusu kukarabati majengo ya kale, kuyaweka vizuri, na yakiwa ni salama yatumike kwa maslahi mapana ya jamii, lakini huku yakiwa yana-*preserve* ile historia ya eneo husika. Kwa hiyo, *Cliff* inaangukia hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata ukija kwenye *by laws* za *UNESCO* na *cultural heritage* inazungumzia masuala haya. Pia inaruhusu jengo hilo likarabatiwe. Tumeona Tanga tulikuwa na shule inaitwa *Old Tanga*, leo hii imekarabatiwa na inatumika. Vilevile tunaona Zanzibar Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi anakarabati majengo mbalimbali ya kale na yanaendelea kukaa katika ubora wake. Ile *structure* haipotei, lakini kwa sababu ni salama yatumike. Kwa heshima na taadhima ninaomba Serikali ilikarabati Jengo la *Cliff* na lianze kutumika rasmi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza hayo, nukta nyingine ya msingi kabisa ni kuhusiana na hospitali yetu ya Bombo. Tuna Wodi

za Galanosi, Sokoine, na Mwapachu. Kwenye Wodi za Sokoine na Mwapachu mifumo ya maji na majitaka yote inatakiwa yarekebishwe, pamoja na mifumo ya umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile tunaomba hii Wodi ya Galanosi Serikali itazame kwa umakini zaidi, kwamba sasa hii wodi iweze kujengwa upya kulingana na mahitaji. Hii ni kwa sababu ndiyo wodi inayohudumia magonjwa ya *internal medicine*. Inachukua takribani 63% ya idadi ya wagonjwa wote wanaokuja katika Hospitali ya Bombo. Hili liangaliwe kwa mapana sana na liangaliwe vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyazungumza hayo, sasa niishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hususan Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutuletea mradi mkubwa wa Jengo la Damu Salama (Benki ya Damu Salama) ndani ya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tanga ambalo linaenda kumaliza changamoto inayotusumbua ndani ya Mkoa wa Tanga inahusiana na Benki ya Damu Salama. Vifaa tayari vimekwishafika, vitendea kazi vipo, kinachohitajika ni jengo hili sasa kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaishukuru Wizara ya Afya na Mheshimiwa Waziri Mohamed Mchengerwa pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri Dkt. Florence Samizi kwa kuhakikisha kwamba ndani ya Mkoa wa Tanga Hospitali yetu ya Bombo takribani shilingi bilioni 2.6 zimetengwa kwa ajili ya ukarabati na kumalizia jengo hili la mradi huu wa Damu Salama. Haya ni mambo makubwa na ni mambo ya kihistoria.

Mheshimiwa Spika, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa jambo hili kubwa na tukufu. Hapo awali hatukuwa na Benki ya Damu Salama. Tukihitaji mahitaji ya damu, lazima twende Kilimanjaro ili damu iweze kusafishwa, kuchakatwa, kisha baadaye ndipo irudishwe Tanga kwa ajili ya mahitaji, lakini sasa tunaenda kupata damu salama.

Mheshimiwa Spika, shukrani sana, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Patrick Mwalunenge na kabla ya Naibu Waziri atakuja Mheshimiwa Devotha Minja.

**MHE. PATRICK A. MWALUNENGE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia machache kwenye hii Wizara yetu muhimu kabisa kwa maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwanza ninampongeza Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uthubutu wake kwa uwekezaji mkubwa sana kwenye Wizara hii. Pia ninampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa na mabadiliko makubwa ambayo ameanza kuyafanya, tunayaona. Kweli yeye ni mtu kazi.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji uliowekezwa kwenye hospitali nchi nzima, na kwenye Jimbo langu la Mbeya Mjini ni mkubwa sana. Pale Mbeya Mjini ninayo Hospitali ya Kanda ya Rufaa, tuna mashine zote. Tuna *CT-Scan* tuna *MRI,* na vilevile inajengwa hospitali kubwa ya kansa pale Mbeya Mjini kwa ajili ya kuhudumia watu wote wa kanda hiyo. Maana yake ni kwamba, wagonjwa wanaotoka mikoa ya Katavi, Sumbawanga, na Songwe watatibiwa Mbeya. Vilevile, hata wagonjwa wakitoka nchi za jirani za Malawi na Zambia watatibiwa Mbeya. Ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri na pia ninampongeza sana Mheshimiwa Rais uwekezaji huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni maboresho ya Hospitali ya Muhimbili. Nchi za wenzetu, hasa hizi za jirani hospitali nyingi zinamilikiwa na watu binafsi, na ndiyo maana matibabu ni ghali sana, ukienda za wenzetu, hata ukienda huko India. Hapa kwetu Serikali imethubutu, inawekeza yenyewe na kuzimiliki hospitali hizo. Maana yake ni kwamba, gharama za matibabu zinapungua na kuwa na unafuu mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine niipongeze bima ya afya imeanza vizuri kwa zile kaya masikini. Hata hivyo, ninataka twende mbali zaidi, tutumie Wizara nyingine zitoe ushirikiano. Hapa ninaenda kwenye Wizara ya Kilimo. Mwenzangu amechangia kidogo, Wizara ya

Kilimo inaweza kutoa majawabu, kwa maana yenyewe ndiyo inayoshughulika na wakulima. 75% ya watu wetu ni wakulima.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wakati sasa umefika Wizara ya Kilimo kuwasajili wakulima wote kwenye ushirika. Kupitia mazao yao, wanaweza wakakatiwa Bima za Afya na Serikali haiwezi kubeba mzigo wowote. Wakatwe makato kidogo, na kila mtu atapata bima, tena akapata Bima *Premium* na akatibiwa bila shida ya aina yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri ashirikiane na Wizara hizo. Wizara ya Kilimo, Wizara ya Viwanda na Biashara, TAMISEMI, kwa maana wale vijana wa boda boda, bajaji wasajiliwe kwenye mfumo rasmi, na wanaweza wakakatiwa Bima za Afya hizi kupitia biashara yao yenyewe badala ya Serikali kubeba mzigo mkubwa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusu uwekezaji wa viwanda. Ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri. Hili alisimamie kweli kweli. Atapata vikwazo. Mheshimiwa Shabiby aliongea kwamba biashara hii imebebwa na mataikuni, ni sawa sawa na biashara ya madawa ya kulevya. Atapata vikwazo vingi sana, lakini asimame imara. Hiyo pekee itapunguza gharama kubwa sana za matibabu kwa wananchi wetu na nchi yetu kwa ujumla. Kwa hiyo, hilo alisimamie na aishike sana *private sector. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa niende mbali zaidi. *NHIF,* Mfuko wa Bima ya Afya ninadhani hao ndio wawe wa kwanza kuwekeza kwenye viwanda kwa sababu wana fedha, hivyo wanaweza wakawekeza kwenye kutengeneza viwanda vya kutengeneza dawa, wakatengeneza viwanda vya kutengeneza dripu za maji na zile huduma zikapungua sana gharama ndogo sana kwa wananchi wetu. Hii ni kwa sababu yeye ndiye hatimaye anayekwenda kukusanya ile fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa ninaomba sana *NHIF* aanze kuwekeza kwenye viwanda vya dawa. Kwanza atatengeneza ajira na pili, atatumia malighafi inavyotokana na wakulima wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kwa dawa za vikohozi atapata tangawazi, zinalimwa kwenye shamba letu, atapata vitunguu saumu, vinalimwa kwenye mashamba yetu sisi, atapata malighali mbalimbali, hata asali inapatikana hapa nchini. Kwa hiyo ni dawa nyepesi ambazo zitaongeza ajira kwa watu wetu, na pia zitauzwa kwa gharama nafuu kwa sababu itakuwa ni dawa ambayo inatengenezwa kutokana na malighafi za kwetu hapa.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ni kuhusu uadilifu wa watumishi wa afya. Ni kweli kwamba Serikali imeajiri. Tunampongeza Mheshimiwa Rais ameajiri watumishi 5,000, lakini wengi wanaenda kusomea zile kazi ili apate ajira ili ndani ya mioyo yao hawana ile *spirit* ya kwenda kuhudumia watu.

Mheshimiwa Spika, baadhi yao wanakuwa na lugha mbovu, wananyanyasa wazee, wananyanyasa akina mama wanaokwenda kujifungua. Kwa hiyo, nilikuwa ninaomba sana, atakapokuja ku-*wind up,* atufafanulie na utueleze kwamba ni hatua gani atakayoichukua? Kabla ya watu kwenda kuajiriwa, wanapelekwa kwenye mafunzo ya aina gani ili kuwajengea uadilifu na kwenda kuipenda kazi yao?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kazi ya kuhudumia wagonjwa ni kama ibada ni kama mtu anaenda Msikitini au Kanisani kwa hiyo inahitaji uadilifu wa hali juu sana. Sio wote, lakini kuna baadhi ya madaktari na manesi hawana uadilifu, na mwisho wa siku wanatuchonganisha sisi Serikali na wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ya kwangu ni hayo. Ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Wageni waliopo Bunge jioni hii, Wageni wa Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, Waziri wa

Afya, Ndugu Durania Sebali, ni rafiki wa Mheshimiwa Waziri, karibu. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Mchengerwa, watalamu wa afya kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili; Taasisi ya Mifupa Muhimbili *(MOI);* Taasisi ya Utafiti wa Dawa za Binadamu *(NIMR);* Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya; Hospitali ya Benjamini Mkapa; Taasisi ya Saratani *Ocean Road;* Hospitali ya Kanda Bugando; Hospitali ya Kanda *(KCMC);* na Hospitali Maalum ya Taifa Kibong'oto. Karibuni sana na hongereni kwa kazi nzuri mnazofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Devotha, jiandae Mheshimiwa Naibu Waziri.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Ninamshukuru Mungu kwa afya na uzima. Ninaomba nitoe mchango wangu katika hii Wizara ya Afya. Nami niungane na walio wengi kupongeza juhudi za Waziri katika hii Wizara ya Afya na Naibu Waziri wake. Kwa muda mfupi ambao wameingia kwenye Wizara hii wameonyesha uwezo mkubwa. Ninaomba niwapongeze kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Watanzania wanasubiri kuona imani ambayo wanayo juu yao kuona ni namna gani watapambana kuhakikisha kwamba wanapunguza gharama za matibabu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuja na Sera ya Bima ya Afya Wote. Kwa kaya yenye watu sita, ni shilingi 150,000. Ziko Kaya masikini ambazo hazina uwezo kabisa wa kumudu shilingi 150,000.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri waangalie namna Serikali itakavyosaidia kaya hizi. Wako watu ambao 150,000 kwao hawajawahi kuiona. Waende vijijini wataona. Wabunge tuko hapa, kuna watu ambao hata 50,000 hawajawahi kuiona, maisha ni magumu. Mtu kama huyu 150,000 kwa ajili ya bima ya afya hataweza. Tuwatambue ili Serikali iweze kuwasaidia watu hawa, washirikishwe, waingie kwenye bima ya afya ili wasaidiwe na Serikali.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nizungumze. Nimesikia kuhusu upanuzi wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, sijasikia kuhusu upanuzi wa Hospitali ya *Ocean Road*. Watanzania zaidi ya 5,000 na kuendelea wanaingia ndani ya Hospitali ya *Ocean Road* ili kupata matibabu. Ugonjwa wa saratani hivi sasa mpaka watoto wadogo wanapa, na kwa bahati mbaya ni magonjwa ambayo mengine ni ya kurithi.

Mheshimiwa Spika, Serikali ifanye kitu *Ocean Road*. Mgonjwa mmoja wa *chemotherapy* kupata matibabu yake dripu moja ni shilingi 10,000,000, shilingi 20,000,000, shilingi 30,000,000 na kuendelea. Je, Mtanzania wa kawaida anaweza? Kama Serikali imeweza kutoa ruzuku kwenye mbolea, dizeli na petroli, Serikali ione namna gani itawasaidia wagonjwa wa saratani waweze kupata matibabu bure.

Mheshimiwa Spika, linguine, Hospitali ya *Ocean Road* ni ya zamani, ina vitanda 200 na havitoshelezi kabisa. Wagonjwa wengi wanalazimika kuondoka kwa sababu hakuna sehemu ya kulazwa. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri, kwa nini kama Muhimbili ...

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, taarifa, taarifa.

**SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninaheshimu sana mchango wa dada yangu anayechangia na ninampenda sana dada yangu Mheshimiwa Devotha, ila ninatambua anachojaribu kusisitiza. Niseme tu, kwenye eneo la bima na watu wasiojiweza tayari Serikali imetengeneza mkakati na ilishatenga hela kwa ajili ya kuhudumia eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, labda tuseme ni kwa kiwango gani? Kama watapatikana wote hilo ni jambo lingine, lakini ukienda kwenye Hospitali yetu ya *Ocean Road*, leo Hospitali yetu ya *Ocean Road* imefanyiwa kazi kubwa, imewekwa vifaa vikubwa ambavyo leo

imekuwa ni kitivo cha rufaa kwa nchi za Afrika Mashariki na Kati kwa *investment* iliyofanyika pale.

**SPIKA:** Mheshimiwa taarifa hutakiwi kuchangia.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, dada yangu ninatambua mchango wake, lakini nilisema tu nimwongezee hayo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mollel, taarifa ina utaratibu wake. Mheshimiwa Devotha unapokea taarifa? *(Makofi)*

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Spika, nimemsikia lakini ninachosema, kupanga ni jambo lingine kutekeleza ni jambo lingine pia. Tunachosubiri na Watanzania wanachokisubiri ni kuona ni namna gani Serikali inasaidia kaya hizi maskini na zenyewe zinufaike na bima ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa ninazungumza suala la *Ocean Road*. Tumesikia Serikali ina mpango wa kuboresha Hospitali ya Muhimbili. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri waone ni namna gani wataboresha na kusaidia Hospitali ya *Ocean Road*. Wagonjwa zaidi ya 5,000 na kuendelea kila mwaka wanatibiwa pale *Ocean Road*. Mheshimiwa Waziri, kwa nini asiache *legacy*? Kwa nini asifunge macho Hospitali ya Muhimbili inaenda kutanuliwa, tayari pale kuna Hospitali ya Jakaya Kikwete, kuna Hospitali ya *MOI*, kwa nini Mloganzila isitumike wakawapa *Ocean Road* ambao hawana eneo wakafanya huduma zote pale za upasuaji, vipimo, *chemotherapy*, mionzi na huduma zote zikaenda Mloganzila?

Mheshimiwa Spika, ninamshauri Mheshimiwa Waziri, aone namna gani wataisaidia *Ocean Road*. Tuna wagonjwa wengi wa *cancer* na kupitia utaratibu huo wa kuipa fursa *Ocean Road*, nchi nyingine zozote zilizoendelea zina *Cancer Institute* ambazo zina mashine za kutosha zinafanya kila kitu wenyewe. *Ocean Road* wanategemea *operations* zikafanyike Muhimbili. Kwa nini tusiwe na kitengo ambacho kinajitegemea na kufanya huduma zote? kwa usikivu wa Mheshimiwa

Waziri ninaoujua ninamwomba muitazame *Ocean Road* kwa jicho la pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matibabu ya saratani ni ya bei kubwa mno. Watanzania hawawezi kumudu. Kama kweli tumeweza kutoa gharama kwenye petroli na dizeli, basi tuondoe gharama za matibabu ya *cancer* kwa watu wanaoumwa ...

**SPIKA:** Mheshimiwa Devotha, muda wako umekwisha. Malizia, halafu unga mkono hoja.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Spika, ninamalizia kwa kuomba Serikali iondoe gharama za matibabu kwa wagonjwa wa *cancer*. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Awali ya yote, niunge mkono hoja. Pia ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama leo katika Bunge lako Tukufu ili niweze kuchangia hoja tuliyonayo mezani ya Wizara ya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa imani kubwa aliyoweka kwangu kuniteua ili niweze kumsaidia katika nafasi hii ya Unaibu Waziri wa Afya. Ninamwahidi Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwamba, nitaitumikia nafasi hii kwa unyenyekevu mkubwa, kwa heshima kubwa. Nitajituma ili kuhakikisha kwamba ninaweza kutimiza yale maono. Imani aliyoiweka kwangu nitailipa kwa imani kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Makamu wa Rais kwa kuteuliwa kutumikia nafasi hiyo ili kuweza kumsaidia Mheshimiwa Rais kwenye nafasi hiyo ya Umakamu wa Rais.

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri na kubwa anayofanya. Wote tumeona jinsi

gani anafanya ili kumsaidia Rais katika nchi yetu. Ziara anazofanya, jinsi anavyosikiliza wananchi katika hoja zao na shida zao. Ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Afya Mohamed Mchengerwa, mtu kazi. Ninasikia fahari, ninasikia furaha kufanya kazi na Mheshimiwa Waziri. Miongozo yake maelekezo yake, lakini msimamo wake wa kuhitaji matokeo kwanza ananipa hamasa na tija ya kuendelea kutumika zaidi. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakupongeza wewe kwa kuchaguliwa kuliongoza Bunge hili Tukufu, Naibu Spika lakini na Wenyeviti wote wa Bunge, kwa jinsi ambavyo mnaliendesha Bunge hili kisasa kabisa. Hongereni sana ninawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza pia watumishi wote wa Wizara ya Afya wakiongozwa na Katibu Mkuu Dkt. Seif Shekalaghe, Naibu Makatibu Wakuu, *CMO*, Wakurugenzi wote wa taasisi, lakini na watumishi wote wa afya katika nchi hii. Ukiwa na maumivu au ukiwa unaumwa huwezi kupata furaha. Ninawahakikishia watumishi wote wa afya, kazi yao ya wito watalipwa na Mungu. Waendelee kuchapa kazi kwa bidii kubwa sana, sisi tunawategemea sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shukrani na pongezi zote tulizopewa humu zinawastahili wao watumishi wa afya, kwa sababu pale ambapo wananchi wanahitaji shida yoyote, tukiwaomba wanaitekeleza kwa wakati. Kwa hiyo, watumishi wote wa afya nchi nzima wanastahili pongezi hizo na shukrani na waendelee kuchapa kazi ili ile azma ya Mheshimiwa Rais aliyoisema ya kuacha tabasamu kwa Watanzania pindi atakapoondoka mwaka 2030 iweze kufikia. Huwezi kupata tabasamu ukiwa na maumivu.

Mheshimiwa Spika, ninakishukuru sana Chama changu Cha Mapinduzi kwa kuniteua niweze kupeperusha bendera katika nafasi hii, lakini kipekee wananchi wa Jimbo la Muhambwe ambao wameendelea kuniamini kwa awamu nyingine hii ya pili.

Ninawahakikishia wananchi wa Muhambwe kwamba niko *gado* niko na nguvu zangu kabisa za kuwatumikia kuliko mwanzo. Nitasimamia yale tuliyokubaliana ili tuweze kuyatekeleza Muhambwe kwa ajili ya maendeleo, tuweze kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru pia wasaidizi wangu wote wanaonisaidia, Katibu wangu Juliana, dereva na wasaidizi wote. Wao wamesababisha kazi yangu iwe rahisi kwa kunisaidia kwa karibu sana. Ninawashukuru sana na Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho siyo kwa umuhimu, familia yangu ikiongozwa na mume wangu Sadock Mugendi na watoto wangu, kwa ushirikiano wanaonipa, upendo wanaonipa na maombi yao yamenifanya niendelee kufanya kazi zaidi na wakati wote nisikie kama sijachoka, ili niweze kutimiza majukumu yangu. Waendelee kuniombea na kunivumilia. Nipo kazini ninachapa kazi kutimiza maono ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitajikita sasa kwenye kuchangia baadhi ya hoja, lakini hata hivyo ninaendelea kuishukuru Kamati yetu ya Bunge kwa michango yao na hoja zao wanazotupatia kwenye Kamati. Zinaendelea kutuimarisha na kuona wapi tuongeze bidii. Kwa heshima na unyenyekevu mkubwa sana, michango yote ya Waheshimiwa Wabunge tumeipokea kwa umuhimu wake mkubwa na tunawathibitishia, hata kama hoja haijajibiwa hapa leo, ninaomba niwahakikishie tumeziandika hoja zote na changamoto zenu, kwa sababu michango yao inawakilisha Watanzania wote. Tutaifanyia kazi kwa umuhimu wake mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, basi nijielekeze kwenye hoja chache. Hoja ya kwanza ni huduma za mama na mtoto ambao Wabunge wangu wamechangia. Hapa kipekee ninamshukuru Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye kwa kweli yeye ndiye kinara wa kupunguza vifo vya mama na mtoto katika nchi hii. Tumejionea akiendelea kupewa tuzo, akiendelea kutunukiwa tuzo mbalimbali kwa sababu ya jinsi ambavyo ameamua kwa dhati kabisa kupunguza vifo vya mama na mtoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sikusudii kurejea takwimu kwa sababu wengi wamezitaja, isipokuwa nitaenda kwenye hoja ya ombi la mama kujifungua kwa staha, lakini na kuwa na mwambata. Waheshimiwa Wabunge ninaomba niwathibitishie tumeshalifanyia kazi jambo hili. Kati ya vituo 8,019, tayari vituo vyetu 1,244 vinatoa huduma hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea kuhakikisha kwamba vituo vyote viweze kutoa huduma kwa sababu kwa mujibu wa takwimu za *WHO* zinaonyesha kwamba, pale mama anapokuwa na mwambata basi mambo mengi yanakwenda vizuri zaidi. Kwa hiyo, ninawathibitishia tunalifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wamechangia jinsi gani hatujafanya vizuri kupunguza vifo vya watoto wachanga ambao tumepunguza kwa *digit* moja kutoka vifo 25 katika vizazi hai 1,000 mpaka vifo 24 kwenye vizazi hai 1,000. Ni kweli, lakini ninawahakikishia Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshaliona hilo na pale 2018 *WHO* walipoleta tathmini na kusema ni lazima tuwe na vyumba au wodi kwa ajili ya kuhifadhi watoto wachanga waliozaliwa chini ya uzito pungufu, kwa maana ya njiti.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 2018 tulipoanza tulikuwa na vyumba 14 nchi nzima ambavyo vinaweza kutunza watoto wachanga. Leo hii tuna vyumba 438 nchi nzima. Huu ni uwekezaji mkubwa uliofanywa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenye kipindi hiki cha Awamu ya Sita ili kuhakikisha kwamba watoto wachanga wanakuwa salama hata kama watazaliwa na uzito pungufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hajaishia hapo, mwaka huu 2026 tunajenga vituo 37 na kwa ubora zaidi vituo hivi navyo vimeboreshwa. Kwa mujibu wa utafiti wa *WHO* imeonyesha kwamba, mama anapojifungua mtoto ambaye ana uzito pungufu na akatengwa kuishi na mtoto wake, basi *chance* ya mtoto kufariki ni kubwa kuliko akiwa na mama yake. Akina mama wengi wanaojifungua watoto njiti

wanapata sonona *(depression)* pale unapomtenga yeye na mtoto wake.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo mwongozo wa *WHO* ni mama anapojifungua mtoto chini ya uzito akae na mtoto wake. Kwa hivyo, vituo hivi 37 vimezingatia vigezo hivyo. Vinajengwa nchi nzima vituo 37 kwenye hatua mbalimbali. Vituo 17 kwenye hospitali za mikoa, lakini vituo 20 viko kwenye hospitali ngazi ya halmashauri.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji huu unaendana na uwekezaji wa vifaa kwa maana ya *Radiator Warmer*, kwa ajili mtoto anahitaji joto, *CPAP* na Oxygen *Concentrator* kwa sababu mtoto anahitaji oksijeni. Lakini *Phototherapy* kwa sababu watoto wengi wanatengeneza manjano ili waweze kupata matibabu.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji huu utapelekea tupunguze vifo vya mtoto mchanga kwa 50% na tutafikia vifo 12 kama ambavyo malengo ya maendeleo endelevu yanataka, kwa maana ya *SDGs*. Tukipunguza kwa 50% ninaomba niwathibitishie Waheshimiwa Wabunge, tutapunguza vifo vya watoto chini ya miaka mitano kwa sababu kwa sasa tuna vifo 43 kati ya vizazi hai 1,000. Hata hivyo, tafiti zinaonyesha kwamba vifo hivi vinasababishwa na vifo vya watoto wachanga, kwa maana ya 0 – 28. Kwa hiyo, uwekezaji huu wa vyumba au wodi za watoto wachanga utapunguza vifo vya watoto chini ya miaka mitano kwa 50%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tutakwenda kufikia lengo la *SDGs* la kuwa na vifo 25 kwa vizazi hai 1,000 vya watoto *under five*. Ujenzi huu unaendelea mahali tofauti tofauti Waheshimiwa Wabunge, wakienda kwenye majimbo yao watajionea.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wengi wamechangia kuhusu huduma ya dharura. Huduma ya dharura ni huduma mgonjwa anayoipata ndani ya saa moja, tunaita *Golden Hour*. Hii ni saa ambayo mgonjwa akipata huduma, basi umeokoa maisha yake kwa 60%. Kumtoa kwenye eneo la dharura, kumpa oksijeni, kumpa maji na

kumpa huduma zote za msingi anazotakiwa mgonjwa kuzipata kwa dharura.

Mheshimiwa Spika, tumefanya nini? Mwaka 2021 tulikuwa na vyumba au wodi za dharura saba tu nchi hii. Leo tunavyoongea tunazo 125. Serikali ya Awamu ya Sita imeamua kuokoa maisha ya Watanzania ndani ya *Golden Hour* waweze kupata huduma muhimu. Nimewasikia Waheshimiwa Wabunge wengi wakisema jinsi gani huduma za dharura zinapatikana pale pale mapokezi anapokuwa sawa ndiyo anajulikana aende wodi gani. Hii itakwenda kuokoa maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hiyo, tumeongeza magari ya dharura *(ambulance)*. Mwaka 2021 tulikuwa na magari 540. Hadi Machi, 2026 tunayo magari 1,267. Ikiwa hiyo haitoshi, tumenunua boti saba kwa ajili ya maeneo ya majini ambazo zimepelekwa kwenye maeneo tofauti tofauti ili nao waweze kupata huduma za dharura kupitia boti.

Mheshimiwa Spika, mwisho, tumetoa pikipiki 300 nchi nzima kwenye halmashauri ambazo zinaenda kutoa huduma za chanjo nchi nzima ili Watanzania waweze kupata huduma bora.

Mheshimiwa Spika, wako Wabunge wengi pia wamechangia hoja ya rasilimali watu. Ni ukweli usiopingika huwezi kutoa huduma bila kuwa na rasilimali watu, lakini hapa ninampongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye kuanzia mwaka 2021, mpaka leo ameajiri watumishi wa Sekta ya Afya 53,633. Hii ikiwemo watumishi 5,000 ambao wameajiriwa mwezi Januari kupelekea ahadi yake aliyotoa wakati wa kampeni.

Mheshimiwa Spika, hivyo sasa, tunao watumishi wa Sekta ya Afya nchi nzima 182,430. Tunaendelea kuongeza watumishi hawa hasa mabingwa na bingwa bobezi. Kupitia *Samia Health Super Specialization*, wako watumishi 1,483 wanaosoma ndani ya nchi na nje ya nchi ambao wanasoma kwa ajili tuendelee kupata watumishi mabingwa.

Mheshimiwa Spika, kumtengeneza Daktari Bingwa Bobezi inachukua zaidi ya miaka 10 mpaka 14. Kwa hiyo, Wabunge wanaweza wakaona siyo rahisi sana kuwapata, lakini Serikali imeamua kwa dhati kuhakikisha kwamba tunawapata watumishi wao. Hata hivyo, tunaendelea kuwaomba viongozi wetu Wakurugenzi wa Halmashauri waendelee kuwaruhusu watumishi wanaotaka kujiendeleza katika fani mbalimbali ili tuweze kupata watumishi wa kutosha kwenye hospitali zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunao mpango wa kufanya msawazo kwa ajili ya hospitali za kanda ambazo zimeonekana bado zinatoa huduma chache za kibingwa, ikiwemo Hospitali ya Lindi ambayo bado inatoa huduma tatu, Hospitali ya Sumbawanga inatoa huduma tano na Hospitali ya Tabora inatoa huduma sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba tuwaahidi Waheshimiwa Wabunge, tulikuwa na mpango huo, kwa hivyo tutafanya msawazo ili tukabiliane na hiyo changamoto. Kwa sababu, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alituelekeza wakati akihutubia Bunge, kwamba tuongeze huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kwamba, hapo awali nchi hii ilikuwa na huduma nne tu, lakini sasa Wizara ya Afya tumejipanga chini ya Waziri wetu, mtu kazi na tumeshatoa mwongozo kutoka huduma nane mpaka 17. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge ninawathibitishia kwamba tupo kazini kuhakikisha kwamba huduma hizi zinafika kote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutaenda mbali zaidi, kwenye hospitali za halmashauri tunataka wawe na huduma tano. Lengo ikiwa ni kwamba huduma za kibingwa ziweze kupatikana kuanzia katika ngazi ya halmashauri. Kwa hivyo, tunaendelea kujipanga kuhakikisha tunatimiza malengo na maono ya Mheshimiwa Rais ambaye amekusudia tupeleke huduma za kibingwa kwa Watanzania ili tupeleke huduma kwa Mtanzania. Amesema Watanzania wasizifuate huduma, bali huduma ziwafuate Watanzania. Kwa hivyo, kwa kufanya

hivyo madaktari hao bingwa watakwenda kuwahudumia Watanzania kule walipo kuanzia kwenye ngazi ya halmashauri.

Mheshimiwa Spika, ili uweze kutoa huduma za kibingwa unahitaji mambo kama matatu au manne. Kama nilivyoanza kueleza, unahitaji rasilimali watu wenye weledi wa kufanya kazi, unahitaji miundombinu yenye uwezo wa kuwezesha hiyo huduma ifanyike na unahitaji wataalam...

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, malizia.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, unahitaji wataalam wenye huduma bobezi.

Mheshimiwa Spika, tumeendelea kuboresha huduma za miundombinu kwenye hospitali zote za rufaa, hospitali maalum na hospitali za mikoa. Waheshimiwa Wabunge, ninaomba niwathibitishie, hata kama hapa haujatajwa, lakini ninaomba niwaambie kila mkoa una kitu umepata.

Mheshimiwa Spika, nimepanga kwa mikoa michache hapa niwaelezee, lakini kwa sababu ya muda ninaomba waridhie niseme michache. Kwanza tuna Hospitali ya Mkoa ya Kitete ambao umepangiwa shilingi bilioni 4.5 kwa sababu ya jengo la watoto wachanga, lakini tuna shilingi bilioni 3,000,000,000 kwa sababu ya kumalizia jengo la mama na mtoto. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Tabora tumewasikia na tumelifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunayo Hospitali ya Rukwa, tunayo shilingi bilioni 2.1 ambayo shilingi bilioni moja inakamilisha jengo la damu salama na shilingi bilioni 1.5 unaanzisha jengo la hospitali mpya. Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Rukwa tunakwenda kutekeleza hiyo miradi. Rukwa wanayo shilingi 542,000,000 ambayo tunaenda kuanzisha huduma ya *Dialysis*, itanunua mashine na itafanya ukarabati wa chumba. Tunayo pia shilingi bilioni 4.7 ambayo inakwenda kujenga

jengo la taaluma kwenye Chuo cha Afya kilichopo Sumbawanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Dodoma tunayo shilingi bilioni 4.7 kwa sababu ya jengo la watoto wachanga, lakini tunayo shilingi 7,000,000,000 kwa ajili ya Benjamini Mkapa kwa ajili ya kuendeleza huduma za upandikizaji figo. Tunayo shilingi 2,000,000,000 kwa sababu ya Hospitali ya Mirembe.

Mheshimiwa Spika, tunayo shilingi bilioni 4.7 kwa sababu ya jengo la taaluma katika Chuo cha Mpwapwa; Hospitali ya Mara, hospitali ya kumbukumbu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, maelekezo ya kiti muda wako umekwisha.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa, ninaomba Wabunge waridhie kwamba tupo hapa na nitawasikiliza na kuwaonesha nini wamepangiwa kwenye mikoa yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi na ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante na hongera. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kuchukua fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Afya kwa kuzungumza na kwa maandishi. Kwa niaba ya Wizara ana Sekta ya Afya tumepokea maoni, tumepokea ushauri na tumepokea hoja za Waheshimiwa Wabunge kwa unyenyekevu mkubwa na kwa dhamira ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, michango iliyotolewa hapa ni michango takribani ya Wabunge 59, lakini nimeshuhudia namna ambavyo kila Mbunge alitamani kuzungumza kwa niaba ya wananchi wake. Hakika Wabunge wa Bunge hili wamedhamiria kwa dhati kabisa kusimamia wananchi waliowaleta hapa Bungeni, ninawapongeza sana sana Waheshimiwa Wabunge kwa kazi kubwa na kazi nzuri hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa ufafanuzi wa hoja za Kamati ya Kudumu ya Afya na Masuala ya UKIMWI, pamoja na hoja za Waheshimiwa Wabunge, ninapenda niwatambue Waheshimiwa wote waliochangia; Wabunge 59 waliochangia hotuba yangu na kati ya Wabunge hao Waheshimiwa Wabunge 50 wamechangia kwa kuzungumza na Waheshimiwa Wabunge wanne wamechangia kwa maandishi akiwemo Mheshimiwa Thomas Kampala Maganga.

Mheshimiwa Spika, nimthibitishie kwamba kwa hoja alizozitoa Wizara ya Afya itashirikiana na Wizara ya Ujenzi ili kusudi tuweze kuona ni namna gani tunaweza tukatengeneza njia nyingine ya kuunganisha kutoka pale Daraja la Jangwani kuelekea katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili. Tumepokea hoja hii kwa mikono miwili kabisa.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja za Wizara wamewasilisha maoni, lakini wamewasilisha ushauri na hoja zilizojikita katika maeneo makubwa tisa; eneo la Bima ya Afya kwa wote, Wabunge zaidi ya 16 wamechangia kuhusu Bima ya Afya kwa Wote, wakiwawakilisha wananchi wao katika maeneo yao ambapo Waheshimiwa hawa Wabunge na wawakilishi wa wananchi wanatoka.

Mheshimiwa Spika, ipo miundombinu ya kutolea huduma ya afya; Wabunge zaidi ya 38 wamezungumzia kuhusu miundombinu, kuhusu ujenzi wa hospitali, lakini wapo waliopongeza kazi kubwa iliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita katika kipindi hiki cha Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi ndani ya Serikali tunatambua kwamba Mheshimiwa Dkt. Samia, atakumbukwa na huu ndiyo ukweli. Inawezekana wapo Watanzania wasiotamani kusikia maneno haya, lakini tunawaambia ukweli, toka Taifa hili lipate uhuru vituo vya afya vilikuwa ni 7,000 tu vya Serikali, lakini Mheshimiwa Dkt. Samia, katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wake amejenga vituo vya afya 3,530. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maono haya tunakiri kabisa kwamba dhamira ya Baba wa Taifa katika ndoto dhidi ya ujinga, umaskini na maradhi. Kama Baba wa Taifa angekuwa hai leo, yeye mwenyewe angekuwa ni shuhuda wa kazi kubwa iliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi hii ni nchi inayobeba misingi ya ujamaa na huo ndiyo ukweli. Nchi hii inabeba misingi ya ujamaa na tunaweza kwa namna moja au nyingine tukawa tume-*overlap* au bado tupo nyuma, lakini ukweli ni kwamba Taifa hili ni Taifa ambalo viongozi lazima tujitoe tufanye kazi kwa bidii kwa ajili ya wananchi, lazima tujitoe. Kwa hiyo, ukiangalia takwimu, Watanzania watamkumbuka Mheshimiwa Rais Samia, kwa kazi kubwa aliyoifanya kwa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunasema nchi hii ni nchi ya kijamaa. Nchi hii ni nchi ya kusaidiana, nchi hii ni nchi ya kutegemeana, nchi hii imebeba misingi ambayo sisi viongozi wa kuteuliwa ni lazima tufanye kazi kwa bidii. Hakuna neno lingine, hakuna neno linguine, tunapofanya kazi kwa bidii tukakusanya kodi itasaidia Taifa letu kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine Waheshimiwa Wabunge wanabeba ajenda za wananchi, wanakuja hapa Bungeni wanazungumza kuhusu kero zinazowakabili wananchi na sisi ndani ya Serikali tunaziona kabisa kero hizi zina mantiki na pengine tunasema tumechelewa sana kutekeleza au kwenda kuwasaidia wananchi katika maeneo ambapo Waheshimiwa Wabunge wanatoka katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, haikubaliki hata kidogo, haiwezekani Mkoa kama Shinyanga ambao kuna wadau wa maendeleo, ambao kuna wadau wa madini, leo hii tunalia kwamba tunahitaji shilingi 200,000,000 ya kutengeneza chumba cha *Dialysis* na viongozi wa mkoa pale wapo, Mganga Mkuu wa Mkoa pale wapo, tuna wadau wa maendeleo pale wapo, zipo benki. Tunajiuliza wakati mwingine ni lazima tuwajibike, tuziangalie kero za wananchi kama kero zetu sisi wenyewe viongozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi kweli leo hii Mkoa kama wa Shinyanga wanasubiri bajeti ya mwaka ujao wa fedha kuomba shilingi 200,000,000 au 300,000,000 kuokoa maisha ya Watanzania ambao figo zimefeli na pale kuna viongozi, hii haikubaliki. Ninawaambia ninawapa mwezi mmoja watu wa Shinyanga, kwa sababu Mheshimiwa Mbunge amezungumza hapa haikubaliki, haikubaliki hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, nchi hii ni ya kijamaa ni lazima tujipange, tujikusanye sisi wenyewe tutafute fedha. Mwalimu Nyerere alikwisha sema Taifa hili haliwezi kuendelea bila kushirikisha wadau wa maendeleo, si maneno yangu ni ya Mwalimu Nyerere. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tunakaa kujadili shilingi 200,000,000 kuokoa maisha ya wananchi ambao figo zimefeli na pale kuna viongozi wa mkoa, tuna madini pale, tuna wadau wa madini, tunashindwa kama mkoa hata kuhitisha harambee tukawaomba wadau mabenki ambayo yamekuwa yakifanya kazi ya kusaidia kujenga majengo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati wangu, viongozi wa Wizara ni lazima wajipange, kweli kweli sitakubali, hili ninalisema wazi sitakubali. Ninatoa mwezi mmoja katika maeneo haya, wakishindwa kujipanga nitawaweka kando, nitawaweka kando. Mganga Mkuu wa Mkoa wa Rufaa yeye na timu yake, haiwezekani Watanzania waendelee kufa tunasubiri Bunge lijalo kujadili maombi ya shilingi 200,000,000 ambayo hata wadau wa maendeleo tukiwaomba wanaweza kutupatia hizo fedha. Hii haikubaliki na wakati wangu siwezi kuiruhusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesema hapa nchi hii ni nchi ya kijamaa. Yapo mambo ndani ya Wizara yanatokea ambayo wakati mwingine hayapo hata kwenye bajeti na ndiyo maana tumekuwa tukisisitiza sana sana kwa Watanzania tuwape viongozi nafasi ya kutusaidia kama Taifa. Tusiwa-*frustrate* viongozi wetu wa kitaifa, kwa sababu kwa takwimu za Wizara ya Afya, Watanzania zaidi ya 40,000,000 walifika kwenye vituo vyetu vya afya na hospitali mbalimbali nchini, zaidi ya Watanzania 40,000,000 kwa mujibu wa takwimu.

Mheshimiwa Spika, kama wewe hukwenda hospitali yupo ndugu yako aliyekwenda hospitali na Watanzania hawawezi gharama za hospitali, ni kubwa sana hawawezi. Ninatoa takwimu ya haraka, takwimu ya haraka kabisa; kwa mwaka huu peke yake *JKCI* wametoa msamaha kwa Watanzania waliokwenda pale hospitali, msamaha wenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 1.9 kwa wenye changamoto za moyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni Taifa gani ambalo linaweza kutoa msamaha wa aina hii ndani ya Afrika Mashariki, ndani ya Afrika tujiulize Taifa lipi tukafanye tafiti. *Ocean Road* Taasisi ya *Cancer* ambayo Mheshimiwa Devota ameizungumza hapa. Kwa mwaka huu peke yake mpaka hapa niliposimama wametoa msamaha wa zaidi ya shilingi 12,000,000,000, *Ocean Road*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda pale *MOI* msamaha wa matibabu zaidi ya shilingi 7,000,000,000; ukija Muhimbili Mloganzila msamaha wa Watanzania waliokwenda. Kwa sababu hatuwezi kuwaacha Watanzania wanakufa tukasema eti walipe fedha, haiwezekani na ndiyo maana kwenye kila kituo chetu cha afya, kwenye kila zahanati, kwenye kila hospitali zetu zote tumeweka wataalam wa ustawi wa jamii. Huduma za afya ni gharama kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda Muhimbili; ninaomba nikutaarifu, msamaha wa Watanzania waliosamehewa ni zaidi ya shilingi 19,000,000,000, msamaha na hii haipo kwenye bajeti yoyote, haipo kwenye bajeti yoyote. Ukienda *KCMC* zaidi ya shilingi 6,000,000,000,

ukienda Benjamini Mkapa zaidi ya shilingi 4,000,000,000. Tunazungumzia karibu shilingi 60,000,000,000 mpaka 70,000,000,000 ya msamaha.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana tunasema viongozi wetu wanahitaji utulivu, fedha hizi zinatoka wapi, hazipo kwenye bajeti. Wakati mwingine hospitali hizi zinatamani kufanya mambo makubwa, lakini itafanyaje hayo mambo makubwa? Kwa sababu Watanzania wanaingia kwenye misamaha.

Mheshimiwa Spika, haiwezekani mgonjwa yupo kitandani, yupo katika hali mbaya ukamwacha kumhudumia na hana fedha, tunafanyaje. Kwa hiyo, niseme tu kwa uwazi, Watanzania wanahitaji kuendelea kuwaombea viongozi wetu wa kitaifa kwa sababu misamaha hii inatoka kwao. Niendelee kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kazi kubwa ambayo wanaendelea kuifanya kwa niaba ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge 18 walizungumzia kuhusu dawa na vifaatiba na Wabunge 12 wamezungumzia kuhusu huduma za kinga ikiwemo chanjo, mifumo ya TEHAMA, *MSD*, sera ya afya na Taasisi ya *TMDA* pamoja na *TBS*. Kwa upande wa kikanda; idadi ya Waheshimiwa Wabunge waliochangia ni kama ifuatavyo: Kanda ya Kati Wabunge saba, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Wabunge saba, Kanda ya Ziwa Wabunge 11, Kanda ya Kaskazini Wabunge wa nne, Kanda ya Magharibi Wabunge tisa, Kanda ya Mashariki Wabunge tisa, Kanda ya Kusini Wabunge wa nne na Zanzibar Wabunge wa tatu.

Mheshimiwa Spika, michango iliyotolewa ina ujumbe mmoja mkubwa kwamba, ujumbe wa uboreshaji wa huduma za afya. Wananchi wanataka huduma ziwe karibu, wananchi wanataka dawa na wananchi wanataka watumishi katika maeneo mbalimbali ya vituo, hospitali, zahanati na hospitali za kanda ziwe na vipimo, ziwe na mifumo inayosomana na ziweze kugharamiwa bila kuangusha kaya katika umasikini.

Mheshimiwa Spika, majibu yangu yatazingatia maeneo ya Bima ya Afya kwa wote, dawa na *MSD*, TEHAMA, miundombinu na rasilimali watu, ushirikiano wa sekta binafsi, kinga, sera, taasisi na mwongozo wa bei elekezi ya matibabu, Bima ya Afya kwa wote na ulinzi wa makundi maalumu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imepokea hoja kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, utekelezaji wa sheria hii ulianza rasmi tarehe 26 Januari, 2026. Baada ya kutangazwa kuanza kutumika kwa kitita cha mafao ya huduma muhimu. Awamu ya kwanza imeanza kwa wananchi wasio na uwezo wanaogharamiwa na Serikali. hadi tarehe 16 Aprili, 2026 kaya 172,297 zimefikiwa na wananchi, 463,228 wamesajiliwa katika awamu ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utambuzi wa kaya zisizo na uwezo, Tanzania Bara ina kaya 3,917,457 zisizo na uwezo kwa mujibu wa takwimu za *NBS*. Hadi sasa kaya 900,228 zimetambuliwa katika Mwaka wa Fedha 2026/2027. Serikali imekamilisha utambuzi wa kaya zilizobaki na inaendelea kuchambua vyanzo vipya fedha ikiwemo kodi ya bidhaa za tumbaku, tozo kwenye bima ya vyombo vya moto na mapendekezo ya miamala yaliyotolewa na Mheshimiwa Kingu, tutakwenda kuyafanyia kazi na tayari tumekwishakutana na wadau hawa na tunaamini wenzetu wa Wizara ya Fedha tutazungumza nao, tutakaa nao.

Mheshimiwa Spika, imani yangu kwa namna nilipokutana na wadau hawa, kama tutakwenda kutekeleza namna ambavyo Mheshimiwa Elibariki Kingu, alivyoshauri, basi inawezekana kabisa kama makusanyo ambayo Mheshimiwa Kingu ameshauri na kwa namna ambavyo mimi mwenyewe nimekutana na wadau hawa, tukifanikiwa kulitekeleza hili pengine tutamshauri Mheshimiwa Rais kwa mwakani, Watanzania wasichange hata senti tano kwa sababu tutakuwa na fedha za kutosha kuhudumia Bima ya Afya kwa wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili ninaomba nimthibitishie kwamba tumelibeba na tutakwenda kulifanyia kazi. Serikali pia

imepokea hoja kuhusu huduma bila malipo kwa watoto chini ya miaka mitano na wazee wenye zaidi ya miaka 60. Sera hii inaendelea kutekelezwa ili haki iweze kuwa ni endelevu, makundi haya yanaingizwa kwa awamu katika Bima ya Afya kwa wote ili huduma ipatikane kupitia mfumo unaolipika, unaofuatilia na unaodumu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Bima ya Afya kwa Waheshimiwa Wabunge, utoaji wa bima hiyo unasimamiwa kwa mujibu wa kifungu cha 24 cha Sheria ya *National Assembly Administration Act*, Sura 115. Kupitia sheria hii Bunge huingia makubaliano maalum na *NHIF* ili kutoa huduma za Bima ya Afya kwa Waheshimiwa Wabunge na wategemezi wao kupitia zabuni.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa mujibu wa Sheria ya *NHIF* na Bima ya Afya kwa wote, fao la wazazi linalowahusu watumishi wa umma na sekta rasmi na binafsi hutolewa kwa utaratibu wa kuchangia asilimia sita ya mshahara kila mwezi, asilimia tatu kutoka kwa mwajiri na asilimia tatu kutoka kwa mtumishi. Kwa msingi huo utaratibu uliopo kwa Waheshimiwa Wabunge, haujumuishi wazazi kama Kundi la wategemezi ndani ya bima hiyo maalum.

Mheshimiwa Spika, dawa *MSD*, *EP-prescription* na bei elekezi za matibabu. Serikali inatambua hoja za Waheshimiwa Wabunge kuhusu dawa, vifaatiba, *form II C, prescription* zinazotumika nje ya vituo na ushiriki wa *community pharmacies*. Dhamira yetu ni kuhakikisha takwimu na uhalisia wa magonjwa vinakutana.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza mchakato wa kuanzisha *EP-prescription*. Mfumo huu utamwezesha mtoa huduma kuona dawa ilipo kituoni kwa wakati halisi, kuandika dawa kwa *generic name* na kwa kuzingatia miongozo ya tiba.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa na changamoto, wapo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wao wamekuwa wakinifikia, wakilalamika baadhi ya vituo vyao kukosa dawa. Ukweli ni kwamba kumekuwa na changamoto, baadhi ya madaktari katika baadhi ya maeneo wamekuwa wakiandika dawa kutumia mifumo ya *generic name* na

wakati mwingine dawa zinakuwepo kwenye vituo lakini wanaandika dawa nyingine wakijua kabisa kwamba dawa ya kutibu ugonjwa husika ipo kwenye kituo. Sasa haya wakati mwingine yanafanywa kwa makusudi, pengine wakishirikiana na baadhi ya watu, pengine wadau walioleta hizo dawa ambazo wao wanataka kwenda kuzitoa.

Mheshimiwa Spika, nikuthibitishie zaidi ya 70% ya dawa tunazo *MSD* na hatuna changamoto ya dawa. Hili nimefanya vikao vya kutosha na *MSD,* tumekwishakubaliana na tumekwishaweka *redline* kwa Mganga Mfawidhi wa Wilaya na Mkoa pamoja na vituo vya afya; wale ambao watakwenda kinyume na makubaliano tuliyokubaliana tutamweka pembeni, hakutakuwa na mjadala kwenye eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo eneo hili tunakwenda kulifanyia kazi kwa ufasaha kabisa, lakini hii tunaamini itakwenda kupunguza *over prescription*, matumizi yasiyo sahihi ya *brand, ghost dispensing* na mianya ya dawa kuingia kwenye mnyororo usio rasmi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *MSD* hadi kufikia mwezi Aprili, 2026 deni la *MSD* kwa upande wa utunzaji na usambazaji wa bidhaa za miradi Msonge, limefikia shilingi bilioni 220.6. Serikali kupitia Wizara ya Afya na Wizara ya Fedha inaandaa mpango maalum wa kulipa deni hili. Vituo vya kutolea huduma vimeelekezwa kuingia makubaliano na *MSD* ya kulipa madeni yao ikiwemo kupitia mifumo ya *NHIF*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wafamasia, Serikali inatambua kuwa mfamasia si mtunza *store* pekee. Mfamasia ni mtaalam wa matumizi sahihi ya dawa, ufuatiliaji wa *stock*, ushauri wa kitaalam na udhibiti wa rasilimali kubwa ya afya. Kutokana na maelekezo niliyoyatoa siku nilipofanya kikao *MSD* tarehe 28 Machi, 2026 Wizara imeshaanza kupitia miongozo, ili wafamasia wote wawe ni sehemu ya menejimenti katika hospitali na vituo na pendekezo la kuifanya famasia kuwa kurugenzi kamili, liko kwenye ngazi ya maamuzi sasa hivi tunavyozungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imepokea kwa uzito hoja ya kuimarisha uzalishaji wa ndani wa dawa, vifaa tiba na bidhaa za afya

nchini. Wizara itaendelea kuvutia wawekezaji, kuimarisha viwanda vilivyopo na kuhakikisha maamuzi ya Serikali yanazingatia ubora, yanazingatia usalama na thamani halisi ya fedha. Tumepokea maono na ushahidi uliotolewa na Mheshimiwa Shabiby. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimthibitishie nimekwishafanya vikao na wenzangu. Tunajua kwamba mchakato wa ujenzi wa viwanda vya dawa, Serikali inatamani kufanya, lakini wapo watu wasiolitakia mema Taifa hili, wamekuwa wao ndiyo kikwazo kikubwa cha kutotekelezwa uzalishaji wa dawa hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watu hawa hawalitakii mema Taifa hili. Ninataka nimthibitishie, tumekubaliana na wenzangu wa *MSD* kwa sababu orodha wanayo tutawafuatilia. Mchakato wa ujenzi wa viwanda vya dawa si maamuzi ya Mchengerwa. Mchakato wa ujenzi wa viwanda vya dawa si maamuzi ya Wizara ya Afya. Mchakato wa ujenzi wa Wizara ya Afya ni maamuzi ya mamlaka.

Mheshimiwa Spika, yeyote atakayejaribu kukwamisha mchakato huu, tutashughulika naye wala hatutamwacha. Hili ninalisema wazi kabisa, nimekwishasema mara kadhaa, hatutarudi nyuma hata kidogo. Haiwezekani kwa Taifa hili lenye miaka zaidi ya 60 bado tuko chini ya 16% ya uzalishaji wa dawa. Huku tukitambua changamoto tuliyoipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati wa *COVID-19* tulipata changamoto nyingi, lakini tunayo majanga chungu mzima ambayo yanaendelea katika dunia hii. Ni lazima tuzalishe dawa sisi wenyewe kama Taifa. Kwa hiyo, ninaomba nimthibitishie Mheshimiwa Shabiby niko imara, niko imara kweli kweli kwenye hili wala asiwe na wasiwasi.

Mheshimiwa Spika, ndani ya Serikali tumejipanga vizuri na nilipoingia katika Wizara hii, jambo la kwanza ambalo Mheshimiwa Rais alinikabidhi ni kuhusu uzalishaji wa dawa. Niliunda timu ambayo ilihusisha Wizara mbalimbali. Kwa maombi yangu, kwa mamlaka, mwenyewe Mheshimiwa Rais, lakini kwa maombi yangu kwa Waziri

Mkuu, tunao wataalam kutoka Wizara ya Viwanda, tunao wataalam kutoka *TRA* wapo kwenye Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimthibitishie hivi nimesimama, ndani ya miezi mitatu ya kutangaza mchakato wa kuanza kuzalisha dawa sisi wenyewe; juzi nimezindua *hub* ya Mloganzila ya uzalishaji wa dawa na tayari tumekwisha wakabidhi wawekezaji kutoka mataifa mbalimbali na tumekwisha saini hati ya makubaliano na kampuni kubwa duniani kutoka Ujerumani ya *Sartorius* ambayo kwa mara ya kwanza Taifa letu tutakwenda kuzalisha chanjo sisi wenyewe kama Taifa. Kwenye hili hatutarudi nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la mwongozo wa bei elekezi ya matibabu, Wizara inaendelea na zoezi la ukokotoaji wa gharama za huduma za afya kwa kuzingatia kitita cha Taifa cha huduma muhimu za afya. Katika kazi hii, Wizara inashirikiana na mshauri elekezi kutoka Shirika la Afya Duniani na kazi hiyo inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka huu. Matokeo yake yatasaidia kuweka bei elekezi zenye ushahidi, zinazolinda mwananchi na kuwezesha huduma kuwa endelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika *TEHAMA* bima ya afya kwa wote haiwezi kufanikiwa bila mfumo wa kidijitali unaosomana. Bila mfumo imara ongezeko hilo linaweza kuleta madai yasiyothibitishwa, udanganyifu, ucheleweshaji wa malipo na shinikizo la mfuko. Serikali imesimika afya *eHMS* katika Hospitali Za Rufaa na Mikoa, Kanda Maalum na Taifa na *GOTHOMIS* katika ngazi ya msingi.

Mheshimiwa Spika, Wizara pia imeanzisha *health data universal* kwa mara ya kwanza kabisa, tunakwenda kuanzisha kanzidata ya afya nchini, kwa mara ya kwanza kabisa, ili kuwezesha mifumo mbalimbali kusomana, kupokea na kutuma taarifa, kutoa rufaa kidijitali na kujenga misingi ya kanzidata ya kitaifa ya afya. Tunataka dai la bima lizaliwe kutoka huduma halisi iliyothibitishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na udanganyifu mkubwa. Labda niseme, kuna wakati wenzetu wa bima wamekuwa wakipokea

kila mwaka madai kutoka kwa mdau wetu wa afya mmoja ambaye aliwekeza shilingi 300,000,000 pekee lakini watu wa bima ya afya kutoka sehemu fulani, walikuwa wakimlipa huyo mwekezaji aliyewekeza kwenye kituo cha afya, ujenzi na vifaa kwa thamani ya shilingi 300,000,000. Kila mwaka alikuwa akilipwa shilingi 2,000,000,000. Sasa hili halikubaliki.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu tunatambua kwamba mchakato huu unahusisha mpaka watu wetu ndani ya Wizara, wataalamu huko kwenye mifumo, ndiyo maana tumeamua kuja na *robust system* ambao hautachezewa na hakutakuwa na Mtanzania mwenye uwezo wa kuuchezea. Tutakwenda kuokoa fedha, tutakwenda kusababisha *NHIF* iweze kuwa imara na iweze kudumu miaka na miaka.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunataka dai la bima lizaliwe kutoka huduma halisi iliyothibitishwa, dai lizaliwe kutoka *prescription* halali, rufaa izaliwe kutoka uamuzi wa kitabibu na malipo yawe *audited*, miundombinu, vipimo na rasilimali watu.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wamewasilisha hoja muhimu kuhusu miundombinu na watumishi. Serikali itaendelea kuimarisha huduma za msingi, hospitali ya wilaya, hospitali za rufaa na mikoa, hospitali za kanda na hospitali za Taifa ili kupunguza msongamano wa wagonjwa kutoka Muhimbili na kuongeza huduma za kibingwa karibu na wananchi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imepokea ushauri kutoka kwa Wabunge mbalimbali ambao wamechangia kuhusu eneo hili. Tutazingatia ushauri, tutazingatia maono yao Waheshimiwa Wabunge na yale ambayo wametamani tuyafanye katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wa Kanda ya Ziwa hasa kule Mkoa wa Mara tumewasikia. Mheshimiwa Waitara tumemsikia, Mheshimiwa Ghati na Mheshimiwa Dkt. Mahera tumewasikia. Ni lazima tuiboreshe hospitali hii ya Baba wa Taifa, hakuna mjadala kwenye hili.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**WAZIRI WA AFYA**: Mheshimiwa Spika, lazima twende kwenye hospitali zote zilizopo mipakani tukaziboreshe ili ziwe imara kwa sababu zitakwenda kuongeza utalii tiba, lakini zitakwenda kuimarisha utolewaji wa huduma za afya katika maeneo yetu na kule Rukwa Mheshimiwa Aeshi Hilaly. Nimekusikia na nimekwishatoa maelekezo ndani ya mwaka huu tutahakikisha huduma za *dialysis* zinafanyika katika Mkoa wa Rukwa pamoja na maoni yako, maono yako na ushauri wa Mheshimiwa Mzindakaya ambao ameutoa kwa Bunge hili na Serikali tumeusikia na tunakwenda kuufanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninatambua kwamba mambo ni mengi na bado Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumza mambo mazuri ikiwa ni pamoja na Mheshimiwa Erick Shigongo kuhusu vita ya homa ya ini. Tumelipokea hili, lakini kwa sababu ya muda tutatoa maelezo kwa maandishi kutokana na muda. Pia, Mheshimiwa Hokororo tunatambua kule Mtwara kuhusu ujenzi wa kituo cha afya, tumelipokea hilo. Pia na Waheshimiwa Wabunge wote wote ambao wamezungumza kwa niaba ya wananchi katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimalizie. Watanzania wanahitaji huduma bora za afya na kwenye hili hatuwezi ku-*compromise* hata kidogo na nimekwishawaeleza wenzangu, wakati huu ni lazima tufanye kazi kama mchwa. Sisi tuliyopata bahati ya kusimama na kuteuliwa kwenye vyeo mbalimbali tunao Watanzania zaidi ya milioni 60 wenye uwezo mkubwa. Sisi tuliopata bahati ni lazima tufanye kazi kwa bidii, hakuna mjadala kwenye hili, hakuna mjadala hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nikiri kwamba hoja zote ambazo zimetolewa zina umuhimu na kwa niaba ya Wizara ya Afya ninawashukuru tena Waheshimiwa Wabunge kwa maoni kwa ushauri wao na hoja zao. Ninaomba Bunge lako Tukufu liendelee kuiunga mkono Wizara ya Afya katika utekelezaji wa bajeti hii, kwa sababu

tunachokifanya si kazi ya mwaka mmoja ni kuweka misingi ya historia mpya ya afya nchini. Historia hii itakumbukwa kama kizazi kilichoamua kwamba afya ya Mtanzania isiwe bahati, afya ya Mtanzania isiwe hisani, isiwe uwezo wa mfukoni pekee bali ni haki inayolindwa na mfumo imara wenye utu, teknolojia, nidhamu na uwajibikaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa nafasi hii, ninaomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Katibu

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**KITABU CHA PILI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 52 – Wizara ya Afya**

Kifungu 1001 – *Administration Human Resources Management*……………….…..Sh.11,537,429,000

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Kifungu hiki ni cha mshahara na nina watu watatu, Tunaanza na Mheshimiwa Ado.

**MHE. ADO S. ADO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kuniona, ninasimama chini cha Kifungu cha 125 cha kanuni zetu,

nikitaka maelezo ya nyongeza juu ya suala la uwekezaji wetu katika Mradi wa Muhimbili mpya. Ninaomba, iingie kwenye rekodi kwamba, mimi sipingi uwekezaji katika Hospitali yetu ya Taifa ya Muhimbili. Ninasema hivyo kwa sababu hali ya Muhimbili ninaifahamu, ni hali inayosikitisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu mimi iko *centred* katika 1.2 *trilion*. Ninataka maelezo ya ziada, kwa nini Wizara imechukua *approach* ya kuwekeza fedha zote hizi shilingi trilioni 1.2 katika Mradi wa Muhimbili mpya badala ya kuzigawanya ili sehemu ya fedha hizi ambao ni uwekezaji mkubwa sana katika historia ya *financing* yetu katika hospitali, ili nyingine ziende zikawekezwe katika hospitali zetu za rufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo ambalo ninataka ufafanuzi wa zaida, hasa ikizingatiwa kwamba sehemu kubwa ya fedha hizi, kama ambavyo Wizara yenyewe imesema ni fedha ambazo zitalipwa na Watanzania kwa sababu ni fedha za mkopo. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, ninaomba kumjibu Mheshimiwa Ado Shaibu. Kwanza nishukuru kwa hoja yako, lakini ninaomba nitoe ufafanuzi kidogo. Ujenzi wa Muhimbili mpya ni ujenzi ambao mchakato wake ulianza mwaka 2018 na ilipofika 2020 wafadhili ndipo walipokubali andiko hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na maandiko 14 nchi nzima kwa ajili ya uwekezaji wa Muhimbili mpya, lakini yaliyopita viwango ni maandiko matatu ikiwemo ujenzi wa Muhimbili mpya. Kwa hiyo, uwekezaji wa Muhimbili mpya hauna *alternative* kwamba ubadilishe andiko ukagawanye gawanye ukajenge hospitali za kanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkopo huo ni Dola za Kimarekani 363,000,000 takribani shilingi 900,000,000,000/= na Nchi ya Tanzania itachangia shilingi 104,000,000. Kwa hiyo, unapata ile trilioni 1.2 kwa

mchango wa mkopo na mchango wa Serikali. Lakini mchango wa Serikali ni wa dola milioni 104 siyo *cash,* ni msamaha wa kodi wa gharama zile za vifaa vya uwekezaji ule. Katika hiyo shilingi 363,000,000,000 ya mkopo, ziko shilingi 60,000,000 ambazo ni za dharura, ambazo zitatumika tu pale ambapo kutatokea changamoto na ujenzi huo wa Muhimbili mpya utachukua miaka mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wajenzi wa ujenzi huo ni watoa mkopo *South Korea*. Kwa hiyo, mkopo huo utakuja kwa awamu kila mwaka, kila mwaka. Kwa hiyo, ukigawa pale kwenye ile shilingi 900,000,000,000 ni kama shilingi 170,000,000 mpaka 200,000,000 kwa mwaka. Kwa hiyo, Mheshimiwa Ado Shaibu, hatuna *alternative* ya kubadilisha na ninaomba nimthibitishie; tuna Hospitali ya Taifa moja tu ambayo ni Muhimbili ambayo ina miaka 120, imejengwa mwaka 1905.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wathamini pia waliona kwamba, tukiendelea na ukarabati wa Muhimbili kila mwaka ambao unatumia zaidi ya shilingi 7,000,000,000, ni hasara zaidi. Ndiyo maana Serikali kwa kuona umuhimu huo wa kuendelea ku-*save* pesa ikaona ni bora iwekeze, ili kuepusha zile gharama za ukarabati wa kila mwaka. Mheshimiwa Mbunge ujenzi huu wa Muhimbili una faida kubwa sana. Kwanza, ujenzi huo unaenda na ujenzi wa hospitali, kuweka vifaa tiba vya kisasa vyote lakini na kujenga mfumo wa kuendeshea hospitali. Gharama yote hiyo milioni 363 ya Dola za Kimarekani iko *included*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge baada ya ujenzi huo, kwanza tutaondoa kabisa ile Muhimbili kusambaa. Muhimbili imesambaa, inashindwa kupata ithibati ya kimataifa kwa sababu imesambaa na miundombinu ni chakavu. Sasa madaktari wetu bingwa wataenda kutoa huduma kwenye hospitali ya kisasa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sasa hospitali hii, itaenda kuingiza mapato kwa sababu huduma zote za kibingwa na kibingwa bobezi zinazotolewa mbali zitafanyika, lakini wataalam wetu ambao ni mabingwa kabisa, wataonesha uwezo wao kwa sababu wana miundombinu wezeshi, wataalam wetu watatoa ubingwa bobezi kwa

sababu sasa wana vifaa vya kuwawezesha kufanya hizo huduma. Kwa hiyo, ninaomba Mheshimiwa Ado Shaibu, aridhie tuweze kupata hospitali hiyo ili tuweze kuboresha huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo mazuri kabisa ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninaomba nimfahamishe mdogo wangu Ado kwamba, ujenzi wa Muhimbili hauisimamishi Serikali kuendelea kuboresha hospitali zote nchini. Tunatamani Wizara ya Afya siku moja Benjamini Mkapa pia iwe Hospitali ya Taifa kwa sababu ya maboresho makubwa ambayo yanaendelea, tunaendelea na ujenzi wa hospitali za mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshasema hapa katika bajeti hii, tuna nyongeza ya fedha ambayo tunapeleka kwenye hospitali za rufaa katika maeneo mengi nchini. Nimekwishazitaja baadhi; Rukwa; kule kwa Mwalimu Nyerere, Mara; nimetaja Kagera, tunaenda kujenga hospitali mpya kabisa katika Mkoa wa Kagera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi juzi tumepeleka shilingi bilioni 25,000,000,000 ujenzi wa Hospitali ya Sekou Toure pale Mwanza, tunaendelea katika kanda zetu zote. Tunataka kuwaambia Watanzania kwenye kanda zote kwamba, Muhimbili haitasimamisha maboresho katika hospitali nyingine zote kote nchini, haitasimamisha maboresho kwenye vituo vya afya kwenye zahanati zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira hii ya Rais Mheshimiwa Dkt. Samia iko wazi, nimesema hapa kwamba, ndani ya miaka minne amejenga vituo vya afya 3,530 na kwa sasa pia tumeweka kwenye mpango, Wizara ya Afya kwa kushirikiana na TAMISEMI tutaendelea kuzijenga na tutazijenga nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu wazi kwamba hakuna Mtanzania atakayeweza kutuzuia kuijenga Muhimbili, hayupo.

Tutaendelea na ujenzi wa Muhimbili. Kwa sababu tunajua kwamba tutakapomaliza ujenzi huu, hawa hawa wanaopinga, ndiyo watakuwa wa kwanza kwenda kuhudumiwa pale. Kama ilivyokuwa *SGR*, kama ilivyokuwa Bwawa la Mwalimu Nyerere, kama ilivyokuwa ununuzi wa ndege, kama ilivyokuwa ujenzi wa meli mpya kule Ziwa Victoria, ujenzi wa Daraja la Dkt. John Joseph Pombe Magufuli na mambo mengi kadha wa kadha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili lina umuhimu kwa Taifa letu, Muhimbili imejengwa ina miaka 125 hivi tumesimama. Ni lazima tuiboreshe tuweze kuijenga kwa maslahi ya Taifa la Tanzania. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kuzungumza muda wa kipindi hiki, mwenye mamlaka ni Spika. Tunawaacha wazungumze kwa kirefu, ili Wabunge muelewe na wananchi waelewe nia njema ya Serikali. Natumaini Mheshimiwa Ado umeelewa vizuri sasa, umeelewa? Usisimame wewe, sema tu ndiyo au bado!

**MHE. ADO S. ADO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimekuelewa.

**MWENYEKITI:** Umeelewa, basi kaa chini. Hiyo hospitali unajua ilianza na jina gani? Hiyo hospitali ilivyojengwa ilianza na jina gani, *Princess Magreth!*

Mheshimiwa Kijakazi Yunus.

**MHE. KIJAKAZI Y. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Tunatambua jitihada za Serikali, imefanya kazi kubwa sana kuhakikisha kwamba, inafikisha huduma za afya kwa wananchi kwa kujenga hospitali za wilaya, hospitali za mikoa, za rufaa na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo changamoto mbalimbali za miundombinu kwenye baadhi ya Mikoa kama Morogoro, Lindi na Kagera. Katika hospitali za wilaya na za mikoa kuna changamoto ya mtambo wa kuchakata *oxygen,* ambapo kwenye baadhi ya maeneo kama vile Morogoro na Lindi mitambo hii imejengwa, lakini

kinakosekana kifaa kidogo cha kutoa *oxygen* kwenye mtambo kwenda kwenye mitungi, hali hii imedumu kwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kauli ya Serikali kuhusiana na hili kuhakikisha kwamba, huduma hii muhimu kwa afya yetu sisi Watanzania inaweza kupatikana katika maeneo yote, hospitali za wilaya na hospitali za mikoa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa *concern* yake. Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amejenga miundombinu ya *oxygen* katika hospitali zetu. Changamoto hii ya hiyo *capacity,* ambayo inasababisha *oxygen* isiende sawa tumeiona. Tumerejea kwenye mkataba, ninaomba niwathibitishie Waheshimiwa Wabunge, yale maeneo yote ambayo mitambo ya *oxygen* ni mikubwa, lakini *transformer* ni ndogo, tunaenda kurudia na kuweka *transformer* ambayo itakidhi ukubwa wa mitambo hiyo, ili *oxygen* iweze kupatikana kwa wagonjwa wote nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumelifanyia kazi na tutabadilisha *transformer* katika maeneo yote yenye changamoto. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Eric Shigongo.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo nia yangu kukwamisha bajeti hii, lakini kuna mambo ambayo wananchi wanahitaji kupata ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Mchengerwa ni mtu mwema, Naibu wake ni mtu mwema, Katibu Mkuu wake pia ni mtu mwema, lakini jambo hili la homa ya ini linahitaji ufafanuzi kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kasi ya maambukizi kwa hivi sasa ni asilimia nne mpaka nane, ni kasi kubwa sana. Watu wengi hawajapima, ni asilimia tano tu ndiyo wamepima katika nchi hii na

kuwa *diagnostic* na asilimia moja tu ya watu wako kwenye matibabu. Watu ambao wameambukizwa 25% yao wana hatari ya kuharibika kwa ini na 10% wanaweza wakapata kansa ya ini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninahitaji ufafanuzi wa Mheshimiwa Waziri na Wizara na *commitment*. Upi mpango wa Serikali kuhusu elimu, upimaji na matibabu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili la muhimu zaidi ni kuhusu chanjo. Nimezungumza kuhusu chanjo hapa kwa takwimu za mwaka 2025…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shigongo, jielekeze kwenye hoja moja tu, usifanye hoja mbili. Hoja moja tu.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa. Mwaka 2025 walizaliwa watoto takribani 2,000,000 katika nchi hii. Asilimia 4.7 ya akina mama katika nchi hii waligundulika wameambukizwa magonjwa haya, hivyo watoto karibu 100,000 walikuwa wanakadiriwa kwamba, wanaweza kuwa na maambukizi, ambapo kati yao asilimia tisa hadi 10%, kwa maana ya kwamba, kila mwaka tunapata watoto takribani 10,000 wanaambukizwa ugonjwa huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chanjo inayotolewa na Serikali inatolewa kwenye wiki sita baada ya mtoto kuzaliwa. Kuanzia umri wa *zero* mpaka wiki sita haitolewi chanjo yoyote. Ninahitaji kupata *commitment* na ufafanuzi wa Serikali, upi mpango wa Serikali kwenye bajeti hii kuwachanja watoto kwa chanjo ya *Monovalent* kuanzia siku ya kuzaliwa mpaka wiki sita? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Kwanza ninaanza kumpongeza Mheshimiwa Eric Shigongo, ambaye ni Mjumbe wa Kamati na hoja yake hii imekuwa ni ya kudumu kwenye Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, homa ya ini tunayo katika nchi yetu. Mwaka 2002 Serikali iliona umuhimu wa kuanza chanjo ya watoto, ambayo ni *Pentavalent*. Chanjo hiyo inatolewa wiki sita, wiki 10 na wiki 14 kwa hiyo, watoto wote waliozaliwa mwaka 2002 mpaka leo wamechanjwa chanjo ya *Pentavalent*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo *concern* ambayo anayo Mheshimiwa Mbunge na ni halisia na sisi, kama Serikali, tumeiona. Maambukizi kutoka kwa mama na mtoto yapo kama hakuna huduma zilizotolewa, kwa hiyo, Serikali sikivu ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan tayari imeweka mpango wa kuanza chanjo ya mtoto baada ya kuzaliwa ndani ya saa 24 *(Birth Dosage)*. Kwa bajeti hii tunayoipitisha Serikali imetenga shilingi 38,000,000,000, ili tuweze kuanza chanjo ya *Birth Dosage*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, chanjo hiyo tutakwenda kuungana na Gavi ambao wamekuwa wanatupatia chanjo. Dirisha la kuomba chanjo hiyo linafunguliwa Mwezi Juni kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, tumejipanga kwenda kuanza hiyo chanjo pale dirisha litakapofunguliwa na Gavi. Sisi tumeanza maandalizi kuimarisha mfumo wa *Cold Chain Supply,* usambazaji wa chanjo, kwa kununua majokofu, kutoa elimu kwa sababu, ni chanjo mpya. Chanjo ile ya *Pentavalent* itaendelea kwa hiyo, *Birth Dosage* inakwenda kuanza kwenye Bajeti hii ya Mwaka wa Fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Serikali yetu ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imejipanga kuendelea kupambana na homa ya ini. Tuna chanjo ya watu wazima, ambayo wanapata dozi tatu, kwa ajili ya kujikinga na homa ya ini. Kwa hiyo, homa ya ini ipo na Serikali inaendelea kutoa chanjo. Watumishi wa Afya wote wanapewa chanjo hii bure kwa sababu, wao ni *at risk,* ili wasiendelee kupata huo ugonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia imelipatia umuhimu suala hili la ugonjwa huu wa homa ya ini. Mwaka 2023 iliamua kuunganisha huduma, kwa maana ya kubadilisha *NACP* kusimamia UKIMWI tu na sasa homa ya ini pamoja na magonjwa ya

zinaa. Kwa hiyo, Serikali imeona umuhimu wa kuendelea kuwakinga Watanzania ndiyo maana imeliwekea gonjwa hili umuhimu wake. Tunaendelea kutoa elimu kwa Watanzania kupitia njia mbalimbali, vyombo vya habari, matamasha kila mwezi Julai na tuna Siku ya Homa ya Ini Duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninatoa wito kwa Watanzania wote na kuwaambia kwamba, homa ya ini ipo na inaua. Njia ni zilezile ambazo tunaambukizwa UKIMWI na homa ya ini ni vilevile. Kwa hiyo tuepuke hizo njia ambazo zinaambukiza magonjwa hayo. Ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 52 – Wizara ya Afya**

Kifungu 1001 – *Administration Human Resources Management*……………………………...Sh. 11,537,429,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*……………....Sh. 1,849,660,430
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*………………......Sh. 2,330,435,724
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*…………………………….Sh. 826,347,698
Kifungu 1005 – *Government Communication Unit*.........…Sh. 515,811,000
Kifungu 1006 – *Procurement Management Unit*………...Sh. 1,552,466,790
Kifungu 1007 – *Legal Services Unit*…………………………..Sh. 496,658,728
Kifungu 1008 – *Information and Communication Technology Unit*……………………………….Sh. 629,016,974
Kifungu 1009 – *Monitoring and Evaluation*………..……...…Sh. 911,865,000
Kifungu 2001 – *Curative Services*……………………….Sh. 533,122,695,842
Kifungu 2003 – *Chief Medical Officer*……………………Sh. 24,864,393,018
Kifungu 2004 – *Nursing and Midwifery Services Division*……………………………………......Sh. 972,343,093
Kifungu 2005 – *Pharmaceutical Services Unit*……………Sh. 1,591,492,076
Kifungu 2006 – *Diagnostic and Health Care*

*Technology Services Unit*…………...…...Sh. 10,826,466,336
Kifungu 3001 – *Preventive Services*……………………..Sh. 27,998,640,790
Kifungu 3002 – *Health Quality Assurance Division*………...Sh. 862,925,000
Kifungu 3003 – *Health Emergency Preparedness*
*Response Unit*…….…………………………Sh. 1,243,639,391
Kifungu 3004 – *Reproductive, Maternal & Child*
*Health Division*...……………………………Sh. 1,876,230,514
Kifungu 5001 – *Human Resource Development*……….Sh. 28,228,353,596

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA NNE**

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 52 – Wizara ya Afya**

Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*………………...Sh. 50,154,552,000
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*..……………………..……………….Sh. 0
Kifungu 1008 – *Information and Communication*
*Technology Unit*…………………………………………..…Sh. 0
Kifungu 1009 – *Monitoring and Evaluation Unit*…..........Sh. 1,078,825,000
Kifungu 2001 – *Curative Services*…….……………….....Sh. 239,488,774,527
Kifungu 2003 – *Chief Medical Officer*.…………………Sh. 138,193,822,569
Kifungu 2005 – *Pharmaceutical Services Unit*..………Sh. 459,988,800,000
Kifungu 2006 – *Diagnostic and Health Care*
*Technical Services Unit*…………..……...Sh. 14,500,000,000
Kifungu 3001 – *Preventive Services*…..…………………Sh. 165,120,412,904
Kifungu 3003 – *Health Emergency Preparedness*
*Response Unit*…….…………………………Sh. 5,000,000,000
Kifungu 3004 – *Reproductive, Maternal & Child*
*Health Division*...………………………...Sh. 46,500,000,000
Kifungu 5001 – *Human Resource Development*……....Sh. 28,000,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. HUSSEIN ATHUMANI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Hapa Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Mtoa hoja, Taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 126(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Agosti 2025, ninaomba kutoa Taarifa kwamba, Bunge lako limekaa kama Kamati ya Matumizi limekamilisha kazi zake. Ninaomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

**SPIKA:** Hoja imeungwa mkono. Sasa nitawahoji kuhusu hoja ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Walioafiki wameshinda. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 Yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninachukua nafasi hii, kwanza kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri, Naibu wako na wataalam wetu. Kwa kweli wataalam hawa wamejitoa, wanafanya kazi kwa moyo mmoja; Hospitali yetu ya *JKCI,* Muhimbili, *Ocean Road, MOI* na Benjamin-Dodoma wanafanya kazi ya utaalam wa juu. Wanavutia wagonjwa kutoka nchi za jirani na mpaka mwisho wanaulizwa kwa nini uko hapa? Njoo kwetu ufanye kazi, wameamua kubaki Tanzania kwa sababu ya kulipenda Taifa lao.

Hospitali zote, ukienda *JKCI* mitambo ya kisasa, Muhimbili, Benjamin, *Ocean Road* na *MOI;* Mbunge mmoja amezungumza hapa kuhusu mtambo wa *Ocean Road,* unaitwa *PET (Positron Emission Tomography)*. Ukiingia ndani, ukitoka unakwambia wewe utapata kansa baada ya miaka miwili au mitatu au wewe hupati kansa, Mungu amekujalia. Hizi ndizo kazi za Rais Samia, kujali maisha ya Watanzania. *(Makofi)*

Faida za hizi hospitali zetu na utalii kutoka nje, wa hospitali, ni mapato ya Taifa, ajira. Sifa ya nchi kwenye masuala ya kiafya inavutia uwekezaji na watu kutaka kuingia ubia na hospitali zetu kutokana na ubora na uwezo wa hospitali. Hongereni sana wataalam wetu. Hospitali za wilaya, nitaizungumzia yangu ya Amana na Mnazi Mmoja, kwa kweli, wanafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, Wabunge wengi wamezungumza kuhusu Bima ya Afya. Maelekezo yangu ni Wizara ya Afya na Wizara ya Fedha zikutane na Kamati ya Bajeti kesho tumalize huu mzozo wa Bima ya Afya, tutoke hapo na *solution* moja ya kusaidia nchi ipate mapato ya kutibu wagonjwa kwa Bima ya Afya. Wabunge na wananchi tumesomewa misamaha ya matibabu ya hospitali zote, ninafikiri ni takribani shilingi 60,000,000,000 na 80,000,000,000 ambazo Serikali itakuja kufidia. Hii yote ni kuwapa afuaeni ya afya Watanzania kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Pamoja na maelekezo, madaktari wetu wana moyo mkubwa wa kuwasaidia wagonjwa wetu. Ninawapongeza tena wataalam wetu,

wauguzi wote na mabingwa wote kwa sababu, kuna neno la kizungu linaitwa *agility*, *dedication*, *consistency* na mapenzi. Mnafanya kazi na raha yake mmetupatia sisi wagonjwa wenu, wataalam wetu wengine mko hapo juu, wengine wako hospitali; furaha kama goli la Clatous Chama. Huo ndiyo ukweli kwa hiyo, madaktari wetu mabingwa tunawashukuru sana kwa kazi nzuri mnayoifanya; wote mliokuja na ambao hawakuja mmewawakilisha.

Baada ya maneno haya, ninaahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho, Saa 3.00 Asubuhi.

*(Saa 1.19 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 13 Mei, 2026, Saa Tatu Asubuhi)*